# Nipashe

Jumatano Mei 29, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579930

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Nyalandu apata dhamana baada ya kulala mahabusu

UKURASA 3






Wajumbe Baraza la Wawakilishi wamlilia Ali Juma Shamuhuna
Ukurasa 15

Rais Mutharika achaguliwa baada ya kushinda kesi katika mahakama
Ukurasa 17

siasa

JUMATANO MEI 29, 2019
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Changamoto za ANC na hatima ya 'vyama tawala' barani Afrika
Ukurasa 18

Hukumu ya Mahakama kubatilisha wakurugenzi kusimamia uchaguzi

• Wangwe asema Mahakama imetenda haki • Ataka wenye dukuduku wasikae kimya, wakimbilie mahakamani

Na Enock Charles

HIVI karibuni, Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, ilitoa hukumu iliyobatilisha Wakurugenzi wa Halmashauri nchini kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Hiyo inafuatia kesi Namba 8/2018, iliyofunguliwa na mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Bob Chacha Wangwe ya kupinga wakurugenzi wa majiji, manispaa na halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Katika kesi hiyo Wangwe aliwakilishwa na wakili wa kujitegemea Fatma Karume.

Hukumu hiyo imevuta hisia za watu wengi na kuripotiwa hata na vyombo vya habari vya kimataifa, kama vile BBC na DW.

Nipashe kupitia kwa mwandishi wake ilifanya mahojiano maalumu na Wangwe aliyefungua kesi hiyo katika Mahakama Kuu. Yafuatayo ni mahojiano hayo:

**SWALI: KESI ya Kikatiba uliyofungua Mahakama Kuu ya Tanzania kuhusu uhalali wa Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, halmashauri kusi-**

INAENDELEA UK.16

Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam. PICHA: MTANDAO

ICC na tishio la kujitoa uanachama
Ukurasa 20

ACT-Wazalendo: Ukawa ni wenzetu lakini... Ukurasa 19

UKURASA 13

# Dereva teksi kortini tuhuma kumteka MO

UKURASA 2



Mshtakiwa Mousa Khamis Twaleb akiwa chini ya ulinzi wa polisi, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka matatu likiwamo la utekaji nyara mfanyabiashara maarufu nchini, Mohamed Dewji 'MO'. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Kada wa CCM mbaroni madai ya wizi bastola

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MAGUFULI AWAENZI MASHUJAA NAMIBIA**

RAIS John Magufuli jana alitembelea na kuweka shada la maua katika eneo la mashujaa waliopigania ukombozi wa Namibia...

UKURASA WA 5

**CWT YAJA JUU WALIMU KUJERUHIWA, KUPORWA**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) mkoani Katavi, kimelaani kitendo cha watu wasiojulikana kuwavamia walimu...

## Waziri atamba kukoma mgawo umeme

UKURASA 3

**MICHEZO** NDEMLA AZISUBIRISHA KWANZA SIMBA, YANGA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Dereva teksi kortini tuhuma kumteka MO

**Na Hellen Mwango**

DEREVA teksi mkazi wa Tegeta, Mousa Twaleb (46), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, akikabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi ikiwamo kusaidia kutendeka uhalifu, kutakatisha Sh. milioni nane na kumteka Mohamed Dewji maarufu kama MO.

Twaleb alisomewa mashtaka yake jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi na Wakili wa Serikali Wankyo Simon.

Kadushi alidai kuwa kati ya Mei Mosi na Oktoba 10, 2018, mahali tofauti jijini Dar es Salaam na jijini Johannesburg nchini Afrika Kusini, kwa makusudi alisaidia utendaji makosa ya jinai kwa nia ya kujipatia fedha.

Shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Oktoba 11, 2018 katika hoteli ya Colloseum iliyopo Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa pamoja na wenzake ambao hawapo mahakamani walimteka MO kwa nia ya kumuhifadhi kwa siri.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 249 cha kanuni ya adhabu cha 16 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2002 kilichotumika kufungua shtaka ya kumteka MO endapo mshtakiwa atakutwa na hatia atahukumiwa kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka saba.

Wankyo alidai katika shtaka la tatu kuwa, Julai 10, 2018 eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam mshtakiwa alitakatisha Sh. 8,000,000 huku akijua zimetokana na genge la uhalifu wa makosa ya kupanga.

Hakimu alisema mshtakiwa hatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Kadushi alidai kuwa upelelezi umekamilika sehemu kubwa na kwamba wanamalizia maeneo machache ili kesi ianze kusikilizwa.

Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itatajwa Juni 11, mwaka huu na mshtakiwa apelekwe mahabusu.



Rais Dk. John Magufuli akisali mbele ya makaburi ya mashujaa wa Namibia yaliyopo katika eneo la Heroes' Acre, nchini humo jana, baada ya kuweka shada la maua. **PICHA: IKULU**

# Kada wa CCM mbaroni tuhuma wizi wa bastola

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

JESHI la Polisi mkoani hapa linamshikilia mtuhumiwa wa ujambazi sugu, Jumanne Mjuzi, mkazi wa Ngarenaro jijini Arusha ambaye pia ni kada maarufu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa kosa la kuvunja na kuiba vitu mbalimbali ikiwamo bastola.

Jeshi la Polisi limesema kuwa bastola hiyo ilikuwa na risasi tisa.

Imeelezwa kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa Mei 16, mwaka huu, saa 11 jioni, baada ya kuvamia na kuvunja nyumba ya mkazi mmoja wa eneo la Olasiva, Msafiri Msuya.

Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Jonathan Shana, aliviambia vyombo vya habari kuwa mtuhumiwa huyo alifanikiwa kupora Sh.milioni sita, kompyuta mpakato (laptop) na bastola aina ya Browning ikiwa na risasi tisa zilizokuwa kwenye begi mali ya Msafiri Msuya.

"Baada ya kupata taarifa hiyo Jeshi la Polisi kupitia askari wenye weledi walifanikiwa kufanya msako na ndani ya saa 48... tulifanikiwa kumtia mbaroni mhusika pamoja na vitu alivyopora," alisema Kamanda Shana.

Mtuhumiwa huyo miaka ya nyuma aliwahi kukimbilia bungeni kwa nia ya kujisalimisha kutokana na kusakwa na kufuatia matukio ya uhalifu yaliyokuwa akidaiwa kuhusika jijini hapa, na baada ya kukiri makosa, aliapa kutoyarudia.

Hata hivyo, mara kadhaa amekuwa akihusishwa na matukio ya uporaji na kufikishwa kituo cha polisi na kukataa kuwa amestaafu ujambazi.

Mjuzi alikuwa kada maarufu wa CCM ambaye alishiriki kwenye uchaguzi mbalimbali wa marudio kama kiongozi wa kikosi maalumu cha ulinzi.

Wakati huo huo watu 35 wamekamatwa na polisi, wakihusishwa na matukio ya uhalifu katika operesheni ya polisi inayoendelea.

Katika msako huo vitu mbalimbali zikiwamo televisheni flat, laptop, sabufa, spika vilikamatwa na watuhumiwa wanashikiliwa kupisha upelelezi kukamilika wafikishwe mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

# JPM awaenzi mashujaa Namibia

**Na Mwandishi Wetu, WINDHOEK**

RAIS John Magufuli jana alitembelea na kuweka shada la maua katika eneo la mashujaa walioigania ukombozi wa Namibia, lililoko nje kidogo ya Jiji la Windhoek, nchini hapo.

Katika eneo hilo, wamezikwa mashujaa wa ukombozi wa Namibia ambao baadhi yao walipata mafunzo katika kambi ya Kongwa nchini Tanzania. Wengine walikuwa maofisa wa Chama cha SWAPO ambacho ofisi zake zilikuwa jijini Dar es Salaam na wengine ni viongozi wakuu walioendesha mapambano wakiwa nchini Namibia.

Baadhi ya mashujaa waliozikwa katika eneo hilo ni Ndimo Hamaambo, Peter Nanyemba, Theo-Ben Gurirabo na Toivo ya Toive.

Katika ziara ya kuweka shada eneo hilo, Rais Magufuli aliongozana na mwenyeji wake, Rais Hage Geingob.

Rais Magufuli pia alitembelea kiwanda cha kusindika nyama cha kampuni ya Meatco kilichoko jijini Windhoek na kuelezwa na Kaimu Mtendaji Mkuu wake, Jannie Breytenbach, kuwa kiwanda kina uwezo wa kuchinja ng'ombe 630 kwa siku, kimeajiri wafanyakazi 650 na kwamba kampuni hiyo iko tayari kushirikiana na Tanzania kuanzisha viwanda vya nyama.

Baada ya kutembelea kiwanda hicho, Rais Magufuli alisema Tanzania ni nchi ya pili kwa idadi kubwa ya mifugo barani Afrika na aliikaribisha kampuni ya Meatco kuwekeza nchini Tanzania.

Katika ziara hiyo, Rais Magufuli ameongozana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi.

Kabla ya kuondoka nchini Namibia kwenda nchini Zimbabwe ambako anakwenda kufanya ziara rasmi ya kitaifa kwa mwaliko wa Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, Rais Magufuli alikutana na kufanya mazungumzo na Rais mstaafu wa pili wa Namibia, Hifikepunye Pohamba, jijini hapa.



## HABARI KITAIFA



Baadhi ya malori ya mizigo yakiwa kwenye foleni yakisubiri kupimwa kwenye mzani Barabara ya Mandela, eneo la Kurasini jijini Dar es Salaam jana. Wamiliki wa ofisi jirani na mzani huo, wamelalamikia usumbufu na kushindwa kuingia kazini kwa wakati kutokana na foleni hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Nyalandu atoka mahabusu kwa dhamana



**Na Romana Mallya**

ALIYEKUWA Waziri wa Maliasili na Utalii, kwenye utawala wa awamu ya nne, Lazaro Nyalandu, ameachiwa kwa dhamana ya Sh. milioni 15 baada ya kukaa mahabusu kwa usiku mmoja.

Nyalandu ambaye kwa sasa ni kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), aliachiwa jana kwa sharti la kuwa na wadhamini watatu ambao kila mmoja amemdhamini kwa Sh. milioni tano.

Nyalandu pia na watu wengine wawili, Peter Jambi na David Jumbe, wanatuhumiwa kufanya mkutano bila kibali ambao nao wamedhaminiwa na wadhamini wawili wawili kwa kila mmoja kutakiwa kuwa na Sh. milioni tano hivyo kufanya dhamana yao kufikia Sh milioni 20.

Nyalandu alikamatwa juzi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Singida, baada ya kushukiwa kuwapo kwa viashiria vya rushwa kwenye mkutano wa chama hicho uliokuwa ukifanyika mkoani humo.

Msemaji wa Chadema, Tumaini Makene, alisema jana kuwa Nyalandu na wenzake wawili walihojiwa na polisi kwa madai ya kufanya mkutano bila kibali.

Makene alisema Nyalandu na wenzake wawili waliachiwa kwa dhamana ya polisi mkoa wa Singida.

"Baada ya kuhojiwa leo (jana) Nyalandu amedhaminiwa kwa masharti ya kuwa na wadhamini watatu ambao kila mmoja amemdhamini kwa Sh. milioni tano. Wenzake wawili wamedhaminiwa na wadhamini wawili wawili kwa dhamana ya Sh. milioni tano kwa kila mdhamini," alisema.

Makene alisema Nyalandu na wenzake wametakiwa kuripoti polisi leo asubuhi.

Awali, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Singida, Joshua Msuya, aliiambia Nipashe kuwa walikwenda kumkamata Nyalandu baada ya taarifa za kuwapo kwa vitendo vya rushwa kwenye mkutano huo lakini Takukuru bado inachunguza tuhuma hizo kupata ukweli.

"Baada ya watu wa Takukuru kufika kwenye mkutano wa Chadema, walijitambulisha na Nyalandu hakupanda gari letu, aliendesha gari lake hadi Takukuru ambako alihojiwa kuhusiana na tukio la rushwa na tulimuachia wakati tunaendelea na uchunguzi," alisema.

Pia alisema Nyalandu alihusika na kufanya mkutano wa nyumba kwa nyumba bila kibali ndiyo maana baada ya kutoka Takukuru alikabidhiwa kwa Jeshi la Polisi ambalo ndilo lenye dhamana ya kuchunguza tukio hilo.

# Watano zaidi watumbuliwa umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amewasimamisha kazi watumishi watano wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili kupisha uchunguzi dhidi yao.

Taarifa iliyotolewa jana na wizara hiyo iliwataja watumishi waliosimamishwa kazi ni Mhandisi Naomi Mcharo, Robert Fundi, Doris Sendewa, Mohamed Mchemi na Mujuberi Masatu.

Hasunga alisema watumishi hao wamesimamishwa kazi kutokana na taarifa za awali za uchunguzi wa kamati iliyoundwa na ofisi ya Waziri Mkuu kubaini udhaifu wa kiutendaji ndani ya tume hiyo ikiwamo matumizi mabaya ya fedha za miradi, matumizi mabaya ya madaraka, upendeleo na kukosa umakini katika ujenzi wa miradi ya umwagiliaji.

Alisema watumishi hao watano wataungana na watumishi wengine waliosimamishwa kazi hivi karibuni na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Mei 14, mwaka huu, Waziri Mkuu Majaliwa, alitangaza kuwasimamisha kazi wakurugenzi saba wa tume hiyo akiwamo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji ili kupisha uchunguzi wa tuhuma mbalimbali zinazowakabili.

Sambamba na kuwasimamisha, Majaliwa alimwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye haraka uchunguzi wa kina, ili kujua ni nani alikuwa mlango wa ubadhirifu huo.

Waziri Mkuu alichukua hatua hiyo wakati wa kikao na viongozi wa tume hiyo kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Hazina, jijini Dodoma na kuhudhuriwa na mawaziri, manaibu waziri na makatibu wakuu.

Mbali na kuwasimamisha kazi wakurugenzi hao, pia Waziri Mkuu aliagiza watumishi wengine 21 wa tume hiyo wachukuliwe hatua za kinidhamu kutokana na utendaji usiori-

INAENDELEA UK 8

# Waziri ajivunia kutokuwa na mgawo umeme mwaka huu

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema wizara yake inajivunia kuliwezesha taifa kutokuwa na mgawo wa umeme katika mwaka huu wa fedha.

Amesema mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya uzalishaji umeme ambayo kwa sasa Tanzania imekuwa na ziada ya MW 300 kwa siku, tofauti na upungufu wa MW 100, uliokuwapo nchini mwaka 2015.

Akiwasilisha hotuba bungeni jijini Dodoma jana kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Dk. Kalemani alisema lengo la serikali ni nchi kuwa na uwezo wa kuzalisha MW 10,000 ifikapo mwaka 2025.

"Hatua hiyo itafikiwa kwa kutekeleza miradi mikubwa ya uzalishaji umeme kama vile mradi wa uzalishaji nishati hiyo katika maporomoko ya Mto Rufiji wa MW 2,115 na mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi 1- Extension wa MW 185," alisema.

Waziri huyo aliitaja miradi mingine kuwa ni wa Rusumo utakaozalisha MW 80, Ruhudji MW 358, Rumakali MW 222 na kuimarisha mifumo ya uzalishaji umeme nchini.

Alisema mifumo itaboreshwa kupitia mradi wa North-West Grid Extension wa KV 400 yenye umbali wa Km 1,384 iliyojumuisha Iringa, Mbeya, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma hadi Nyakanazi.

"Maeneo mengine ya kisekta yatakayozingatiwa ni kuendeleza utekelezaji wa awamu tatu ya mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati na Umeme Vijijini (REA) katika vijiji 1,990 vilivyobaki kati ya vijiji 12,268.

"Kuendelea na kutekeleza mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, kuimarisha shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia, kuongeza kasi ya usambazaji gesi asilia na kuendeleza miradi ya nishati

INAENDELEA UK 8




# Wafungwa kifungo cha nje kwa kughushi vyeti

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, imewahukumu waliokuwa watumishi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kifungo cha mwaka mmoja kila mmoja baada ya kupatikana na hatia ya makosa tofauti, likiwamo kughushi nyaraka za serikali na vyeti vya shule.

Vyeti hivyo ni vinavyoonyesha viwango vyao vya elimu.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Gabriel Ngaeje, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Washtakiwa hao ni waliokuwa wahudumu wa Idara ya Afya, Hadija Mmanja, Subira Kilete na Ridhiwani Ally walioghushi vyeti la shule pamoja na Ofisa Uvuvi wa wilaya hiyo, Ulimboka Ndile, aliyeghushi nyaraka za serikali zilizotokana na malipo ya ushuru wa mazao ya bahari.

Hata hivyo, inaelezwa watumishi hao kwa sasa wapo nje ya mfumo wa ajira baada ya serikali kutekeleza zoezi la uhakiki wa vyeti vya taaluma kuwabaini watumishi waliokuwa na vyeti halali na waliokuwa na vya kughushi.

Baada ya washtakiwa wote kutiwa hatiani, Hakimu Ngaeje aliwapa nafasi ya kujitetea, kila mmoja aliomba aonewe huruma kwa madai ni wakosaji wa mara ya kwanza.

Pia walijitetea kuwa wana familia zinazowategemea na hawana ajira kama waliyokuwanayo hapo awali, hivyo wakipewa adhabu kubwa, kutazifanya familia zao kuishi mazingira magumu.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Lindi, Peter Camilius, alipoulizwa iwapo anazo kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa washtakiwa, alijibu hana, huku akiiomba mahakama kuwapatia washtakiwa hao adhabu kali ili liwe fundisho kwao na wengine wenye tabia hiyo.

Hakimu Ngaeje akitoa hukumu katika kesi Namba 70/2017 na 42, 43 na 44 mwaka huu, vifungu 333, 335 (a),337 na 342 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, sura ya 16 marejeo ya 2002 na kifungu cha 22 cha Sheria ya Kuzuia Kupambana na Rushwa, Namba 11/2007, aliwahukumu kila mmoja kifungo cha nje cha mwaka mmoja kila mmoja.

Awali ilidaiwa na Mwanasheria wa Takukuru, Peter Camilius, kuwa washtakiwa watatu wa Idara ya Afya walifanya kosa la kughushi vyeti vya elimu ya kidato cha nne, wakati wamehitimu darasa la saba.

Aliendelea kudai kuwa ofisa uvuvi alighushi stakabadhi za makusanyo ya fedha za ushuru na kujipatia malipo yasiyo halali.

# Upinzani wataka ripoti, mikataba mikubwa iwasilishwe bungeni

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imeitaka serikali kuwasilisha bungeni ripoti za utekelezaji wa mapendekezo makubwa na mikataba mikubwa ikiwamo inayohusu gesi asilia ili ijadiliwe na chombo hicho cha kutunga sheria.

Akiwasilisha hotuba yake bungeni jijini Dodoma jana kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha, Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika wizara hiyo, John Mnyika, alisema upinzani unaitaka serikali kuwasilisha bungeni mikataba yote mikubwa inayohusu ujenzi wa mradi wa umeme kwenye Mto Rufiji (Stiegler's Gorge) ili ijadiliwe na Bunge.

Alisema tathmini ya kimazingira na upembuzi yakinifu kuhusu mradi huo ipelekwa bungeni na kujadiliwa na chombo hicho.

Mnyika pia alisema upinzani unaitaka serikali kupeleka bungeni mikataba yote mikubwa kuhusu ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

"Serikali iwasilishe bungeni taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge iliyoundwa na Spika wakati huo, Anne Makinda, kuchunguza kuhusu mgogoro kati ya wananchi wa Mtwara na serikali juu ya ujenzi wa bomba la gesi.

"Serikali iwasilishe bungeni taarifa ya utekelezaji wa maoni ya mapendekezo ya kamati iliyoundwa na Spika Job Ndugai kuchunguza mikataba, utafutaji na uvunaji wa gesi asilia," Mnyika alisema.

BAJETI YA WIZARA MBILI

Mnyika pia aliitaka serikali kuacha utaratibu wa kurundika fedha kwenye miradi michache, akieleza kuwa kutakuwa na athari kubwa katika utekelezaji wa bajeti.

Alibainisha kuwa katika ya mwaka ujao wa fedha, Wizara ya Nishati na Wizara ya Ujenzi zinachukua zaidi ya asilimia 50 ya bajeti yote ya nchi.

"Lazima serikali izingatie mgawanyo wa rasilimali fedha kwa sekta mbalimbali nchini kwa sababu kurundika rasilimali nyingi kwenye miradi michache kunaweza kusababisha kudumaa kwa miradi mingine ya maendeleo," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, kwenye viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Kanyasu awatoa hofu kuhusu kupokwa ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewatoa hofu wananchi kutokana na kazi ya kupanga matumizi bora ya ardhi inayoendelea katika wilaya 10 nchini hasa katika maeneo yanayopakana na hifadhi za taifa.

Kanyasu amesema serikali haina mpango wowote wa kunyang'anya maeneo mapya kutoka kwa wananchi kwa ajili ya kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Alisema hayo juzi kutokana na hofu iliyokuwa imetanda miongoni mwa wananchi wa vijiji vinane vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, wilayani Bunda mkoani Mara waliokuwa wakidai mpango huo unalenga kuchukua maeneo yao ya malisho.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Sarakwa kinachotenganishwa na Mto Rubana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Kanyasu aliwaeleza wakazi hao kuwa kazi ya kupanga matumizi bora ya ardhi katika maeneo hayo ina faida kubwa ikiwamo kuepusha migogoro ya ardhi inayotokea mara kwa mara.

Naibu Waziri alisema mpango wa matumizi bora ya ardhi ni wa kitaifa ambao umelenga kutenga maeneo maalum kwa ajili ya malisho, kilimo na shughuli za maendeleo ili kuepusha migongano inayotokea sehemu mbalimbali nchini na si kunyang'anya ardhi mpya kama inavyodaiwa.

"Nataka niwahakikishie kuwa wizara yangu haina mpango wa kuanzisha msitu wa hifadhi wala jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori katika kijiji chenu. Huu ni uzushi upuuzeni," alisema.

Aidha, Kanyasu aliwaambia wananchi hao kuwa mpango wa matumizi bora ya ardhi utasaidia kuepusha watu wachache kujimilikishia maeneo makubwa na kuwaacha wengi wakiwa hawana ardhi.

"Kinachofanyika kwa sasa ni kuweka rekodi na nyaraka kwa ajili ya vizazi vyenu," alisisitiza.

Alisema katika mchakato wa mpango wa matumizi bora ya ardhi, kunachoweza kufanyika ni kutenga eneo la msitu wa asili wa kijiji kwa ajili ya manufaa yao ikiwamo kuokota kuni na eneo hilo litakuwa chini ya umiliki wa kijiji na si serikali kuu.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliwatoa wasiwasi wananchi hao kuwa licha ya kijiji hicho kuingia katika mpango wa matumizi bora ya ardhi, mifugo yao haitazuiwa kwenda kunyweshwa maji katika Mto Rubana.

"Nimesikia baadhi ya watu wakieneza uzushi kuwa baada ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kukamilika, hakuna mtu yeyote kupeleka mifugo katika Mto Rubana, huu ni uwongo," alisema Kanyasu.

Hata hivyo, aliwaambia kuwa mita 500 kutoka katika mto huo ni eneo la kijiji kwa ajili ya malisho ya mifugo isipokuwa vitu ambavyo havitaruhusiwa kufanywa na mtu yeyote ni kulima pamoja na kujenga nyumba kwa vile eneo hilo ni shirikishi kwa wanyamapori pamoja na mifugo.

HABARI KITAIFA

## EATV yazindua kampeni kuchangisha taulo za kike

Na Elizabeth Zaya

KAMPUNI ya EATV Limited kupitia vyombo vyake vya habari vya radio na televisheni imezindua kampeni ya kuchangisha taulo za kike kwa wanafunzi wenye uhitaji shuleni.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo katika ofisi za kampuni hiyo zilizopo Mikocheni jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Vipindi wa East Afrika Radio, Nasser Kingu, alisema kampeni hiyo itafanyika kwa mwaka mzima.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanawasaidia wanafunzi wa kike zaidi ya 5,000 kwa mwaka huu kwa kuwaondolea vikwazo mbalimbali vinavyokwamisha ndoto zao za kufanya vizuri kielimu ikiwamo kuwapatia taulo za kike za kutumia kwa mwaka mmoja.

"Hii ni mwendelezo wa kampeni ambayo ilianza rasmi mwaka 2017 na kuendelea kwa miaka iliyofuata na ilianzishwa baada ya kubaini ukubwa wa tatizo kupitia takwimu mbalimbali zilizoonyesha wanafunzi wa kike kushindwa kuhudhuria masomo kwa muda wa siku tano hadi saba kila mwezi sawa na siku 60 hadi 70 kwa mwaka wanapokuwa katika siku za hedhi kutokana na kukosa taulo za kike kwa ajili ya kujisitiri," alisema Kingu.

Alisema kampeni ya mwaka huu imelenga kufikia hasa wanafunzi walio katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Pwani, Mara, Kigoma, Manyara, Tabora, Morogoro na Njombe.

Kwa upande wake Mratibu wa Vipindi EATV, Sophia Mng`anya, alisema kampeni hiyo itaenda sambamba na uchangishaji wa pesa taslimu ambazo zitatumika kununua, kupokea taulo hizo kutoka kwa wadau mbalimbali na kuwafikishia wanafunzi husika pamoja na utoaji wa elimu kuhusiana na hedhi salama na mambo yote yanayohusiana na hedhi.

"Kwa mwaka 2017, tulifanikiwa kufikia wanafunzi 550 ndani ya mikoa mitano nchini ikiwa ni robo ya lengo tulilokuwa tumejiwekea la kuwapatia taulo za kutumia kwa mwaka mzima wanafunzi walio shuleni, na kwa mwaka 2018 tulifanikiwa kufikia wanafunzi 2773," alisema Sophia na kuongeza:

"Tunafahamu kwamba ukimuelimisha mtoto wa kike, umeelimisha taifa zima, lakini changamoto ni nyingi katika kufanikisha lengo hilo, na ndiyo maana kampuni ya EATV Limited kupitia vyombo vyake vya habari imekuwa ikiandaa kampeni hii maalum ili kuwasaidia wanafunzi hawa wa kike kufikia ndoto zao kwa kupunguza baadhi ya vikwazo vinavyowakabili ikiwamo kukosa taulo za kujisitiri wakati wa hedhi ili wasiache kuhudhuria masomo ambayo ndiyo msingi wa kufikia malengo yao kimaisha."

Aliwaomba wadau kuunga mkono kwa kuchangia kampeni hiyo kwa kupeleka taulo hizo katika ofisi za EATV Mikocheni au kutuma fedha taslimu katika akaunti ya benki ya CRDB kwa namba 0150431938200 yenye jina Namthamini au kwa kutuma fedha kwa njia ya Airtel Money kupitia namba 0787 633 313 ya East Afrika Televisheni.

# Sababu tatu za upinzani kupinga Stiegler's Gorge

Na Sanula Athanas, DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imeelieleza Bunge sababu tatu za kupinga utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji ya Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge.

Akiwasilisha hotuba yake bungeni kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha, Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika wizara hiyo, John Mnyika, alisema wanakubaliana na dhana ya kuzalisha MW 2,100, lakini hawakubaliani na namna utekelezaji wa mradi huo.

Mnyika ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Tanzania Bara, alisema sababu ya kwanza ya upinzani kutokukubaliana na utekelezaji wa mradi huo ni gharama za kiuchumi za ujenzi wa mradi huo.

Alibainisha kuwa kwa mwaka huu wa bajeti, serikali ilitenga Sh. bilioni 700 kwa ajili ya mradi huo, lakini tayari Wizara ya Fedha na Mipango imeshaeleza kuwa iko katika hatua za mwisho kuidhinisha malipo ya Sh. bilioni 984, hivyo kuwa na ongezeko la Sh. bilioni 284.

"Serikali ya awamu ya tano inaongoza kwa kukiuka taratibu na sheria za nchi. Kwenye mradi huu, serikali imetoa wapi nyongeza ya Sh. bilioni 284 ambazo hazikupitishwa na Bunge?" Mnyika alihoji.

Waziri kivuli huyo alisema sababu ya pili ya upinzani kupinga utekelezaji wa mradi huo ni muda na ongezeko la gharama halisi za ujenzi wa mradi huo.

Alisema Mkakati wa Mwongozo wa Mabadiliko ya Sekta ya Usambazaji wa Umme nchini wa mwaka 2014-2025, unabainisha kuwa uwezo wa kuzalisha umeme unatakiwa kuongezeka kutoka MW 1,583 mwaka 2014 mpaka kufikia MW 10,000 mwaka 2025, ili kuiwezesha nchi kufikia uchumi wa kati sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

"Mradi huu wa umeme wa Mto Rufiji tunaambiwa na serikali kuwa utakamilika ndani ya kipindi cha miezi 36 na utaweza kuzalisha MW 2,100, kiasi ambacho ni asilimia 21 ya lengo kufika kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati.

"Wakati ujenzi unakamilika ndani ya miezi 36 kama tulivyoaminishwa na serikali, itakuwa imesalia miaka miwili tu kufika 2025, hivyo shabaha ya kufikisha MW 10,000 ifikapo mwaka 2025 bado ni ndoto za mchana ambazo serikali yetu imeendelea kuota," Mnyika alisema.

Aliongeza kwa utafiti uliofanywa na Ode-

INAENDELEA UK 8



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio ya Mkutano Mkuu wa 109 wa Nchi za Afrika, Kariabian na Pasifiki (ACP), uliofanyika hivi karibuni Ubelgiji. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## CWT yaja juu walimu kujeruhiwa, kuporwa

Na Gurian Adolf, KATAVI

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) mkoani Katavi, kimelaani kitendo cha watu wasiojulikana kuwavamia walimu kwenye nyumba za shule za kata ya Magamba Manispaa ya Mpanda na kuwapora fedha sambamba na kujeruhi kwa kuwakata mapanga.

Tukio hili lilitokea hivi karibuni ambapo kikundi cha watu wasiojulikana wanaojiita "tukale wapi" wamekuwa wakiwavamia watumishi wa umma hususan walimu na kuwajeruhi kwa mapanga kisha kuwapora fedha. Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Katavi, John Mshyota, alisema kikundi hicho cha uhalifu kimekuwa kikifanya uhalifu takribani miezi kadhaa tofauti katika maeneo tofauti mkoani humo kikitumia kaulimbiu hiyo.

Mshyota alisema vitendo vya kuwavamia na kuwapora walimu ni vita inayodidimiza elimu mkoani humo, hivyo kuziomba mamlaka husika kuchukua hatua na kukomesha vitendo hivyo kwa kuwa vinahatarisha maisha ya walimu.

Alisema kumekuwapo na mfululizo wa matukio yaliyowahi kutokea mkoani Katavi kuanzia Desemba 2018.

Miongoni mwa matukio hayo ni la mwalimu mmoja wa shule ya msingi kuvamiwa vyumbani kwake usiku na kupigwa rungu huku akitishiwa kuchomwa kisu na kubakwa. Alisema Januari 12, 2018 mwalimu mwingine alivamiwa majira ya usiku hivyo hivyo akiamrishwa kutoa fedha zote za mshahara wake sambamba na kuporwa simu yake ya kiganjani.

Mshyota aliongeza katika Shule ya Sekondari ya Magamba Januari 31, 2019 saa 3:30 usiku, walimu wawili walivamiwa na kukatwa mapanga sehemu za mikono na usiku wa siku hiyo hiyo mwalimu mwingine alivamiwa na kuporwa shilingi 250,000.

## Mirungi yanaswa

Na Cynthia Mwilolezi ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha limebaini mbinu mpya inayotumika kusafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi kupitia mpaka wa Namanga na kuwatia mbaroni watuhumiwa wawili wakiwa na madumu nane yaliyokuwa yamehifadhi dawa hizo za kulevya zenye uzito wa kilo 140.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Jonathan Shana, aliwataja watuhumiwa ni Philipo Mungasi Lairumbe na Ngaruma Nairishoo, wote wakazi wa Kijiji cha lengijave, wilayani Arumeru. Alisema walikamatwa jana asubuhi katika eneo la Sakina jijini Arusha wakiwa na madumu manane waliyokuwa wameyapakia kwenye pikipiki zao aina ya King Lion zenye namba MC 772 BVT na MC 404:CEE yakiwa yamesheheni dawa hizo za kulevya.

Alisema polisi waliokuwa doria waliyatilia shaka madumu hayo na kuwasimamisha watuhumiwa hao na walipoyafanyia upekuzi walibaini ni dawa za kulevya aina ya mirungi zikiwa zimehifadhiwa kwenye madumu hayo yakiwamo manne ya lita 40 na manne ya Lita 20.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Mahakama inastahili pongezi kwa hukumu hii*

**MAMLAKA** zote husika zina jukumu la kuhakikisha vitendo vya ukatili hasa ubakaji kwa watoto vinakomeshwa, ili kuwafanya waishi maisha ya furaha na amani.

Miongoni mwa mamlaka hizo ni pamoja na wizara mbalimbali, Jeshi la Polisi, Ustawi wa Jamii, Mahakama na taasisi nyinginezo zinazohusika katika kusimamia masuala ya haki na malezi ya watoto.

Tunatambua kuwa vitendo vya ukatili kwa watoto vinaathiri kwa namna nyingi ikiwamo kiakili, kimwili na kisaikolojia hali ambayo ni wazi isipodhibitiwa inaweza kuathiri ustawi wa jamii kwa ujumla.

Hivi karibuni Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto 2017 -2022, ulizinduliwa na Waziri wa Afya, Maendeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Alikaririwa na vyombo vya habari akibainisha kuwa ukatili dhidi ya watoto unafanywa katika nyumba wanazoishi na shuleni, hivyo kila shule ya msingi na sekondari kutaundwa timu za ulinzi pamoja na kila kata kuwa na timu ya ulinzi.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Jeshi la Polisi, vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto vilivyoripotiwa 2015 vilifikia 22,876 kati ya hivyo vitendo vya ubakaji vilikuwa 3,444, shambulio, kujeruhi na matusi vilikuwa 14,561.

Jambo linalotia moyo ni kwamba baadhi ya mamlaka zimejitokeza kuonyesha umakini wa hali ya juu katika kuhakikisha zinakomesha vitendo hivyo viovu.

Tumepata taarifa kuwa Mahakama ya Wilaya Mkoa wa Kigoma imemhukumu mkazi wa Burega, Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Sadock Amani (21), kifungo cha maisha jela kwa kosa la kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka mitano.

Hukumu hiyo ilitolewa Mei 27, mwaka huu na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kenneth Mutembei, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo bila kuacha shaka.

Tunampongeza Hakimu Mutembei kwa kuwa amekaririwa na vyombo vya habari akieleza kuwa mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili liwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia ya kikatili kama yake.

Pia tunapongeza upande wa mashtaka kwa kuwa umefanikisha kutolewa kwa hukumu hiyo kali, kwa sababu uliwezesha ushahidi usio na shaka kutolewa na mashahidi watano pamoja na kielelezo kimoja cha PF3 ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimbaka mtoto huyo.

Makahama hiyo ilielezwa kuwa mshtakiwa huyo na mama wa mtoto wamepanga nyumba moja maeneo ya Burega, Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Mahakama haikuwa na wasiwasi na ushahidi uliotolewa na daktari pamoja na mtoto huyo, ambapo alimbaini mshtakiwa kuwa ni jirani yake, ndiye aliyembaka kwa sababu walikuwa na mazoea ya kuitana anko.

Pia mtoto huyo aliyefanyiwa ukatili imeelezwa kuwa alikuwa na uelewa mkubwa wa kueleza, hivyo kufanya Mahakama hiyo kuamini kuwa mshtakiwa huyo alimbaka mtoto huyo.

Upande wa mashtaka umethibitisha kosa bila kuacha shaka yoyote, hivyo Mahakama inamtia mshtakiwa hatiani kwa kosa alilοshtakiwa.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Benedict Kivuma, alidai kuwa Januari 5, 2018 majira ya mchana eneo la Burega, mkoani Kigoma, mshtakiwa alimbaka mtoto huyo na kumsababishia maumivu makali.

Tunasisitiza kuwa hatua kali za kisheria zinaweza kusaidia kukomesha vitendo hivi vya kikatili, lakini pia wanajamii hasa wazazi wanapaswa kuongeza umakini katika kufuatilia nyendo za watoto pamoja na kuzungumza nao ili kuwaelimisha wasiogope kujieleza wanapotendewa ukatili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Salome Kitomari

# Elimu bado muhimu kuelekea marufuku mifuko ya plastiki

**JULAI** Mosi imekaribia ambayo ni tarehe rasmi ya mwisho iliyowekwa na serikali ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini.

Wazalishaji na wauzaji wa mifuko hiyo walipewa mwezi mmoja kusambaza mzigo walio nao, kama ilivyo kwa watumiaji wengine kwa maana ya wenye maduka.

Nao wanatakiwa kuhakikisha hawaendelei kutumia wala kusambaza mifuko hiyo baada ya muda wa huruma wa mwezi mmoja uliotolewa kumalizika.

Hatua hii ya serikali ni nzuri kwani inakwenda kuyaokoa mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Hiyo ni kwa sababu kiasi cha mifuko ama plastiki inayokwenda ardhini karibu kila siku itapungua au kwisha kabisa.

Hata hivyo, changamoto anayoiona Muungwana kuelekea siku hiyo ni ile ya kutokuwapo kwa mifuko mbadala ya kutosha kwa ajili ya mahitaji ya wateja wanapokwenda dukani ama sokoni kununua mahitaji mbalimbali.

Hii ni kwa sababu wauzaji wa maduka ya kawaida wanatumia mifuko hii ya plastiki inayopigwa marufuku kwa ajili ya kuwekea wateja wao bidhaa wanazonunua, iwe ni unga, sukari au chochote.

Pamoja na hatua njema zinazoendelea kuchukuliwa, wasiwasi wa Muungwana ni ukweli kwamba bado mifuko mbadala haijasambazwa kwenye maduka ya jumla ili wauzaji wa kawaida waipate.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, aliwatahadharisha viongozi wa serikali za mitaa dhidi ya matumizi ya nguvu kwa wananchi watakaokutwa wanatumia mifuko ya plastiki.

Ni tahadhari nzuri kwa kuwa ipo mifano ya viongozi wa ngazi hiyo wakiwatumia mgambo wa halmashauri, manispaa na majiji kutumia nguvu dhidi ya wananchi.

Mathalani, ni katika zoezi la kukabili wanaotupa takataka ovyo ambapo zilitumika nguvu kupita kiasi, hali iliyosababisha baadhi ya wananchi kujeruhiwa kutokana na vipigo.

Si mgambo tu kwani hata vijana waliopelekwa kwenye mitaa mbalimbali nao wanadaiwa kujichukulia sheria mkononi pamoja na kuwapo sheria za kushughulikia jambo hilo.

Tahadhari iliyotolewa na waziri ni muhimu kuzingatiwa tukichukulia uzoefu wa matukio ya nyuma.

Kwamba wapo watakaogeuza operesheni hiyo mtaji wa kujipatia kipato.

Sheria imetaja kiwango cha faini atachachotozwa mhusika, lakini upo utaratibu wa kutoza na si kila anayekamata anastahili kutoza faini mfano mgambo.

Muungwana ana rai kwamba wakati jitihada za kutoa elimu na tahadhari kuhusiana na marufuku hii zikiendelea kwa kasi inayotakiwa, ni vyema kwa upande mwingine kasi ya kutengeneza mifuko mbadala nayo ikaendelea.

Lakini pia kuisambaza kwa watumiaji wa jumla na rejareja ili kuondoa mkanganyiko.

Kwa kufuata mfano wa Zanzibar na Kenya, kuwe na utaratibu wa kuwaelimisha wananchi kupitia vikao vya serikali za mitaa na vijiji, au kwenye maeneo yote ya huduma za kijamii kama hospitali na shuleni.

Muungwana anatarajia kuona picha, video fupifupi zikielimisha wananchi juu ya mifuko inayotakiwa ili kunapotokea mwananchi amekamatwa aweze kujitetea.

Vilevile uonevu unaweza kujitokeza kwa wafanyabiashara wenye maduka kwa sababu ya kukutwa tu na bidhaa zilizotoka viwandani ambazo hufungwa nailoni badala ya maboksi.

Katika hali kama hii ni wazi kwamba mtumiaji wa mwisho ambaye ndiye muuzaji anaweza akakutwa na mfuko wa plastiki ambao umeshapigwa marufuku na kukamatwa.

Ndipo panapojitokeza umuhimu wa kukagua viwanda vya kuzalisha plastiki na viwanda vinavyofunga bidhaa kwa plastiki.

Eneo lingine ni kwenye viwanja vya ndege ambapo baadhi ya wasafiri hufunga mizigo yao kwa kutumia nailoni maalum.

Hivyo basi kuna umuhimu wa kuwaelimisha wananchi kupitia mitandao ya kijamii, kama vile Instagram, Facebook, WhatsApp, Twitter unapojitokeza ili ujumbe usambae kwa haraka.

**Hii ni kwa sababu wauzaji wa maduka ya kawaida wanatumia mifuko hii ya plastiki inayopigwa marufuku kwa ajili ya kuwekea wateja wao bidhaa wanazonunua, iwe ni unga, sukari au chochote.**

BARUA/MJADALA

# Mwenendo huu si wa kiungwana kabisa

***Mhariri***

*Habari za majukumu!*

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaotupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani.*

*Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili.*

*Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimueleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake.*

*Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*

*Ni muhimu watu hao wakaelewa kwamba ndani ya usafiri wa umma, kila mtu anakuwa ni mipango yake kichwani kama anaenda kazini, na anahitaji utulivu kama anarudi kutoka kazini kwa sababu ya uchovu wa siku nzima na changamoto nyingine alizokutana nazo katika mizunguko yake.*

*Hahitaji kusikia kelele za namna mnavyotongozana au jinsi ulivyomchongea jirani yako kwa mumewe au jinsi ulivyomshushua shoga yako mbele ya watu.*

***Jackton Mwamba- Mbagala***



# Kasi iongezwe kusambaza mawasiliano kwa ustawi wa Tanzania ya viwanda

**Na Mashaka Mgeta**

SERIKALI ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, imeazimia na kuwekeza katika utekelezaji wa sera itakayoifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati unaotokana na sekta ya viwanda ifikapo 2025.

Hatua kadhaa zilizofikiwa zinadhihirisha utashi wa kisiasa na uwajibikaji katika kufanikisha matakwa ya sera hiyo, ingawa si jambo la ajabu kukubali kwamba zipo changamoto zinazopaswa kufanyiwa kazi ili kupata ufanisi zaidi wenye kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Pengine hali hiyo imechochewa pia na namna Rais Magufuli anavyosisitiza umuhimu wa utekelezaji wa sera hiyo, sanjali na kuwawajibisha viongozi wa serikali katika ngazi tofauti, wasiokidhi matakwa ya kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati unaotokana na viwanda.

Karibu mara zote ambapo Rais Magufuli anazungumza na wananchi ama taasisi nyinginezo, suala la Tanzania ya viwanda limekuwa moja ya ajenda anazozisisitiza na kuzidi kuzitolea maelekezo.

Na kwa hali hiyo, wasaidizi wake hasa mawaziri na wengine waliopo katika nafasi za uteuzi kama mawaziri, wamekuwa 'wakiibeba' ajenda hiyo kila wanapotekeleza majukumu yao.

Ukweli kwamba ajenda hiyo iliyopewa kipaumbele (pengine) kuliko nyinginezo, inaibua umuhimu kwa jamii kuijadili ili, si tu kubaini wenye fursa za kuifanya ifanikiwe, lakini pia kutambua nafasi ya ushiriki wa kila raia na taasisi za kijamii ikiwamo sekta binafsi.

Ufanisi katika huduma ya mawasiliano ni mojawapo ya nyanja za sekta binafsi zinazochangia katika kutimiza azma hii ya Tanzania ya viwanda hasa kupitia huduma bora ya simu za mkononi ama njia nyingine za mawasiliano ya kisasa.

Kwa mfano, katika miaka michache tangu simu za mkononi zihusishe teknolojia za kisasa zinazorahisisha mawasiliano, jamii imeshuhudia mageuzi 'yanayopenya' hadi kwenye sekta nyingine kama fedha, elimu na ujasiriamali, japo kuzitaja kwa ufupi.

Huduma hizo za muhimu zimeweza; katika kipindi kifupi, kuokoa na `kuzimua' maisha ya Watanzania katika kada mbalimbali, kiasi kwamba sasa imekuwa vigumu kufikiri kuhusu maisha ya watu pasipo matumizi ya teknolojia zilizoko katika sekta hiyo ya mawasiliano.

Kwa babati mbaya, kumekuwa na tofauti kubwa ya upatikanaji wa huduma hizo baina ya wananchi waishio mijini na wale wa vijijini kwa maana maeneo mengi ya vijijini hayajafikiwa ama kunufaika ipasavyo na huduma hizo ikilinganishwa na mijini.

Hii si kusema kwamba hakuna kilichofanyika kwa maeneo ya vijijini, la hasha. Zipo hatua zenye kuashiria matokeo chanya zilizopigwa hadi sasa.

Pamoja na serikali kutimiza wajibu wake, kwa sehemu kubwa baadhi ya wadau wa sekta ya mawasiliano ya simu za mkononi zinazotegemewa zaidi katika mageuzi hayo wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba tofauti hizo za mijini na vijijini zinapatiwa ufumbuzi.

Ipo mifano mingi katika suala hilo, lakini kwa mfano mdogo ni hatua ya hivi karibuni ya kampuni ya tigo ilikaririwa kuingiza huduma zake katika Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa.

Sehemu ya kijiografia ya wilaya hiyo `inakaliwa' na vijiji na hivyo kuwa miongoni mwa maeneo yasiyolingana na yale ya mijini katika upatikanaji wa huduma za mawasiliano.

Ni dhahiri kwamba wananchi wa maeneo ya wilaya hiyo na kwingineko watakuwa miongoni mwa kada zenye uhakika wa kupata mawasiliano bora yanayochochea maendeleo ya jamii hasa katika kipindi hiki cha kuelekea katika Tanzania ya viwanda.

Ni jambo la kuaminika kwamba watu wanapopata mawasiliano yaliyoboreka kwenye maeneo yao kunachangia kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa huduma nyingine ikiwamo miamala ya fedha.

Nimegusia eneo moja linalohusu nyanja ya mawasiliano, lakini yapo maeneo mengi zaidi kama kilimo, mazingira, pembejeo, malighafi na nyinginezo zenye nafasi ya pekee katika kuchagiza mipango na mikakati ya kuifanya Tanzania kuwa yenye uchumi unaotegemea viwanda.

Lakini yapo maeneo mengine kama elimu, afya na maarifa na stadi zinazokidhi mabadiliko yaliyofikia, yote hayo yakichagiza kuifikia nia hiyo inayosimamiwa kwa weledi na serikali ya Rais Magufuli.

Pasipo shaka, ushirikiano huu wa serikali na sekta binafsi zikiwamo kampuni za mawasiliano unaweza kuwa kichocheo kizuri cha ndoto za Tanzania ya Viwanda kutimia kwa wakati uliopangwa na kwa mafanikio makubwa.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Sababu tatu za upinzani kupinga Stiegler's Gorge

INATOKA UK 5

bretcht (2012) na iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini (2016), gharama za mradi huo zinatarajiwa kupanda hadi kufikia Sh. trilioni 22.95.

"Kupanga ni kuchagua, Sh. trilioni 22.95 ni sawa na asilimia 69.3 ya bajeti nzima ya mwaka 2019/20 inayopendekezwa na serikali ya CCM. Mradi huu wa umeme wa Mto Rufiji utakuwa aina nyingine za uamuzi unaoenda kuiweka nchi katika hali mbaya ya kifedha," alisema.

Mnyika alisema sababu ya tatu ya upinzani kupinga utekelezaji wa mradi huo ni athari za kimazingira. Alisema imesemwa mara nyingi na watalaamu mbalimbali kwamba mradi huo utaathiri Hifadhi ya Selous kwa kuharibu mazingira na hatimaye uchumi na maisha ya watu.

"Mradi huo utazuia tani milioni 16.6 za virutubisho vya ardhi kwa mwaka, hivyo kusababisha mmomonyoko wa ardhi kwenye delta ya Rufiji.

"Ipo pia hoja ya eneo ambalo mradi husika utatekelezwa ambalo ni kilomita za mraba 1,200. Eneo hili ni kubwa na litaufanya mradi kuwa ni bwawa kubwa kuliko Afrika Mashariki na kuzua hofu ya kukausha maziwa madogo madogo yote ya eneo la jirani, litaathiri utalii, kukomba rutuba yote ya ardhi ya eneo hilo hadi Delta ya Rufiji na hivyo kuua samaki na kuathiri uvuvi wa samaki kamba na kamba koche wanaotegemewa na watu zaidi ya 200,000 wa eneo hilo.

"Mradi huo unatekelezwa kinyume cha mikataba ya kulinda urithi wa asili ambayo Tanzania imetia saini. Mradi wa Stiegler's Gorge uliasisiwa tangu enzi za Nyerere na haukutekelezwa kutokana na sababu za kimazingira," Mnyika alisema.

HASARA TANESCO

Waziri kivuli huyo pia alisema Shirika la Umeme (Tanesco) limekuwa na mwenendo usioridhisha kutokana na kupata hasara mfululizo.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2015/16, hasara iliyopatikana ilikuwa Sh. bilioni 346.4 na hesabu za miezi 18 hadi mwaka ulioshia Juni 2015, hasara ilikuwa Sh. bilioni 124.46 na hadi kufikia mwaka 2018, hasara ilikuwa imefikia Sh. bilioni 346.

"Mwenendo wa hasara umekuwa ukichangiwa na hali isiyoridhisha ya maji ya kuzalisha nguvu ya umeme pamoja na ongezeko la gharama za uzalishaji.

"Mfululizo wa hasara hizo una athari kubwa kwenye mtaji wa shirika, hivyo kulifanya kutokopesheka ili kukidhi mahitaji yake ya kifedha," alisema.

Mnyika alisema kambi yao inaitaka serikali kuanzisha operesheni maalum kuhakikisha mikoa ambayo haijafanya vizuri katika kuunganisha umeme kaya za maeneo hayo.

Alisema utafiti wa hali ya umeme (2016), ulibaini Mkoa wa Rukwa ndiyo ulishika mkia katika kaya zilizounganishwa na huduma ya umeme (asilimia 8.7) ulifuatwa na mikoa ya Simiyu asilimia 11.5, Shinyanga asilimia 12.8, Geita asilimia 14, Songwe asilimia 15.9 na Kigoma asilimia 16.2.

Alibainisha kuwa mikoa iliyoongoza kwa kaya zake nyingi kuunganishwa na huduma ya umeme ni pamoja na Dar es Salaam asilimia 75.2, Njombe asilimia 50.5 na Kilimanjaro asilimia 42.6.

Alisema kambi yao pia inaitaka serikali kutoa ufafanuzi kuhusu jitihada inazofanya kuhakikisha wateja zaidi wa gesi asilia wanapatikana mkopo wa mradi wa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam wa Dola za Marekani bilioni 1.225 ulipwe.

Mnyika alisema kwa sasa Tanesco ndiyo mteja mkuu wa gesi asilia akitumia wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku, sawa na asilimia sita tu ya ujazo wa bomba hilo, hivyo kuwa na upungufu wa futi za ujazo 737.39 kujaza bomba.

Kuhusu mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania, Mnyika alisema upinzani unaitaka serikali kulieleza Bunge idadi ya ajira zilizoanza kutolewa kwa raia wa Tanzania na endapo serikali imepata mapato yoyote kutoka kwa kampuni zilizokuwa zinatekeleza hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo.



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kelvin Boya, John Alfred na Essa Mohamedali ambao ni washindi wa shindano la ubunifu wa suluhisho la Teknohama ya kufikisha elimu vijijini (Hackathon), lililodhaminiwa na Vodacom Tanzania Foundation kupitia mradi wa "Instant Schools" lililofanyika wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu ( Innovation week ) jijini Dar es Salaam, wakifurahia kompyuta zao baada ya kukabidhiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Vodacom Tanzania PLC, Jacquiline Materu (kushoto) wakati wa hafla iliyofanyika katika makao makuu ya kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Watano zaidi watumbuliwa umwagiliaji

INATOKA UK 3

dhisha kwenye miradi mbalimbali.

Alisema serikali imechukua hatua hiyo kutokana na udhaifu wa kiutendaji ndani ya tume hiyo ikiwamo matumizi mabaya ya fedha za miradi, rushwa, matumizi mabaya ya madaraka, upendeleo na kukosa umakini.

Waziri Mkuu pia alisema tume hiyo imeshindwa kusimamia miradi takribani 10 katika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha sekta ya umwagiliaji kushindwa kupata mafanikio yaliyotarajiwa kutokana na ubadhirifu.

Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na mradi wa umwagiliaji wa Luiche unaokadiriwa kumwagilia hekta 3,000 ambao upo katika hatua za awali za utekelezaji, lakini tayari pamekuwapo na matumizi mabaya ya fedha za mradi.

Pia katika tuhuma hizo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu alitoa kibali na kulipa fedha taslimu masurufu ya jumla ya Sh. milioni 100.7 kwa wahandisi wa makao makuu, maofisa mipango, tathmini na ufuatiliaji kwenda kufanya ukaguzi badala ya kujenga hatua iliyosababisha mkaguzi wa nje kuhoji uhalali wa malipo hayo bila majibu.

# Waziri ajivunia kutokuwa na mgawo umeme mwaka huu

INATOKA UK 3

jadidifu," alisema.

Dk. Kalemani alibainisha kuwa hali ya upatikanaji umeme imeendelea kuimarika katika kipindi chote cha bajeti ya mwaka huu wa fedha.

Alisema mahitaji ya umeme yameongezeka kutokana na kuongezeka shughuli za kiuchumi zenye kuhitaji nishati ya umeme wa kutosha.

Kwa sababu hiyo, alisema uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme imeongezeka hadi kufikia MW 1,601.90 kutoka MW 1,517.47 zilizofikiwa katika mwaka wa fedha uliopita.

"Kati ya jumla ya MW 1,601.90 zilizopo nchini, MW 1,565.72 zimeunganishwa katika mfumo wa gridi ya taifa na MW 36.18 zipo nje ya mfumo wa gridi ya taifa," alibainisha.

Dk. Kalemani alisema matumizi ya juu ya umeme yamefikia MW 1,116.58 kulinganishwa na MW 1,051.27 zilizofikiwa mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 6.2.

Alibainisha kuwa umeme uliozalishwa nchini uliongezeka kutoka MW 7,114 mwaka 2017 na kufikia MW 7,374 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 3.7.

"Hadi kufikia mwaka 2015, nchi yetu ilikuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 1,204 ikilinganishwa na uwezo wa sasa wa MW 1,601.9, sawa na ongezeko la asilimia 33," alisema.

Akizungumzia kuhusu nishati ya gesi asilia na mafuta, Waziri Kalemani alisema hadi kufikia Mei mwaka huu, futi za ujazo trilioni 57.54 za gesi asilia zimegunduliwa nchini.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2018/19, shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia zimeendelea kutekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na Kampuni za Kimataifa za Mafuta (IOCs).

"Uchukuaji wa data za mitetemo za 2D zenye kilometa 442 za mstari katika kitalu cha Ruvu umekamilika," Dk. Kalemani alisema.

Aliongeza kuwa uchakataji na utafsiri wa data hizo unafanyika kubaini ukubwa wa mashapo na eneo zuri la kuchoronga visima vya utafutaji na uendelezaji bado unaendelea.

Alisema uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo umeongezeka kufikia futi za ujazo milioni 190 kwa siku kwa mwaka 2018/19, ikilinganishwa na wastani wa futi za ujazo milioni 175 kwa siku, sawa na ongezeko la asilimia 8.6.

Ili kutekeleza majukumu yake, Waziri Kalemani aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 2.1 kwa ajili ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dustan Kitandula, aliitaka serikali kutoa kibali cha ajira ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa watumishi katika taasisi zilizo chini ya wizara hiyo.

**HABARI KITAIFA**

# RC aunda timu kuchunguza malalamiko malipo korosho

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa NACHINGWEA**

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, ameunda timu ya watu saba kwa ajili ya kuchunguza malalamiko ya wakulima wa korosho wanaodai hawajalipwa fedha zao, ili kama yana ukweli yafanyiwe kazi haraka.

Zambi alisema hayo juzi kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Runali uliofanyika mjini na Nachingwea na kufafanua kuwa amepata malalamiko mengi kutoka kwa wakulima.

Alisema timu hiyo inaendelea kufuatilia malalamiko hayo na kwamba itawasilisha taarifa kwake mwishoni mwa mwezi huu.

"Zaidi ya Sh. bilioni 190 zimelipwa, lakini malalamiko yamekuwa ni mengi wakulima wanadai hawajalipwa, mara wamelipwa pungufu, hivyo nimeamua kuunda timu ya watu saba kufuatilia malalamiko hayo," alisema Zambi.

Alisema timu hiyo itachunguza ili kujua ni wangapi hawajalipwa na pia kubaini sehemu ya tatizo, kwa vile serikali inataka kila mkulima apate malipo yake.

"Timu yangu ilianzia kwenye vyama vya wakulima na maeneo mengine kikiwamo kituo cha kuhakiki malipo ya korosho kilichopo Mtwara ili kubaini wapo penye tatizo, nani amelipwa na nani bado," alisema.

Aidha, alisema kwenye vyama vya ushirika kumekuwapo na changamoto nyingi zinazosababisha na viongozi wasio waaminifu wanaosababisha serikali ilaumiwe na kumbe wao ndio wenye makosa.

Alitolea mfano msimu wa korosho uliopita kwamba wapo baadhi ya viongozi wa vyama hivyo waliokuwa wakisafirisha korosho kwenda katika ghala kuu, huku wakizipunguza njiani. "Mwisho wa siku wanasingizia kwamba korosho zimeibiwa katika ghala kuu na kumbe wao ndio wamepunguzia njiani...hivyo ninyi viongozi msipokuwa waaminifu mtaua ushirika," alisema.

Zambi alisema ushirika huwa unajengwa uaminifu na kuwataka wajumbe wa vyama vya ushirika wawe na utaratibu wa kuchagua viongozi wanaotanguliza maslahi ya vyama na siyo yao binafsi.

"Vilevile, ni lazima chama cha ushirika kujua idadi ya wanachama wake, majina yao na ukubwa wa mashamba yao ili iwe rahisi kufanya uhakiki, kwani kuna chama kimoja tulikwenda kukitembelea tukakuta viongozi hawajui idadi ya wanachama, majina wala ukubwa wa mashamba yao, hili ni tatizo," alisema.

Mwenyekiti wa Runali, Hassan Mpako, aliahidi kusimamia kikamilifu maagizo hayo ili kuhakikisha wanachama wa chama hicho ambao ni vyama vya ushirika vya msingi vinakuwa na viongozi bora.

"Runali inaundwa na wilaya tatu za Ruangwa, Nachingwea na Liwale, ilianzishwa mwaka 2013 ikiwa na wanachama 52, wameongezeka kufika na kufikia 104, wengine wanazidi kutuma maombi ya kujiunga," alisema Mpako.



Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Lilian Matinga, akikata utepe kuzindua mnara wa mawasiliano wa Tigo, uliopandishwa hadhi kutoka 3G kwenda 4G, wilayani humo mkoa wa Katavi jana. Kulia ni Meneja Mauzo wa kampuni hiyo, Kanda ya Kusini, Francis Ndada. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mikakati ya Chadema ya usalama wa Lissu

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimebainisha kuwa kina mikakati maalum ya kuhakikisha Mbunge wa Singida Mashariki na Mwanasheria Mkuu wa chama hicho, Tundu Lissu, anakuwa salama atakaporejea nchini.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, licha ya kutoweka wazi mikakati hiyo, lakini alikiri kuwapo kwake, na kuwa itatekelezwa kadiri ya muda husika.

"Mikakati ya kiusalama huwa haiwekwi hadharani, lakini jua kwamba ipo na itaendelea kutekelezwa kadiri ya muda na wakati husika," Mrema alisema.

Mbunge huyo ameshaweka wazi kuwa atarejea nchini Septemba 7, mwaka huu, akitokea Ubelgiji alipokwenda kwa matibabu baada ya shambulio la risasi linalodaiwa kutekelezwa na watu wasiojulikana Septemba 7, mwaka juzi.

Akizungumza na Nipashe Ijumaa, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, alimhakikishia Lissu usalama wa kutosha atakaporejea nchini.

Kamanda Sirro alisema kurejea kwa Lissu kutasaidia kukamilisha uchunguzi na kufahamu waliohusika na shambulio dhidi yake, na kwamba kama raia wengine wa Tanzania anahakikishiwa usalama wake kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

"Kwanza tunashukuru kuwa amepona na sasa anarejea... tutaweza kufahamu zaidi waliohusika na shambulio lake, lakini pili usalama wake ni jambo la muhimu kama raia mwingine yeyote wa nchi ndio maana hata wewe upo salama, kwa hiyo tutahakikisha anakuwa salama," Sirro alisema.

Septemba 7, mwaka juzi, Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 akiwa ndani ya gari nyumbani kwake Area D jijini Dodoma na watu hao wakati akitoka bungeni.

Baada ya shambulio hilo la risasi, Lissu ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Upinzani Tanzania alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Dodoma kwa matibabu ya awali na siku hiyo hiyo usiku alihamishiwa katika hospitali moja mjini Nairobi, Kenya.

Lissu alikaa siku 121 hospitali ya Kenya hadi Januari 6, mwaka jana, alipohamishiwa hospitali nyingine Ubelgiji ambako Desemba 31, alimaliza matibabu yake ya awali na kuanza ziara nchi mbalimbali.

Januari 19, mwaka huu, Lissu alihojiwa katika kipindi cha Dira ya Dunia cha Idhaa ya Kiswahili ya BBC na kuonyesha nia ya kugombea urais mwaka 2020 kama wanachama na viongozi wenzake wa Chadema watampa ridhaa hiyo.

# Wakerwa uchakavu majengo ushirika

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

MAJENGO ya iliyokuwa hoteli ya Angoni Arms, mali ya Chama Kikuu cha Ushirika Songea na Namtumbo (SONNAMCU) mkoani Ruvuma, yapo hatarini kubomoka kutokana na kutelekezwa na mmiliki kwa zaidi ya miaka mitatu bila kukarabatiwa.

Wapangaji walizungumza kwa nyakati tofauti mjini Songea, kwa masharti ya kutotajwa majina, walisema kuwa hali ya majengo ya hoteli hiyo yapo katika hali mbaya kutokana na kuwa na nyufa pamoja na kuvuja nyakati za masika au mvua inaponyesha.

Walisema majengo hayo ambayo kwa sasa baadhi ni makazi ya popo, yapo katika eneo zuri, lakini wanashindwa kuelewa ni sababu zipi zinazoifanya uongozi wa SONNAMCU kushindwa kuyafanyia matengenezo wakati hoteli hiyo ilikuwa ni kitega uchumi kikubwa kwa chama hicho.

Walifafanua zaidi kuwa kwa muda mrefu baadhi ya majengo ambayo yapo katika hali nzuri kidogo, wajanja waliamua kuwapangisha watu kwa kupewa masharti tofauti. Baadhi waliambiwa walipe miezi mitatu na wengine miezi sita na kila mwezi walilipa Sh. 15,000 kila chumba, hoteli hiyo ina vyumba 17 ambavyo vimepangishwa.

Wapangaji hao wanalipa kila mwezi, lakini wanashangaa kwa nini fedha hizo hazifiki SONNAMCU, na wapangaji wanapokwenda kuuliza kwa wamiliki hao wanajibiwa kuwa hawawatambui wakidai wanachokijua majengo hayo kwa sasa hayana mpangaji.

Wameiomba serikali ifanye jitihada ya kuyanusuru majengo hayo ambayo ni mali ya wakulima wa tumbaku Songea na Namtumbo ili yaweze kurudi katika hali yake ya kawaida na yaendeshwe kwa tija na wakulima wenye mali hiyo kupitia chama chao kiukuu.

Meneja Mkuu wa SONNAMCU, Juma Mwanga, alikiri kuchakaa kwa majengo hayo, na kusema wapo katika harakati za kumtafuta mwekezaji atakayewekeza kibiashara katika majengo hayo, hivyo kuwaomba wadau wajitokeze kuchangamkia fursa hiyo.

Mwanga alisema kuhusu waliopangishwa na mtu asiyejulikana tayari wamepewa barua ya kuwataka waondoka haraka katika majengo hayo na kama wana tatizo wamtafute aliyewapangisha.

HABARI BUNGENI

## Mbunge ataka ufaulu masomo Sayansi na Hisabati

MBUNGE wa Tarime Mjini (Chadema), Esther Matiko, amehoji serikali ina mpango gani wa kunusuru ufaulu wa wanafunzi katika masomo ya Sayansi na Hisabati ambayo yanaonekana kushuka kila mwaka.

Akiuliza swali bungeni jana, alisema kwa mwaka 2015 asilimia 85 ya wanafunzi walifeli somo la Hisabati katika matokeo ya kidato cha nne.

"Aidha, katika masomo mengine ya Kemia, Fizikia na Biolojia, ufaulu bado ni duni sana," alisema.

Alihoji serikali ina mpango gani wa haraka wa kuinusuru Halmashauri ya Mji wa Tarime na janga hilo la ufaulu duni katika masomo hayo.

"Je, nini mkakati wa serikali katika kuziwezesha maabara za shule za sekondari zilizojengwa kwa nguvu kubwa ya wananchi ndani ya Jimbo la Tarime Mjini kuweza kupata wataalamu na vifaa vya maabara ili kuinua ufaulu kwenye masomo ya Sayansi?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema serikali inatekeleza mipango mbalimbali ya uboreshaji wa elimu ya sekondari nchini, ili kuinua kiwango cha ufaulu na ubora wa elimu kwa ujumla.

Alieleza kuwa serikali imeipatia Halmashauri ya Mji wa Tarime walimu 59 wa masomo ya Sayansi ili kuboresha ufundishaji na kujifunza.

Aidha, alisema serikali katika mwaka wa fedha 2019/20, imepanga kutumia Sh. bilioni 58.2 kupitia EP4R kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu ya sekondari 70 nchini ikiwamo Halmashauri ya Mji wa Tarime.

"Kupitia mradi mpya wa uboreshaji wa elimu ya sekondari nchini, serikali imepanga kutumia Sh. bilioni 48.9 kwa ajili ya kuboresha elimu ya sekondari nchini," alisema.

Kadhalika, alisema katika shule zote tisa za sekondari zilizopo Halmshauri ya Mji wa Tarime, wanafunzi wanafanya mitihani ya masomo ya Sayansi kwa vitendo kwa kutumia maabara zilizopo.

Aidha, alisema maabara hizo zinakabiliwa na upungufu wa vifaa na huduma nyingine kama maji na gesi.




# Vijana 1,000 kutoka Zanzibar wajiunga JKT

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imesema kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita vijana 1,000 wamejiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kutoka Zanzibar kwa hiari.

Hayo yalielezwa jana bungeni na waziri wa wizara hiyo, Dk. Hussein Mwinyi, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Angelina Malembeka. Malembeka alihoji ni vijana wangapi kutoka Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Kaskazini B, wamepata nafasi ya kujiunga na jeshi kuanza mwaka 2015.

"Je, mgawanyo wa idadi ya vijana wanaojiunga na jeshi kwa kila wilaya nchini ukoje?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Dk. Mwinyi alisema vijana hao 1,000 ni kuanzia mwaka 2015 hadi 2018 na kwamba jukumu la kugawa nafasi hizo kwa wilaya liko chini ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Aidha, alisema kwa mwaka 2019/20 Zanzibar imetengewa nafasi 500.

"Mgawanyo wa idadi ya vijana wanaojiunga na JKT kwa kujitolea kwa kila mkoa huzingatia uwiano wa idadi ya watu kulingana na Takwimu za Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi, Elimu, Jinsia na sifa nyingine zinazokuwa zimeainishwa na Mkuu wa JKT," alisema.

Aliongeza: "Zoezi hili ikiwa ni pamoja na mgawanyo wa vijana hadi ngazi ya wilaya huratibiwa na wakuu wa mikoa husika baada ya Makao Makuu ya JKT kuainisha idadi ya vijana kwa kila mkoa."



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na Kaimu Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Verity Nyagah, alipomtembelea ofisini kwake bungeni, jijini Dodoma.

# Serikali yaendelea kupitia mikataba iliyoingia

BUNGE limeelezwa kuwa kwa sasa serikali bado inaendelea na mapitio ya mikataba yote iliyoingiwa ili kutambua kama vigezo na masharti katika mikataba hiyo vinatimizwa ipasavyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ileje (CCM), Janeth Mbene.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni mikataba mingapi imesitishwa na sekta ngapi zinaongoza, serikali imeingia gharama kiasi gani katika kesi zilizofunguliwa mahakamani kutokana na kusitishwa kwake.

"Je, serikali imepata faida au hasara gani kwa kusitisha mikataba hiyo," alihoji.

Akijibu maswali hayo, Waziri Mahiga, alikiri kuwa serikali imekuwa ikisitisha mikataba ya uwekezaji kutokana na sababu mbalimbali.

"Moja ikiwa ni upande mwingine wa mkataba kushindwa kutimiza masharti kwa mujibu wa mkataba au makubaliano ama inapobainika kulikuwa na udanganyifu ambao haukuwekwa wazi taarifa za msingi wakati wa kuingiwa kwa makubaliano au mkataba husika.

"Kwa sasa serikali bado inaendelea na mapitio ya mikataba yote iliyoingiwa ili kutambua kama vigezo na masharti katika mikataba hiyo vinatimizwa ipasavyo," alisema.

Aidha, alisema mara zoezi hilo litakapokamilika serikali itakuwa na takwimu sahihi ya mikataba yote iliyositishwa na kufanya tathmini ya gharama zote zilizotumika kwa kesi zilizofunguliwa kutokana na usitishwaji wake.

Dk. Mahiga alifafanua kuwa serikali kupitia hati idhini ya Rais iliyochapwa katika gazeti la serikali kwa Tangazo Na. 48 la mwaka 2018 na sheria ya marekebisho mbalimbali ya sheria ambayo pamoja na mambo mengine imerekebisha majukumu ya ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali(AG).

"Utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii umeboreshwa zaidi kwa kuanzishwa kwa idara itakayoshughulikia utekelezaji wa mikataba yote baada ya kufanyiwa mapitio na jukumu hilo litawezesha kutambua na kupata takwimu sahihi za mikataba yote iliyositishwa, inayotakiwa kusitishwa na inayotakiwa kufanyiwa marekebisho," alisema.

Alisema mabadiliko ya sheria hiyo yameanzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo kwa sasa inasimamia mashauri yote ambayo inashtaki au kushtakiwa.

Hata hivyo, alisema kwa sasa ofisi hiyo inaendelea na kazi ya utambuzi wa mashauri yote dhidi ya serikali kutoka katika wizara na taasisi zote za serikali.

"Jitihada zote hizi zina malengo ya kusaidia upatikanaji wa takwimu sahihi za mashauri yaliyofunguliwa kutokana na usitishwaji wa mikataba na kutambua faida na hasara zake," alisema.

## Tanroads yakerwa uharibifu taa za barabarani

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WAKALA wa Barabara Mkoa wa Arusha (Tanroads), umekerwa na uharibifu wa miundombinu ya taa za kuongozea magari unaofanywa na madereva wa magari wasiozingatia sheria na kanuni za usalama barabarani ambao wamekuwa wakigonga taa hizo na kukimbia.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Tanroads Mkoa wa Arusha, Mhandisi John Kalupale, alisema madereva hao, wamekuwa wakifanya uharibifu mkubwa katika barabara kuu ya Arusha, Moshi katika eneo la Sanawari, Mianzini na Philips.

Alisema hatua hiyo imekuwa ikiisababisha serikali hasara kwa kugharamikia ukarabati wa miundombinu hiyo.

Aidha, Kalupale aliwataka wananchi kushirikiana na serikali kuwabaini wahalifu wanaoharibu miundombinu hiyo.

"Uharibifu wa taa za kuongozea magari barabarani umekuwa ukisababisha msongamano mkubwa wa magari pamoja na kuleta ajali zisizokuwa za lazima," alisema Kalupale.

Hata hivyo, aliwataka madereva kuwa makini wakati wa uendeshaji wa vyombo vya moto barabarani kwa kuwa matukio mengi ya kugongwa taa hizo yamekuwa yakitokea nyakati za usiku.

Alisema kwa mtu atakayebainika kufanya uharibifu huo atapigwa faini Sh.300,000 hadi Sh. milioni moja na kufikishwa mahakamani.

Aidha, alieleza kuwa kucheleweshwa kwa matengenezo ya taa hizo kumetokana na fedha kuchelewa kuwafikia kwa wakati.

Alisema Tanroads ipo mbioni kuzifanyia taa hizo matengenezo ili kuzirejesha katika hali yake ya kawaida ziweze kuwaka kwa ajili ya kuondoa usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo.

Akizungumzia hali hiyo, alipotafutwa kwa njia ya simu, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Elius Mwakalinga, aliahidi kulishughulikia suala hilo, huku akisema kuwa hakuwa na taarifa ya kuwapo wa tatizo hilo.

**"Uharibifu wa taa za kuongozea magari barabarani umekuwa ukisababisha msongamano mkubwa wa magari pamoja na kuleta ajali zisizokuwa za lazima," alisema Kalupale.**

# Nassari akaribishwa kujiunga CCM

**Na Cynthia Mwilolezi ARUSHA**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM), Raymond Mwangwala, amemkaribisha aliyekuwa Mbunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Joshua Nassari kuingia katika chama hicho.

Ukaribisho huo aliutoa jana katika Kijiji cha Mbuguni, wilayani Arumeru wakati alipokuwa akitoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa wa aliyekuwa mfanyabiashara maarufu wa madini ya Tanzanite, Thomas Mollel, maarufu kwa jina la Askofu.

Alisema Nassari ni kijana mwenye uwezo mkubwa wa kifikra na hivyo anaamini katika hatua ya sasa atafanya maamuzi yalio sahihi kwa kuwa ni kijana.

"Mimi nawapa pole kwa msiba huu na nipo msibani hapa kumzika Askofu Thomas, lakini nitumie fursa hii pia kumkaribisha Nassari kuja CCM na mimi nitampokea maana nipo hapa Arusha," alisema.

Aidha, alimpongeza Mbunge mpya Dk. John Pallangyo, aliyeapishwa hivi karibuni bungeni Dodoma na kumtaka kufanya kazi za kuwaletea maendeleo wananchi.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Loata Sanare, alimtaka mbunge mpya kutekeleza mipango ya Askofu Thomas kwa kuwasaidia wahitaji wa jimbo hilo.

Alisema muda wa kupambana kisiasa umeisha na kiongozi amepatikana kilichobaki wote kushirikiana kuwaletea wananchi maendeleo.

"Tena nampongeza Nassari kwa kuja katika msiba wa kada wetu CCM na huo ndio uungwana tuliouzoea Tanzania hivyo sio mbaya nawe ukimuunga mkono marehemu Askofu Thomas kwa kujiunga CCM," alisema.

Sanare alisema marehemu alifanya mambo mengi mazuri ambayo vema kila kiongozi akamuenzi kwa kutekeleza ikiwamo kujali wahitaji kama yeye alivyotumia utajiri wake kusaidia wahitaji mbalimbali na kujenga shule na vituo vya afya.



Mshiriki wa kinyang'anyiro cha kumsaka mrembo wa Mkoa wa Arusha, Anna Fanuel (23), akiwapa elimu ya usafi wa mwili na kuwafundisha namna ya kuvaa taulo za kike wanafunzi na 1,000 wamepatiwa taulo hizo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wachimbaji wahofu muda wa kujenga uzio

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

WAMILIKI na wachimbaji wa madini ya tanzanite wa Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wameiomba serikali kuwapa mwaka mmoja ili waweze kuboresha miundombinu ya migodi yao ikiwamo kuweka uzio.

Wametoa tamko hilo baada ya baadhi ya migodi yao ambayo haina uzio iliyopo kitalu D na B (Opec) kuwekewa alama ya X na kuandikwa ondoa, vunja au fukia.

Wakizungumza kwenye kikao kilichofanyika jana, wachimbaji na wamiliki hao walisema wanaomba muda huo ili kufanikisha miundombinu yao kwa kuwa wengi wao wanakabiliwa na ukata.

Mmoja kati ya wachimbaji wa madini, Hamis Zacharia alisema wengi wao uchumi wao ni mdogo, hivyo wanaomba muda huo ili kutekeleza hilo kwa kuwa agizo hilo limekuja kipindi ambacho wana hali ngumu.

"Wachimbaji wadogo bado wanahitaji kuwa wakubwa baada ya kupata madini, hivyo tunaomba serikali ituongezee muda wa mwaka mmoja ili tutekeleze hilo," alisema Zacharia.

Mwenyekiti wa Kamati ya Tanzanite, Money Yousuph, alisema wachimbaji wamegawanyika kwenye matabaka tofauti kiuchumi hivyo wanaomba mwaka mmoja wa kutekeleza hilo.

"Ofisa madini mkazi wewe ni mlezi wetu na mchimbaji asiyekuwa rasmi mnamtambua na hamchukulii hatua kali na pia ukuta siyo kero ni tija tunaomba busara na hekima zako kwa kuwa sisi ni wasikivu," alisema Yousuph.

Mmoja kati ya wamiliki hao, Fatuma Kikuyu, alisema Ofisa Madini Mkazi, Daudi Ntalima, ameacha alama ikiwamo wachimbaji wengi wa madini ya tanzanite kulipa kodi bila shuruti na kutaka waongezewe mwaka mmoja.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini mkoani Manyara (Marema) tawi la Mirerani, Shwaibu Mushi, alisema ofisa madini mkazi Daudi Ntalima ni msikivu kwa kuwa amekuwa akiwajali wachimbaji madini hasa wadogo.

"Hata suala la mishahara ya wachimbaji madini alitutetea kuwa haliwezekani hivyo utaratibu wa kulipana kupitia asilimia 10 pindi madini yakipatikana uendelee," alisema Mushi.

Mmiliki mwingine, Mwanaidi Kimu alisema wanaomba mwaka mmoja wa kutekeleza hilo kwa kuwa wachimbaji wengi walianza kwa tabu, lakini sasa hivi wamepiga hatua kubwa.

Hata hivyo, Ofisa Madini Mkazi wa mkoa wa kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, alisema hawezi kutoa muda wa mwaka mmoja badala yake atawapa miezi sita ili watekeleze hilo.

Ntalima alisema migodi yote inapaswa kuwekwa uzio wa ukuta wa matofali au mabati ili kuimarisha usalama mgodini tofauti na kuwa wazi.

# Madereva Bajaj walia na ada, faini

Na Mwandishi Wetu, MOSHI

BAADHI ya madereva pikipiki zenye magurudumu matatu (Bajaj) katika Manispaa ya Moshi, wameulalamikia uongozi wa manispaa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (Sumatra) kwa kushindwa kusimamia maegesho ya pamoja na uwekwaji wa namba, hivyo kusababisha ugumu katika kufanya biashara hiyo.

Mmoja wa madereva hao, Frank Simon, alisema mbali na manispaa kushindwa kutoa utaratibu wa maegesho, pia kumekuwapo na chama ambacho hakitambuliki kisheria kinachowalazimisha wamiliki na madereva kujiunga kwa kiingilio cha Sh. 12,000, huku Sumatra wakitaka 10,000/-

Alisema mbali na kuwataka wa walipe Sh. 22,000 kwa mamlaka hizo mbili, pia wamekuwa wakipewa risiti za mkono hali inayoashiria ni ukiukwaji wa ulipwaji wa mapato.

"Sisi ni watafutaji wadogo wa pesa halali, lakini tunanyanyaswa na serikali kupitia viongozi wa Manispaa na Sumatra kwani hawatoi elimu sahihi ya nani anasimamia nini. Hali hii inasababisha mkoanganyiko mkubwa una upigwaji wa fini za mara kwa mara kwa kutumia chama hicho kisichotambulika na viongozi wake hatujawachakua sisi. Zaidi kabisa wanatoa risiti za mkono hali ambayo inaashiria kuna hujuma zinatendeka," alisema.

Naye Amos Lukas alisema: "Mbali na Sh. 12,000 ya kujiunga na kikundi ambacho hatukitambui pia tunalazimika kulipa Sh. 10,000 kwa ajili ya kuchorewa namba inayotoka Sumatra kinyume cha taratibu na sheria za nchi."

Mmoja wa abiria wanaotumia usafiri wa Bajaj, Ismail Kondo, alikiriki kunyanyaswa kwa baadhi ya madereva hao na kuiomba serikali kuhakikisha wanalifanyia kazi kwa uwazi na ukweli ikiwa ni pamoja na kuchukuwa hatua stahiki kwa watendaji wote wanokiuka matumizi ya mashine za kielektroniki ( EFD).

Ofisa Mfawidhi wa Sumatra Mkoa wa Kilimanjaro, Jones Makwale, alikanusha madai hayo kwa kusema ulipwaji wa pesa za Sumatra unatumika kwa njia zilizoainishwa kisheria na risiti za kielektroniki zinatolewa.

**"Sisi ni watafutaji wadogo wa pesa halali, lakini tunanyanyaswa na serikali kupitia viongozi wa Manispaa na Sumatra kwani hawatoi elimu sahihi ya nani anasimamia nini. Hali hii inasababisha mkoanganyiko mkubwa una upigwaji...**

# Waziri aingilia kati kiwanda cha kahawa

Na Mary Mosha, MOSHI

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, ameitaka Tume ya Ushirika nchini kukitazama kiwanda cha kukoboa kahawa cha Tanganyika Coffee Curing Company (TCCCo) Ltd, kilichoko Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro kwa jicho la ziada ili kuongeza uzalishaji.

Alitoa agizo hilo jana alipotembelea kiwanda hicho na kuahidi kuitisha kikao kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Moshi kwa lengo la kuangalia namna ya kukabiliana na changamoto zinazokikumba kiwanda hicho.

Alisema tume hiyo ina jukumu kubwa la kuhakikisha uzalishaji unaongezeka kwa kuwa kilikuwa na uwezo wa kukoboa tani 50,000 kwa mwaka, lakini sasa kinakoboa tani chini ya 1,000 kwa mwaka.

"Serikali ya awamu ya tano ni sikivu na imewekeza nguvu zake katika kuhakikisha inaendeleza viwanda, hivyo kikao tutakachokaa ni kwa ajili ya kuzungunzia kiwanda namna ya kuongeza uzalishaji ikiwa ni pamoja na kutoa hamasa kwa wakulima kuendelea kulima kahawa," alisema.

Kakunda pia aliomba mahakama kutenda haki kwa watu wote ambao wamehujumu zaidi ya Sh. bilioni 1.2 zilizotengwa kwa ajili ya kununulia mitambo na serikali imeshawafikisha katika mikono ya sheria.

"Inasikitisha kuona bodi zilizopita zimehujumu kiwanda hiki kwa madai ya kununua mitambo mipya wakati kuna mitambo yenye miaka 60 bado inatumika kukoboa kawaha. Hii nimeshuhudia leo (jana) na waliohujumu tunaomba mahakama kutenda haki," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya kiwanda hicho, Prof. John Boshe, alisema kwa sasa wanakabiliwa na changamoto ya kushuka kwa mapokezi ya kahawa kutoka tani 50,000 kwa mwaka hadi 900, kiwanda kukosa uwezo wa kifedha wa kujiendesha, hali inayosababisha kushindwa kulipa tozo mbalimbli za serikali kwa mujibu wa sheria na taratibu. Alisema pia kiwanda kinakabiliwa na muundo na mfumo wa watumishi usio na uhalisia, uamuzi na matumizi mabaya ya rasilimali za kiwanda ikiwamo uuzaji wa nyumba tatu na magari matatu ya kampuni zenye thamani ya Sh. bilioni 2.2.

"Kutokana na hali hiyo kiwanda kimeshindwa kulipa mishahara na stahiki za watumishi na hadi sasa kiwanda kina jumla ya madeni ya Sh. 1,272,189,484.77, hili ni tatizo na tunaomba serikali kuliangalia kwa namna ya pekee," alisema Profesa Boshe.



Wafanyakazi na baadhi ya wadau wa kampuni ya simu za mkononi Airtel Tanzania, wakichukua chakula kilichoandaliwa na kampuni hiyo kwa ajili ya futari katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, hafla iliyofanyika jana katika ofisi za Airtel Makao Makuu Morroco jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi walalamikia uongozi wa wilaya

Na Mary Mosha, MOSHI

ZAIDI ya wananchi 800 wa kijiji cha Uchira, Moshi mkoani Kilimanjaro, wameilalamikia serikali ya wilaya kwa kushindwa kuwawajibisha viongozi waliohujumu miradi miwili ya visima vya skimu ya umwagiliaji na mabwawa.

Miradi hiyo iko katika vijiji vya Uchira na Koresa yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 640.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye mkutano wa kijiji, wananchi hao walisema licha ya mradi huo kutumia fedha nyingi, umeshindwa kufanya kazi baada ya kujengwa chini ya kiwango.

Kutokana na uwapo wa ubadhirifu huo mkubwa kwenye miradi hiyo, wananchi hao wameiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kilimanjaro kuichunguza miradi hiyo ambayo imekwama tangu mwaka 2014, huku wananchi wakiendelea kukumbwa ukame.

Geofrey Mlay, alisema ujenzi wa miradi hiyo ulianza rasmi mwaka 2015, na kwamba katika awamu ya kwanza zilitolewa zaidi ya Sh. milioni 220 na awamu ya pili Sh. milioni 230 na awamu ya tatu fedha zilitolewa, lakini diwani na kamati yake hawataki kuweka wazi na miradi imekufa.

Alisema miradi hiyo kushindwa kukamilika imechangia kukwama kwa kilimo cha umwagiliaji katika kijiji hicho. Zaidi ya ekari 250 zimeshindwa kuendelezwa.

"Vijana waliokuwa wanayatumia mashamba hayo kulima mazao mbalimbali wameshindwa kufanya shughuli za kilimo huko wengi wamejiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kutokana na kukosa kazi," alisema Mlay.

"Miradi hii tulipokea mwaka 2014 kwenye kijiji tukachagua kamati ya kusimamia miradi hiyo, akiwamo mwenyekiti wa kijiji pamoja na diwani, lakini leo hii miradi imekufa kabisa hakuna kinachoendelea huko fedha nyingi zimeliwa na wajanja, tunamwomba Waziri Mkuu aingilie kati sakata hili wahusika wawajibishwe," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Uchira, Julius Mkojera, alisema kukwama kwa miradi hiyo kumesababisha zaidi ya ekari 220 kushindwa kuendelezwa licha ya eneo hilo kuwa na maji ya umwagiliaji.

Akijibu malalamiko hayo, Diwani wa Kirua Vunjo Kusini, Chata Madata, alikiri miundombinu hiyo kuhujumiwa na watu wachache na kwamba kuna haja ya kamati iliyoundwa kusimamia miradi hiyo kutoa taarifa za miradi hiyo ili kuondoa sintofahamu kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastori Msigala, ameahidi kufuatilia miradi hiyo na kwamba atatoa taarifa kamili baada ya uchunguzi.



Ukurasa 15

**Wajumbe Baraza la Wawakilishi wamlilia Ali Juma Shamuhuna**




Ukurasa 17

Rais Mutharika achaguliwa baada ya kushinda kesi katika mahakama




Ukurasa 18

**Changamoto za ANC na hatima ya 'vyama tawala' barani Afrika**

siasa

JUMATANO MEI 29, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 20

**ICC na tishio la kujitoa uanachama**

# Hukumu ya Mahakama kubatilisha wakurugenzi kusimamia uchaguzi

• Wangwe asema Mahakama imetenda haki • Ataka wenye dukuduku wasikae kimya, wakimbilie mahakamani

**Na Enock Charles**

HIVI karibuni, Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, ilitoa hukumu iliyobatilisha Wakurugenzi wa Halmashauri nchini kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Hiyo inafuatia kesi Namba 8/2018, iliyofunguliwa na mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Bob Chacha Wangwe ya kupinga wakurugenzi wa majiji, manispaa na halmashauri kuwa wasimamzi wa uchaguzi.

Katika kesi hiyo Wangwe aliwakilishwa na wakili wa kujitegemea Fatma Karume.

Hukumu hiyo imevuta hisia za watu wengi na kuripotiwa hata na vyombo vya habari vya kimataifa, kama vile BBC na DW.

Nipashe kupitia kwa mwandishi wake ilifanya mahojiano maalumu na Wangwe aliyefungua kesi hiyo katika Mahakama Kuu. Yafuatayo ni mahojiano hayo:

**SWALI: KESI ya Kikatiba uliyofungua Mahakama Kuu ya Tanzania kuhusu uhalali wa Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, halmashauri kusi-**

INAENDELEA UK.16



Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

**ACT-Wazalendo: Ukawa ni wenzetu lakini...** Ukurasa 19

# Mamlaka ya kijeshi Sudan yafikia mwafaka na wasomi wanaharakati

• Hata hivyo, mgawo wa madaraka bado



Kiongozi wa sasa wa Baraza la Kijeshi nchini Sudan, Luteni Jenerali Yasser al-Atta. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

VIONGOZI wa kijeshi wa Sudan wamefikia makubaliano ya awali na viongozi wa waandamanaji wanaosimamiwa na Sudan Professionals Association (Chama cha Wanataaluma) kuhusu muundo wa serikali ya mpito itakayosimamia nchi hiyo kwa miaka mitatu, kabla ya kufikia utawala halisi wa kiraia.

Kilichoafikiwa ni rahisi zaidi kwani ni idadi ya wajumbe watakaokuwa katika Baraza la Kutunga Sheria, kuwa theluthi mbili watatoka miongoni mwa raia (waandamanaji, wakiwakilisha makundi ya kijamii). Theluthi moja ndiyo watakaotoka jeshini.

Baraza la Mpito la Kijeshi (TMC) lilitangaza mwafaka huo na kueleza kuwa pande hizo mbili bado hazijakubaliana muundo wa Baraza la Taifa (Sovereign Council) ambako kila upande unataka uwe na wajumbe wengi zaidi.

Makubaliano hayo ndiyo hatua ya kwanza ya kutoa mwanga kuwa hali ya Sudan huenda ikatulia bila jeshi kupokonya kabisa ushindi wa wananchi kupitia 'maandamano yasiyoisha.'

Maandamano yaliyomng'oa madarakani aliyekuwa kiongozi wa nchi hiyo kwa miaka 30, Jenerali Omar al Bashir.

Katika hatua ya mwisho, waandamanaji wamekuwa wakipiga kambi nje ya makao makuu ya jeshi kutaka serikali ya kiraia ichukue madaraka.

> Na taarifa zingine zilisema kuwa wanajeshi walimshambulia kwa risasi mwandamanaji mmoja ambaye alikuwa amevaa sare za daktari.

Baraza hilo la kijeshi lilionyesha cheche za kutaka kutwaa madaraka kikamilifu kwa nguvu wakati waandamanaji watano walipouawa pale wanajeshi walipotumia risasi za moto.

Na taarifa zingine zilisema kuwa wanajeshi walimshambulia kwa risasi mwandamanaji mmoja ambaye alikuwa amevaa sare za daktari.

Hicho ni kielelezo cha hasira za jeshi kuwa wanataaluma kama hao wanaoheshimika nchini mwao katika maandamano, hivyo jeshi haliwezi kusema ni ya wahuni, wapigwe risasi waandamanaji watawanyike.

Hata hivyo, juhudi za kutumia nguvu, kama awali wakati wa Al-Bashir na nchini Algeria alivyoondolewa Rais Abdelaziz Bouteflika, hila hizo ziliisha na risasi hazikutumika tena. Jeshi linajua wakiua watu na kukamatwa, hawatapona.

Wakati taarifa ya kijeshi ilisema kuwa waandamanaji watano na mwanajeshi mmoja walifariki katika mapigano au ghasia jijini Khartoum, taarifa za vyombo vya habari hazionyeshi kuwa waandamanaji wametwaa silaha.

Zilisema kuwa risasi zilisikika katika eneo maandamano yalikofurika, na watu kadhaa walijeruhiwa, bila kuwapo dalili kuwa kulikuwa na mapigano, hivyo taarifa ya kifo cha mwanajeshi mmoja ilikuwa bado kinatiliwa mashaka.

Wachunguzi wa habari wanahisi kuwa taarifa za jeshi zina lengo la kuchochea waandamanaji kushika silaha za aina moja au nyingine, ili wapate kisingizio cha kuwaswaga kwa kudai kuwa nchi ipo hatarini.

Kiongozi wa hivi sasa wa Baraza la Kijeshi, Luteni Jenerali Yasser al-Atta alisema katika mkutano na waandishi wa habari kuwa makubaliano ya mwisho ya kugawana madaraka yatatiwa saini na mkusanyiko wa upinzani.

Mkusanyiko wa upinzani umepewa jina la Azimio la Uhuru na Mkondo wa Mageuzi (Declaration of Freedom and Change Forces) katika siku moja inayofuatia, ingawa hapakuwa na dalili kuwa mvutano kuhusu Baraza la Taifa (ni kama Baraza la Mawaziri, lakini bila katiba halisi, au mfumo wa uteuzi wa kikatiba) utamalizika haraka.

Kutoa saa 24 kwa suala hilo ilikuwa ni kuweka shinikizo kwa viongozi wa upinzani kutia saini haraka.

Jenerali Atta, akijaribu kuzungumza kwa niaba ya wananchi badala ya jeshi, alisema kuwa "tunawaahidi watu wetu kuwa makubaliano yatafikiwa kikamilifu ndani ya saa 24 katika njia ambayo inaafiki matazamio ya watu."

Ni kama kusema hakuna mgongano kati ya matazamio ya waandamanaji na jeshi, au 'watu' siyo wale waandamanaji na viongozi wao wanataaluma bali makundi ya itikadi kali yaliyolelewa na utawala wa Jenerali al-Bashir ambayo yako nyuma ya Baraza la Mpito la Kijeshi.

Isitoshe baraza hilo lilishaanza kutoa mwelekeo wa nchi katika sera na sheria zinazoendana na itikadi hizo, hata kabla ya kufikiwa mfumo wa kugawana madaraka.

Baraza la Kutunga Sheria litakuwa na wajumbe 300 ambako DFCF watakuwa na theluthi mbili za wajumbe, hali inayomaanisha kuwa maamuzi ya Baraza la Taifa hayawezi kupitishwa na baraza hilo lenye hadhi ya Bunge endapo yatakuwa yameshinikizwa tu na jeshi.

Bado hakuna dalili kuwa raia wataongoza Baraza la Taifa au kama maamuzi yake yote yategemea baraza lote kukubali, hali ambayo ina maana kuwa jeshi likiwa linasimamia baraza hilo la juu linaweza kupitisha maamuzi ya sera, bila baraza lote kukubali.

Endapo ingebidi yafikishwe Baraza la Kutunga Sheria (kwa mfano ili bajeti ya sera hiyo ipitishwe) ni wazi yangekwama.

Kiongozi wa waandamanaji, Taha Osman alisema kuwa pande hizo mbili zimekubaliana mfumo wa utawala utakaoundwa, yaani Baraza la Taifa, Baraza la Mawaziri na Baraza la Kutunga Sheria, mfumo ambao Jenerali Atta hakuonekana kuutilia mkazo.

Kiongozi mwingine wa upinzani alieleza matumaini kuwa makubaliano kamili ya kugawanya madaraka yatafikiwa punde, bila kugusa 'saa 24' alizoashiria Jenerali Atta.

Mjumbe wa timu ya majadiliano ya DFCF Sadiq Yousuf alisema kuwa mpangilio wa wajumbe katika Baraza la Kitaifa la wajumbe 11 bado ulikuwa unaendelea, mfumo unaoonyesha kuwa baraza hilo ndilo ambalo litahitaji kutanguliza makubaliano kwa hatua zozote muhimu za sera, halafu mawaziri wawajibike kila mtu kivyake.

Katika hatua za kwanza za majadiliano, jambo la kushangaza ni kuwa Baraza la Kijeshi la Mpito lilitaka kuwe na kipindi cha mpito cha miaka miwili, wakati viongozi wa vyama vya kitaaluma vinavyounda uongozi wa maandamano walitaka miaka minne ya serikali ya mpito.

Sababu ni kuwa kipindi hicho kinapokuwa kifupi, uchaguzi ukifikiwa ni miundombinu ya kisiasa ya utawala wa Jenerali al-Bashir itakayokuwa na uwezo zaidi wa kujumuisha wafuasi wake, kama ilivyokuwa Misri baada ya kuondolewa madarakani Rais Hosni Mubarak kutokana na 'maandamano yasiyoisha' na kutumia nguvu dhidi ya waandamanaji.

Ukafanyika uchaguzi ndani ya miezi sita ulioshuhudia vitendo vya kutumia nguvu kupata ushindi kwa makundi ya itikadi kali.

Mvutano mkubwa uko katika idadi ya wajumbe wa kijeshi na wa kiraia katika baraza la juu la kitaifa, ambako kwa muda wa takriban wiki moja hakuna mabadiliko katika madai ya pande zote mbili, au kubadilika kwa misimamo.

Jeshi linataka wajumbe saba watoke jeshini na wanne uraiani wakati viongozi wa makundi ya waandamanaji wanataka saba watoke uraiani na wanne jeshini.

INAENDELEA UK.15

# Wajumbe Baraza la Wawakilishi wamlilia Ali Juma Shamuhuna

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

'HAKIKA kila nafsi itaonja umauti', ni kauli ya baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kupokea taarifa ya kifo cha aliyekuwa mjumbe wa Baraza hilo na Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Ali Juma Shamuhuna.

Wajumbe hao wa Baraza la Wawakilishi walipokea taarifa ya msiba wa kiongozi huyo aliyefariki Mei 19 mwaka huu, wakiwa katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi juzi.

Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Dk. Mohamed Said Dimwa, anamtaja marehemu Ali Juma Shamuhuna kama kiongozi jasiri, aliyefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwenye wizara na idara mbalimbali alizoteuliwa kuziongoza.

Anasema Shamuhuna atakumbukwa kwa utendaji wa majukumu yake ya kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Donge kwa uadilifu mkubwa kwa vipindi vitatu akiwa mwakilishi wao.

"Kila nafsi itaonja mauti... tunapaswa kumkumbuka mwenzetu ambaye alikuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na waziri aliyefanya kazi zake kwa uadilifu mkubwa," anasema.



Ali Juma Shamhuna (aliyesimama), enzi za uhai wake akiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, akisisitiza jambo wakati alipozungumza na wazazi katika ziara yake ya kutembelea shule mbalimbali za Unguja na Pemba. **PICHA: MTANDAO**

**HAMZA HASSAN JUMA**

Mwakilishi wa jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma anamtaja Shamuhuna kama mwalimu wake aliyempatia mbinu mbalimbali za kuihoji na kuibana Serikali, wakati wa kupitisha bajeti za Serikali kwa kuhoji vifungu vya fedha.

Anasema wakati marehemu Shamuhuna alipokuwa mwakilishi wa kawaida, alimuongoza mbinu za kuibana na kuihoji Serikali zaidi katika kupitisha vifungu vya matumizi ya fedha za Wizara mbalimbali.

"Marehemu Shamuhuna alikuwa mwalimu wa wajumbe wengi na alitusaidia kwa kutupatia mbinu na ujuzi wa kuendesha shughuli za Baraza la Wawakilishi na vikao vyake," anasema.

**WAZIRI ABOUD**

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa , Mohamed Aboud, anasema Shamuhuna atakumbukwa na Baraza la Wawakilishi kwa mchango na uadilifu wake mkubwa wakati akiwa waziri na mwakilishi wa Jimbo la Donge.

"Marehemu hatasahaulika kwa kuweka mbele uzalendo na maslahi ya taifa kwa ustawi wa wananchi wote na hasa wa Jimbo la Donge," anasema.

> Ni Abdelaziz Bouteflika aliondolewa madarakani mwezi uliopita, kwa njia ya katiba kumaliza maandama-

Waziri Aboud anasema serikali pamoja na Chama cha Mapinduzi (CCM) kimepata pigo kubwa la kuondokewa na mkongwe na mwasisi huyo wa chama tawala.

"Kwa kweli ni msiba mkubwa wa kuondokewa na ndugu Shamuhuna ambaye alishika nyadhifa tofauti serikalini...lakini ndio kazi ya Mungu haina makosa," anasema.

**WASIFU WA ALI JUMA SHAMUHUNA**

Alizaliwa katika Kijiji cha Donge, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Januari Mosi mwaka 1944.

Katika uhai wake, Marehemu Shamuhuna alipata elimu ya Msingi katika shule ya Kiembe Samaki iliyoko Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na Shule ya Msingi ya Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja mwaka 1952 hadi 1959.

Mwaka 1959 hadi 1963, alisoma kidato cha kwanza hadi cha nne katika shule ya Sekondari ya Lumumba.

**ELIMU YA JUU**

Kwa upande wa elimu ya juu, Marehemu Shamuhuna alisoma Diploma ya juu (Diary Technology), kisha shahada ya kwanza (B.SC- Animal Production) mwaka 1977 hadi 1980.

Mwaka 1981 hadi 1982, Marehemu alisoma Shahada ya Umahiri ama Uzamili (M.B.SC- Animal Genetics and Breeding).

Aidha, mwaka 1992 hadi 1996, alisoma Shahada (B.A Economic Inter Trade).

**AJIRA**

Kwa upande wa ajira, Marehemu aliwahi kuwa Meneja Mkuu katika Shamba la Mifugo Kizimbani mnamo mwaka 1966 hadi 1969.

Akawa Meneja Mkuu wa Shamba la Wanyama Kizimbani, Tunguu, Pangeni na Hanyegwa Mchana, kuanzia mwaka 1969 hadi 1976.

**USHIRIKA**

Marehemu Shamuhuna aliwahi kuwa Meneja Mkuu wa Ushirika wa Uzalishaji wa Wanyama kati ya mwaka 1981 hadi 1985.

Baada ya hapo akateuliwa kuwa Mkuu wa Mradi wa "World Food Programme" ulioendeshwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la (UNDP) mwaka 1985 hadi 1988, kabla ya kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo mwaka 1988 hadi 1990.

**KISIASA**

Kwa upande wa nafasi za Kisiasa, Marehemu Shamuhuna alikuwa Mwanachama mwaminifu wa CCM akishika nyadhifa mbalimbali.

Alikuwa Mhasibu katika Tawi la Kwahani mwaka 1981 hadi 1985, kisha Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa mwaka 1985 hadi 2012.

Marehemu Shamuhuna aliwahi kuwa Mjumbe wa Kuteuliwa kwa uteuzi wa Rais katika Baraza la Wawakilishi (BLW) mwaka 1995 hadi 2000.

Aidha, aliwahi kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia (BLW) mnamo mwaka 1995 hadi 2000.

**TUME YA MWAFAKA**

Katika majukumu mbalimbali aliyoyashika, ni pamoja na la kuwa Kamishna wa Tume ya Mwafaka 2001 hadi mwaka 2002.

Alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Donge mwaka 2000 hadi 2015 na kisha akastaafu shughuli za kisiasa.

**UWAZIRI**

Marehemu Shamuhuna amewahi kushika nyadhifa mbalimbali za Uwaziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na kuwa Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Aidha, aliwahi kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Waziri wa Ardhi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango.

Marehemu ameacha watoto tisa na kizuka mmoja.

Mwenyezi Mungu ailaze mahala pema peponi, roho ya Marehemu Ali Juma Shamuhuna, Amin.

## Mamlaka ya kijeshi Sudan yafikia mwafaka na wasomi, wanaharakati

**INATOKA UK.14**

Nje ya suala la idadi ya wajumbe wa baraza hilo kutoka upande mmoja au mwingine, bado kuna tatizo la uongozi wa baraza lenyewe, bado kuna tatizo la nani ataongoza baraza lenyewe, na licha ya matazamio chanya, inaelekea wanajeshi wameshinda hapo, watasimamia.

Ina maana kuwa kimsingi Sudan inaingia katika mazingira ya kisiasa ambako mamlaka halisi yako mikononi mwa jeshi, ikiwamo kiongozi halisi wa serikali ya mpito na zaidi kidogo ya nusu ya baraza la juu la taifa.

Kuna kipengele kuwa mkusanyiko wa upinzani ndiyo utakaotoa majina ya wajumbe wa Baraza la Mawaziri, ingawa sera na maamuzi halisi yatakuwa kwa baraza la juu.

Kinachoonekana ni kuwa Baraza la Kijeshi la Mpito linataka liendelee katika hali hiyo kama ilivyo sasa, liingize tu wajumbe kadhaa wa kiraia ambao inaweza kusikiliza kiasi fulani maoni yao lakini maamuzi yawategemee wao.

Hali hiyo ingegusa kila kitu ila kwa masuala ambayo yanaweza kuzua kuvurugika kwa makubaliano, suala ambalo Baraza la Kutunga Sheria haliwezi kukubali, pamoja na kuwa wajumbe hao wa Baraza la Juu la Taifa (ambalo kimsingi linakuwa liko chini ya uongozi wa jeshi) watakuwa chini ya shinikizo kutorudisha nchi katika machafuko.

# Hukumu ya Mahakama kubatilisha wakurugenzi kusimamia uchaguzi



Baadhi ya viongozi wa upinzani nchini, Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba (kushoto), Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe (katikati), na Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia. PICHA: MTANDAO

INATOKA UK.13

**mamia uchaguzi na hatimaye hukumu ikatolewa ikikubaliana na hoja zako, imekuwa gumzo kila mahali nchini na nje ya nchi pia, unadhani ni kwanini?**

**JIBU:** SABABU kuu ni kwamba Mahakama imetenda haki, haki ambayo kwa kweli watu wengi sana imewagusa, kwa sababu Watanzania wengi wanachohitaji ni kuwa na uchaguzi ambao ni huru na wa haki. Kwa hiyo kwa kupiga marufuku wakurugenzi ambao wanafungamana na chama ambacho kipo madarakani, lazima kwa vyovyote vile ingepokewa kwa msisimko wa hali ya juu sana .

**SWALI: Kwa maoni yako kutokana na ushindi huo, Je, imekuongezea ari ya kuendelea kupigania vifungu vingine vinavyolalamikiwa na upinzani nchini kama vile matokeo ya Rais kupingwa mahakamani?**

**JIBU:** Imeniongezea ari ya kuendeleza mapambano ya kidemokrasia na utawala bora, lakini zaidi ninafuraha kwamba imeongeza juhudi hata jamii imeona kwamba, hizi jitihada za mahakamani za kupigania haki na kujaribu kuzuia sheria ambazo ni mbovu zinawezekana. Kwa hiyo naamini kwamba huko tunakoelekea haitakuwa ni Bob (Wangwe) tu au Fatma (Karume) peke yake, naamini tutakuwa wengi.

> …sasa nakuhakikishia endapo utawezesha mradi huo kukamilika, hakuna legacy (urithi) kubwa utakayokuwa umeacha kama hiyo kwa jiji letu.




Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma.



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage.

**SWALI: Serikali imesema inaenda Mahakama ya Rufaa dhidi ya hukumu hiyo, nini maoni yako?**

**JIBU:** Kwanza imekata rufaa kwa sababu ni haki yake ya Kikatiba kufanya hivyo kwa mujibu wa ibara ya 13 ya Katiba, kwa upande ambao haujaridhishwa na maamuzi kukata rufaa, lakini pili inaweza kuwa inashangaza sana kwa sababu tuanaamini kuwa viongozi wa Serikali hasa Rais, Waziri Mkuu, Wabunge waliapa kwa kutumia Katiba na vitabu vyao vya dini kwamba watailinda na kuihifadhi Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa inapokuja kuwa Mahakama Kuu inabaini kuwa Sheria fulani iliyotungwa inavunja Katiba, haikutarajiwa kwa Serikali kupinga hasa kwa kuwa Serikali ipo kwa ajili ya wananchi na maamuzi haya yamefanyika kwa nia njema ya kutetea wananchi kwa hiyo binafsi naishangaa Serikali.

**SWALI: Kwa hali ya kisiasa ilivyo nchini tunapoelekea uchaguzi mwaka huu wa serikali za mitaa na mwakani kwa upande wa Rais, Wabunge na Madiwani huku upinzani ukizidi kupungua makali na makada wake kuhamia chama tawala, kuna nafasi ya upinzani kushinda au vita ya upinzani sasa ihamie mahakamani?**

**JIBU:** Hali ya Kisiasa ni ngumu kwa sababu wananchi wa Tanzania na wanasiasa hawawajibiki vya kutosha kwa sababu kuna msemo unaosemwa ambao uliwahi kusemwa na Friedrick Douglas kwamba "Power concedes nothing without the demand never will never did" kwamba 'bila kudai, mtawala hawezi kutoa au kukubali' kwa hiyo tunavyoona hali ngumu ni kwa sababu hatujatimiza wajibu wetu vizuri, wanasiasa hawajatimiza wajibu wao vizuri, wanaharakati hawajatimiza wajibu wao vizuri na wananchi hawajatimiza wajibu wao vizuri wa kupambana na kudai yale mambo ambayo ni ya msingi kwa Taifa hili.

**SWALI: Nini maoni yako kwa Mahakama ya Tanzania baada ya uamuzi huu?**

**JIBU:** Maoni yangu na ushauri kwa Mahakama zetu ni kuendelea kutenda haki kwa sababu hiyo ndio kazi yao ya msingi na ndio jukumu lao la kikatiba na wanaapa kwa kutumia vitabu vya dini kwamba itakuwa ni chombo ambacho kinatoa haki. Kinapaswa kuendelea kufanya hivyo bila kutishwa, bila kuogopa, bila rushwa pamoja na changamoto zilizopo ziwe za rushwa, ziwe za kuingiliwa na mhimili wa Serikali, Mahakama isimame imara na kuendelea kutoa haki. Jambo la pili, Majaji na mahakimu wanapaswa kuiga mfano wa jopo la Majaji ambao wameamua hii kesi.

**SWALI: Unawashauri nini Watanzania wenye dukuduku na vifungu vinavyokinzana na Katiba ?**

**JIBU:** Watanzania hawatakiwi kuwa na madukuduku, wanatakiwa wachukue hatua. Wewe ambaye una dukuduku unalalamika unachukua hatua gani? Unamlaumu nani? Kwa sababu ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imetupa wajibu wa kuilinda na kuihifadhi Katiba yetu. Kwa hiyo pale ambapo inaonekana kuna sheria mbovu, maana sheria inatakiwaisikinzane na Katiba ambayo ni sheria mama. Kwa hiyo wanatakiwa kwenda Mahakamani bila kujali nafasi zao katika jamii. Tunatakiwa tufanye hivyo badala ya kuwa na dukuduku.

**SWALI: Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema utaratibu wa kuwatumia wakurugenzi utaendelea kwa kuwa tayari ameshakata rufaa kuhusu kesi hiyo, unasemaje?**

**JIBU:** Si sahihi kwa sababu huo sio utaratibu wa Sheria kwani tunaongozwa na Sheria zetu. Nasikitika sana kwa sababu sijui Mwanasheria Mkuu ametoa wapi hicho kifungu, lakini kwa mujibu wa Katiba yetu hiyo haiwezekani. Kilichopo sasa hivi ni amri ya Mahakama, kwa hiyo tunachoangalia ni Mahakama imesema nini sio Mwanasheria Mkuu amesema nini .

**SWALI: Kwa uelewa wako wa masuala ya sheria, ni kwa namna gani utekelezaji wa hukumu unaweza kusimama?**

**JIBU:** Utekelezaji wa hukumu hasa kwa kesi za Kikatiba unaweza ukasimama kwa namna mbili. Namna ya kwanza ni kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuomba kusimamisha hiyo hukumu kwa hoja za msingi na Mahakama kuridhia ombi lake. Namna ya pili ni pale ambapo wanatoa notisi ya Kukata rufaa kwenye mashauri ya Kikatiba yale ambayo hayana athari endelevu. Lakini yenye athari endelevu kama hili la kwetu ambapo kuruhusu wakurugenzi kusimamia chaguzi maana yake ni kuwa athari zinaendelea, hiyo haipo kwa interpretation (tafsiri) yake ni wrong (makosa).

**SWALI: Watu wangependa kufahamu Bob Wangwe ni nani baada ya hukumu hii katika uga wa kisiasa ?**

**JIBU:** Bob Wangwe ni kijana wa pili wa Marehemu , Chacha Wangwe aliyewahi kuwa mbunge wa Tarime kati ya mwaka 2005 na 2010, kabla mauti hayajamfika na pia aliyewahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema). Mimi ni mzaliwa wa Kemakorere Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara. Nimesoma Shule ya msingi Sabasaba (2000-2006), Kidato cha kwanza hadi cha nne, nimesoma Shule ya Sekondari Msangani iliyopo Kibaha 2007 -2010 na Kidato cha tano na sita, Saint Mathew Kongowe 2011 Kibaha, 2013 nilijiunga na JKT Kambi ya Mlale Songea na mwaka huohuo nilijiunga na chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa masomo ya Shahada ya Sheria niliyohitimu 2017.

Kwa sasa ni Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania.

> Taarifa zilizopo ni kuwa itachukua miezi 18 kutengeneza mitaro ili maji yasiingie kwenye makazi.

**SWALI: Una malengo ya kisiasa na kama yapo ni yapi?**

**JIBU:** Malengo yangu mimi ni kuendelea kuitumikia nchi yangu kwa nafasi yoyote ile na kwa muda wowote mpaka nitakapokufa na kupigania ustawi wa nchi yangu.

**SWALI: Ikitokea Rais John Magufuli akakuteua kuwa mkurugenzi wa halmashauri yoyote nchini, utapokea uteuzi huo?**

**JIBU:** Nitakubali endapo tu Rais ataunda Tume huru ya kusimamia chaguzi ili nitakapokuwa natekeleza majukumu yangu, nitekeleze bila kuvunja Katiba ya nchi lakini vilevile kutokuwa sehemu ya kubaka maamuzi ya wananchi kupitia chaguzi.

## Rais Mutharika achaguliwa baada ya kushinda kesi katika mahakama

RAIS wa Malawi, Peter Mutharika, amepata ushindi mwembamba unaomwezesha kusalia madarakani kwa awamu ya pili.

Kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 78, alikumbana na upinzani mkali katika uchaguzi uliofanyika Mei 21.

Profesa Mutharika ametangazwa mshindi baada ya kupata asilimia 38.5 ya kura zote.

Matokeo yalicheleweshwa baada ya kinara wa upinzani Lazarus Chakwera aliyepata asilimia 35.4 ya kura zote, kwenda mahakamani kupinga uchaguzi huo akidai ulikuwa na kasoro lukuki.

Matokeo ya uchaguzi huo yametangazwa juzi jioni baada ya Mahakama Kuu kutupilia mbali shauri la upinzani. Tangazo la Mkuu wa Tume ya Uchaguzi ya Malawi (MEC), Jane Ansah, linaonyesha kuwa Mutharika wa chama cha DPP alipata ushindi mwembamba kwa kumshinda mpinzani wake mkuu Chakwera wa MCP kwa kura 159,000.

Makamu wa Rais wa Mutharika, Saulos Chilima, alimaliza katika nafasi ya tatu, akifanikiwa kupata asilimia 20 ya kura zote.

Awali alidai kuwa jina lake halikuwamo kwenye karatasi ya kupigiwa kura kwa wagombea wa urais. Ikiwa inakabiliwa na makali ya umaskini, mustakabali wa uchumi na rushwa ndizo zilikuwa mada kuu za uchaguzi huo. Uchaguzi huo ulikuwa ndio mgumu zaidi na usiotabirika katika historia ya taifa hilo.

Waliopiga kura ni asilimia 74 ya raia milioni 6.8 waliojiandikisha kwenye daftari la wapigakura.

Malawi ilipata uhuru wake kutoka kwa Mwingereza mwaka 1964. Huu ulikuwa ni uchaguzi wa sita wa urais nchini humo toka utawala wa chama kimoja kumalizika mwaka 1994.




Wagombea urais Lazarus Chakwera (kushoto) na Saulos Chilima (katikati) waliokuwa wakichuana na Rais Mutharika (kulia). **PICHA: MTANDAO**

Chama cha MCP kilikimbilia mahakamani kikitaka matokeo yasitangazwe wakidai kuna makosa lukuki, ikiwamo wizi wa kura.

MCP ilitaka kura zirudiwe kuhesabiwa walau kwenye majimbo 10 ya uchaguzi kati ya 28. Katika baadhi ya maeneo kulikuwa na tuhuma za kubadilishwa kwa kura kwa kutumia wino maalumu.

Zuio la kutangazwa matokeo ya awali lilikubaliwa na mahakama baada ya tume kupokea ripoti 147 za upungufu. Ripoti hizo zilisababisha baadhi ya maeneo, hususani ngome za wapinzani kukumbwa na maandamano, shirika la habari la Reuters linaripoti.

Makamu wa Rais pia amesema kulikuwa na upungufu mkubwa katika uchaguzi huo. Licha ya ripoti hizo, mahakama ilitupilia mbali ombi la upinzani na kuruhusu matokeo yatangazwe.

**RAIS MUTHARIKA NI NANI?**

Rais Mutharika, ni mwanasheria na mwanataaluma kwa ngazi ya profesa. Amekuwa kiongozi wa taifa hilo dogo la Kusini mwa Afrika, kutokea 2014.

Amepata elimu yake nchini Uingereza na Marekani, na amekuwa kwenye ulingo wa siasa za nchi hiyo toka mwaka 2008, ambapo aliteuliwa kuwa mshauri mkuu wa sheria na kaka yake aliyekuwa rais wa nchi hiyo kwa wakati huo.

Alikamatwa mwaka 2013 pamoja na baadhi ya mawaziri kwa tuhuma za kutaka kumpindua mrithi wa kaka yake.

Kuelekea uchaguzi huo, umri na afya ya Mutharika viliangaziwa sana na kuna ambao waliozusha kuwa amefariki ambapo ilibidi akanushe uvumi huo.

Upinzani pia ulidai kuwa ufisadi umetamalaki katika kipindi chote ambacho Mutharika amekuwa madarakani.

Rais huyo alishawahi kuhusishwa na kashfa ya rushwa, lakini akasafishwa na mamlaka ya kupambana na ufisadi ya nchi hiyo. **BBC**

# Changamoto za ANC na hatima ya 'vyama tawala' barani Afrika

Na Mashaka Mgeta

AFRIKA Kusini imefanikiwa kuhitimisha Uchaguzi Mkuu wake wa mwaka huu na kukiwezesha chama tawala cha African National Congress (ANC) kurejea madarakani.

Uchaguzi Mkuu huo uliofanyika Mei 8, mwaka huu, ulikuwa wa sita tangu kumalizika kwa utawala wa ubaguzi wa rangi uliokuwa chini ya makaburu na kufikia ukomo wake miaka 25 iliyopita.

ANC ilipata ushindi wa jumla kwa asilimia 57.5 na kufuatiwa na chama cha Democratic Alliance (DA) chenye wazungu wengi kilichopata asilimia 20.8, wakati chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) cha Julius Malema kikiwa na asilimia 10.8.

Matokeo hayo yakaonyesha kuwa vyama vingine vidogo vikiwamo Inkatha Freedom Party (IFP), Freedom Front Plus (FFP), African Christian Democratic Party (ACDP) na United Democratic Movement (UDM) vilifanikiwa kupata nafasi za uwakilishi bungeni.

Pia kulikuwa na vyama ambavyo kwa mara ya kwanza vilifanikiwa kupata nafasi za uwakilishi bungeni ikiwa ni pamoja na GOOD kinachoongozwa na aliyekuwa Meya wa Jiji wa Cape Town, Patricia de Lille na African Transformation Movement cha aliyewahi kuwa Msemaji wa Serikali, Mzwanele Manyi.

**MAJIMBO**

Matokeo ya majimbo yalionyesha kuwa ANC ilifanikiwa kupata ushindi mkubwa kwenye mikoa mingi isipokuwa Western Cape ambapo chama cha DA kiliendelea 'kulikamata' jimbo hilo.

ANC ilipoteza uungwaji mkono na wengi huko Gauteng kwa kupata ushindi wa asilimia 50.19.

Mfano mwingine ni majimbo ya Limpopo, Mpumalanga na Eastern Cape ambapo ANC ilipata theluthi mbili na kupata ushindi wa zaidi ya asilimia 50 kwenye majimbo ya Free State, Northern Cape na KwaZulu Natal.

Kwa upande wake, EFF kilifanikiwa kupata upinzani rasmi kwenye majimbo matatu ya Limpopo, Mpumalanga na North West.

Chama cha IFP, kikawa kambi rasmi ya upinzani katika Jimbo la Kwa Zulu Natal wakati DA ikiwa katika hali hiyo kwenye majimbo mengine isipokuwa Western Cape ilipopata ushindi.

Ingawa ANC ilishinda, lakini ushindi huo mdogo ambao haijawahi kuupata tangu kuanzishwa kwake, umetafsiriwa kwa namna tofauti na wachambuzi mbalimbali wa masuala ya siasa na uongozi ndani na nje ya bara la Afrika.

Wapo wanaoutafsiri ushindi huo kama 'mafanikio ambayo hayakutegemewa', kutokana na sababu kadhaa zilizokidhoofisha chama hicho ikiwamo kashfa zilizowaandama baadhi ya viongozi wa ANC, hususani aliyekuwa kiongozi wake, Rais aliyeondoka madarakani, Jacob Zuma.

Zuma alikabiliwa na kashfa mbalimbali zilizohusiana na masuala ya ufisadi, akafikia hatua ya 'kuachia ngazi' na nafasi yake kuchukuliwa na aliyekuwa Makamu wa Rais na




Kiongozi wa Chama cha Economic Freedom Fighters (EFF), Julius Malema (picha ikiwa imebebwa), ambacho kimepata asilimia 10.8. katika uchaguzi mkuu nchini Afrika Kusini ambapo ANC ilishinda kwa asilimia 57.5. **PICHA: MTANDAO**

> Vijana wengi waliopo upinzani hawazipendi siasa za ANC, hivyo ni dhahiri kwamba waliojitokeza, walikipigia kura chama cha EFF.

ambaye kwa sasa ndiye Rais wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa.

**MKOKO**

Mhadhiri wa Shule ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), aliyeko Afrika Kusini, Egbert Mkoko, anasema kama uchaguzi huo ungefanyika kati ya miaka miwili hadi mitatu iliyopita, ANC ingepata ushindi wa asilimia za chini zaidi kuliko ilivyo mwaka huu.

"Hali ndani ya ANC haikuwa shwari kwa kipindi hicho na viongozi wake akiwamo Zuma walikabiliwa na tuhuma mbalimbali za ufisadi, hali ambayo ingewaathiri sana kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kama mabadiliko yasingefanyika na kumfanya Ramaphosa kuiongoza ANC," Mkoko alisema na kukaririwa na idhaa ya Kiswahili ya radio Dutch Welle (DW) ya Ujerumani.

Mkoko anasema pamoja na upinzani hasa vyama vya DA na EFF kutofanikiwa kuingia Ikulu, bado vina mchango mkubwa kwa mchakato wa demokrasia, maendeleo na ustawi wa taifa hilo lililopo Kusini mwa Afrika.

Anatoa mfano kuwa, chama cha DA kilichofanikiwa kuitwaa ngome yake ya Jimbo la Western Cape na hasa Jiji la Cape Town, inajivunia mafanikio katika kupunguza kadhia ya ukosefu wa ajira na kuimarisha usalama jimboni humo.

Katika Afrika Kusini, vijana waliojiandikisha na kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, walizungumzia kadhia hiyo ya ukosefu wa ajira wakati ambapo takwimu nchini humo, zikionyesha kwamba ukosefu wa ajira umefikia asilimia 27.

"Ingawa Jimbo la Western Cape linakaliwa na wazungu wengi, lakini kwa mfumo wa siasa na utawala wa Afrika Kusini, mafanikio hayo yanahesabika kuwa ya nchi na raia wake," anasema Mkoko.

**KOMU**

Mchambuzi mwingine, Isack Komu anasema ushindi mdogo wa ANC unaweza kuchangiwa na wanachama na wafuasi wake wachache kujitokeza kupiga kura.

"Vijana wengi waliopo upinzani hawazipendi siasa za ANC, hivyo ni dhahiri kwamba waliojitokeza, walikipigia kura chama cha EFF," anasema.

Taarifa zisizopaswa kupuuzwa kwa matokeo ya uchaguzi huo ni kwamba hasira za baadhi ya wapigakura kuhusu kashfa za kushamiri kwa rushwa kwa baadhi ya viongozi wa ANC na washirika wao na kushindwa kuboresha uchumi wa nchi hiyo ulioteteteka ni miongoni mwa sababu za ANC kupata ushindi 'kiduchu' katika Uchaguzi Mkuu huo.

Miongoni mwa raia waliodhihirishwa kukerwa na mwenendo wa siasa na uongozi wa ANC ni Thabo Makhene, anathibitisha kuwa mfuasi wa chama cha ANC, lakini hakukipigia kura katika Uchaguzi Mkuu huo.

"Wanastahili kuzinduka...namna wanavyoliendesha taifa, kutumia vibaya fedha za umma, wamepoteza maadili yao," Makhene alisema alipohojiwa na shirika la habari la Reuters.

**MAKABURU**

Afrika Kusini ilikuwa katika muda mrefu wa utawala wa makaburu uliokithiri kwa ubaguzi wa rangi uliopendelea wazungu na kuwakandamiza weusi tangu mwaka 1948 hadi 1994.

Upendeleo huo unatajwa kuhusisha masuala mbalimbali ya kiuchumi ikiwamo umiliki wa ardhi kwa idadi ndogo ya wazungu kuliko idadi kubwa ya raia weusi nchini.

Pengine, kwa kutambua hali hiyo ndio maana chama cha EFF cha Malema kimeongoza katika 'kupigana' ili kuondokana na tatizo hilo la umiliki wa raslimali za nchi hiyo hasa ardhi.

Shirika la Habari la Uingereza (BBC) limeripoti kwamba mwandishi wake, Andrew Harding aliyekuwa jijini Johannesburg, alisema msimamo wa chama ulilazimu ANC kufikiria kuchukua hatua kali kukabidhi ardhi zaidi kwa haraka mikononi mwa raia weusi pasipo kutoa ahadi ya kuwalipa fidia raia weupe (wazungu).

Lakini, chama kikuu kingine cha upinzani, DA kinachosadikiwa kuwa na wazungu wengi, hakiamini kwamba mageuzi katika suala la ardhi ni muhimu sana likahusisha kupora watu ardhi yao na kuwamilikisha wengine.

**'VURUGU' ZA MALEMA**

Akijulikana zaidi kama "mwana wa kiasili", Malema ameshiriki kujenga mifumo na 'kuivisha' itikadi katika kipindi cha miaka sita ya kuanzishwa kwake, hivyo kuwapata 'makamanda' wenye nidhamu na wanaotambua namna bora ya kufanya utetezi na kufikisha ajenda na sera zao kwa umma.

Malema, mwanasiasa kijana mwenye umri wa miaka 38, alifukuzwa kutoka chama tawala cha ANC mwaka 2012.

**MAPAMBANO YA ANC**

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa ANC ndicho kilipambana dhidi ya utawala wa kibaguzi chini ya uongozi wa Nelson Mandela na hivyo kuwa sababu inayoaminika kuungwa mkono na raia weusi wengi wa Afrika Kusini.

**DHANA YA UBAGUZI**

Wakati ANC ikitambulika kuwa kinara wa kupiga vita ubaguzi wa rangi, baadhi ya viongozi wake wakajitokeza kutoa kauli zilizoashiria ubaguzi katika uchaguzi huo.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ace Magashule ni miongoni wanaotajwa kujihusisha na hali hiyo alipowatamkia wapigakura, "usipoteze kura yako tena kwa mtu mweupe."

Kwa ujumla, matokeo ya Uchaguzi Mkuu huo yanaibua hisia nyingi, kubwa zaidi ni ujumbe kwa 'vyama tawala' hasa vilivyoshiriki harakati za kudai uhuru barani Afrika kutambua mabadiliko ya kijamii yanayowapasa kubadili namna ya kufanya siasa ndani ya vyama hivyo, ili kukidhi matakwa ya walio wengi.

*Makala haya yameandikwa kutoka vyanzo tofauti na mwandishi wake anapatikana kupitia simu namba 0754691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.*

# ACT-Wazalendo: Ukawa ni wenzetu lakini...

Na Sabato Kasika

MWISHONI mwa mwaka jana, viongozi wa vyama vya upinzani nchini Tanzania walikutana visiwani Zanzibar kwa mwaliko wa mwanasiasa mkongwe, Maalim Seif Sharif Hamad.

Baadhi ya vyama hivyo ni ACT-Wazalendo, NCCR-Mageuzi, Chama cha Ustawi wa Umma (Chauma), National League for Democracy (NLD) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Miongoni mwa maazimio yaliyotolewa na vyama hivyo ni kuutangaza mwaka 2019 kuwa ni wa kudai demokrasia na kuunganisha makundi ya wananchi nchi nzima ambayo ni pamoja na ya wafanyakazi.

Wengine wanaotakiwa kuunganishwa ni wakulima, wanafunzi na wavuvi kwa pamoja kupigania haki na kurudisha demokrasia kwa nguvu zao zote.

Ndani ya vyama hivyo, vimo vile vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), ambavyo ni Chadema, NLD na NCCR- Mageuzi.

Awali Ukawa ilikuwa inaundwa na vyama vinne, lakini sasa vimebaki vitatu baada ya CUF kujiweka pembeni.

Hata hivyo, umoja huo umepata marafiki wengine ambao ni ACT-Wazalendo na Chauma.

Katibu wa Uenezi wa ACT- Wazalendo, Ado Shaibu anafunguka kuwa hiyo haina maana kwamba chama chao kiko ndani ya Ukawa, bali huo ni ushirikiano ambao unatosha kuufanya upinzani kupiga hatua zaidi kwa ajili ya ushindi.

"Sisi ACT-Wazalendo hatuko Ukawa, lakini tunashirikiana nao, ndio maana tulikuwa pamoja kule Zanzibar na pia yapo mambo mengi tu ambayo tumekuwa tukishirikiana kama wapinzani," anasema.

Anasema ushirikiano wa upinzani uliopo sasa ni zaidi ya Ukawa, hivyo hawana budi kuuendeleza ili baadaye uweze kuwa na matokeo mazuri kwa maendeleo ya vyama hivyo.




Msemaji wa Chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu. **PICHA: MTANDAO**

### MSIMAMO WA CHAMA

Anataja msimamo wa ACT- Wazalendo kuwa ni kushirikiana na vyama vingine vya siasa ili kufanikisha malengo ya kuleta mapinduzi ya kiuchumi na kwamba ndio maana walifanya mkutano wa pamoja visiwani Zanzibar.

"Yaani niseme kwamba msimamo wetu upo wazi na huwa tunaueleza mara kwa mara kuwa tunaunga mkono juhudi zozote za kushirikiana kwa vyama, kwani hili linathibitishwa na jina letu Alliance," anasema.

Shaibu anasema chama hicho kinataka ushirikiano unaonufaisha wananchi na si ushirikiano wa kugawana nafasi za uongozi.

Anabainisha kwamba wapo tayari kushirikiana na chama chochote kilicho tayari kushirikiana nao ili kuiangusha CCM.

"Kwa kuwa vyama vinavyounda Ukawa tunavyo kwenye ushirikiano, basi hao ni wenzetu, lakini siyo kwamba chama chetu kiko Ukawa...jambo la kuzingatia ni kwamba Ukawa ni wenzetu lakini hatupo ndani ya Ukawa," anasema.

> Kwa mfano kuna makubaliano yaliwahi kufanywa kati ya ACT-Wazalendo na Chadema wa kushirikiana katika uchaguzi mdogo wa jimbo la Buyungu mkoani Kigoma.

Anafafanua kuwa kuwa ndani ya Ukawa ni lazima misingi ya kiitikadi na kifalsafa izingatiwe katika ushirikiano na kwamba wapo tayari kwa umoja na kwamba umoja ni moja ya misingi mikuu 10 ya chama chao kwani umoja ni nguvu.

Shaibu anasema kuna baadhi ya mambo ambayo chama hicho kinashirikiana na vingine vya upinzani ambavyo vilikutana Zanzibar, kwa kuwa vyote vina lengo moja la kushika dola kwa njia ya uchaguzi halali.

"Kwa mfano kuna makubaliano yaliwahi kufanywa kati ya ACT-Wazalendo na Chadema wa kushirikiana katika uchaguzi mdogo wa jimbo la Buyungu mkoani Kigoma," anasema.

Anafafanua kuwa Chadema nao waliunga mkono mgombea udiwani wa ACT- Wazalendo katika Kata ya Gehandu, wilayani Hanang, mkoani Manyara.

"Nina uhakika huko tuendako tutafikia pazuri kwani makubaliano ya ACT- Wazalendo na Chadema yaliyofanyika kwa ajili uchaguzi mdogo wa jimbo la Buyungu, ilikuwa ni mwanzo wa kuelekea katika uundwaji wa kitu kinaitwa The United Democratic Front (DeFront)," anasema.



Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe. **PICHA: MTANDAO**

### AZIMIO LA ZANZIBAR

Februari mwaka huu chama mshirika cha Chadema kilikaririwa na vyombo vya habari kikisema kinafanya uratibu na kupanga ratiba ili kuanza mikutano ya hadhara kama walivyoazimia walipokutana Zanzibar.'

Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vicent Mashinji ndiye aliyekaririwa akisema hayo ingawa serikali ilishapiga marufuku mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa na kuruhusu viongozi wa kuchaguliwa tu katika maeneo yao husika.

Marufuku hiyo imekuwa ikilalamikiwa na vyama vya upinzani na wadau wa demokrasia nchini kwamba inapingana na katiba na sheria, ingawa wanalazimika kuiheshimu.

Kutokana na hali hiyo, Chadema kinasema kinafanya uratibu na kupanga ratiba ili kianze mikutano ya hadhara nchi nzima kama walivyoazimia katika 'Azimio la Zanzibar.'

Wakati kikiwa na mkakati huo ambao pia unatakiwa kufanywa na vyama vingine vya upinzani vilivyokutana Zanazibar mwishoni mwa mwaka jana, tayari Wizara ya Mambo ya Ndani imeshatoa tahadhari kwa vyama hivyo.

### KAULI YA SERIKALI

Serikali inaonya kuhusu azimio la vyama vya siasa vya upinzani vilivyokutana Zanzibar, kwamba hiki ni kipindi cha kuchapa kazi uchaguzi umekwisha na sasa ni muda wa wananchi kuchapa kazi.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yussuf Masauni anasema:

"Kwa kuzingatia hilo nasisitiza vyombo vya dola hususan polisi kuwa macho na kuhakikisha hakuna uvunjifu wowote wa sheria unaofanyika. Hatuwezi kukubali watu wahatarishe amani ya nchi," anasema.

Masauni amewataka wapinzani waiache serikali ya Chama Chama Mapinduzi (CCM) iliyopewa dhamana na wananchi ifanye kazi zake, na anatoa wito kwa polisi kudhibiti vitendo vyovyote vya uvunjifu wa amani vitakavyofanywa na vyama hivyo huku akisema serikali itaendelea kusimamia sheria na taratibu ilizojiwekea.

# ICC na tishio la kujitoa uanachama

**Na Mwandishi Wetu**

KUANZISHWA kwa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kibinadamu (ICC), kulikotokana na Mkataba wa Rome wa Julai 17, mwaka 1998 na kuanza kutekelezwa Julai Mosi, 2002, kulitarajiwa kufikia mafanikio mengi, ikiwamo kudhibiti vitendo vya uhalifu huo.

Vitendo hivyo vilivyoripotiwa kutokea katika nchi mbalimbali duniani na kudaiwa kufanywa na baadhi ya viongozi waliopo madarakani, na wengine wanaochochea, kufadhili ama kuchangia kwa namna nyinginezo wakiwa nje ya mifumo ya utawala.

Lakini ikiwa katika mchakato wa kupeleleza, kuunda mashtaka na kuwafikisha washukiwa wa vitendo hivyo kwenye mahakama hiyo iliyopo Hague nchini Uholanzi, baadhi ya nchi wanachama zikaanza kukosoa utendaji kazi wake.

Zilitumia kigezo cha kuwalenga washukiwa katika nchi zinazoendelea hususani barani Afrika na kuwaacha 'mabwana wakubwa' wa dunia wakishiriki pasipo kuwaguswa.

Dhana hiyo ikachagiza kasi ya nchi wanachama kupuuzia maagizo ya ICC hasa kuhusu kuwatia nguvuni washukiwa wanaotakiwa kufikishwa kwenye mahakama hiyo.

Pia miongoni mwa nchi wanachama zikasimama kidete kutaka kujitoa kwenye mkataba wa Rome, ingawa zilishindwa kutokana na sababu kadhaa ikiwamo mchakato mrefu uliopo kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha mahakama hiyo.

Itakumbukwa kwamba barani Afrika, nia ya nchi wanachama kujitoa ilikolea zaidi pale Kenya ilipotaka kujitoka ICC baada ya raia wake sita waliojulikana zaidi kama 'Ocampo Six' kufikishwa kwenye mahakama hiyo.

Raia hao wa Kenya akiwamo Rais wa sasa, Uhuru Kenyatta na Makamu wake, William Ruto walidaiwa kuchochea, kufadhili na kufanikisha machafuko yaliyotokea nchini humo baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2007.

Wengine waliotajwa na aliyekuwa mwendesha mashtaka wa ICC kwa wakati huo, Luis Moreno Ocampo ni aliyekuwa Waziri wa Viwanda, Henry Kosgey, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Francis Muthaura, mtangazaji wa redio, Joshua arap Sang na Kamishna mstaafu wa Polisi, Mohammed Hussein Ali.

Wakati huo Kenyatta alikuwa Naibu Waziri Mkuu wa serikali iliyoongozwa na Rais (mstaafu) Mwai Kibaki, wakati Ruto alikuwa Waziri wa Elimu na Mbunge wa Eldoret Kaskazini.

Serikali ya Kenya iliyoongozwa na Kibaki, ikamtuma aliyekuwa Makamu wa Rais, Kalonzo Musyoka kuzunguka nchi mbalimbali akitafuta kuungwa mkono ili nchi hiyo ijitoe ICC.

Kilichoelezwa kuisukuma Kenya kufikia hatua hiyo, ilikuwa ni fikra kwamba Kibaki alitaka kuwanusuru washirika wake, Kenyatta na Ruto ambaye licha ya kuwa Mbunge kupitia chama cha upinzani cha Orange for Democratic Change (ODM), alikuwa kwenye mgogoro dhidi ya kiongozi wa chama hicho na Waziri Mkuu (kwa wakati huo), Raila Odinga.

Iliaminika kwamba kama Kenyatta na Ruto wangehukumiwa na kufungwa kutokana na tuhuma zilizowakabili huko ICC zikiwamo mauaji, kujeruhi na uharibifu wa mali uliofanyika baada ya Uchaguzi Mkuu huo, Odinga angepata 'mteremko' kushinda katika uchaguzi huo.




Mwendesha Mashtaka Mkuu wa ICC, Fatou Bensouda ambaye amepigwa marufuku kuingia Marekani. **PICHA: MTANDAO**

> Mahakama hiyo ikajiridhisha kwamba kiasi cha takribani watu 1,200 waliuawa, maelfu wakafungwa magerezani na maelfu wengine kuteswa huku mamia ya raia wa nchi hiyo 'wakipotezwa'.

Lakini mashtaka ya washukiwa hao yalishindwa kuthibitishwa mahakamani na hivyo kwa nyakati tofauti, 'Ocampo Six' wakajikuta wameachiwa huru.

### AL BASHIR ALIVYOKWEPA KUKAMATWA

Lakini wakati hali ikiwa hivyo, Rais wa Sudan aliyeng'olewa madarakani kwa 'nguvu za umma', Omar al- Bashir alichochea mgogoro kati ya ICC na baadhi ya nchi wanachama zilizogoma kumkamata na kumfikisha kwenye mahakama hiyo.

Uamuzi huo ukatafsiriwa kuwa ni ukiukwaji wa mkataba wa Rome, hivyo kwa nchi ya Jordan itakayoelezwa baadaye kwenye makala haya, ikatakiwa 'kushtakiwa' kwenye mkutano wa wakuu wa nchi wanachama na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC).

Sura ya 27(2) ya Mkataba wa Rome inaeleza kwamba hakuna kinga kwa mshukiwa wa makosa yanayotajwa kwenye mkataba huo kukamatwa, hata kama atakuwa katika wadhifa wa urais kwenye taifa lake, hivyo Al-Bashir alipaswa kuchukuliwa hatua hiyo alipofanya ziara kwenye nchi mwanachama wa ICC.

Al Bashiri alikuwa akituhumiwa kwa makosa ya mauaji ya kimbari yaliyofanyika dhidi ya makundi ya kikabila ya Fur, Masalit na Zaghawa.

Makosa hayo ni pamoja na kuua, kujeruhi kimwili na kiakili na kuchochea kwa makusudi kwa kila kundi hali ambayo ilisababishwa kusambaratika kwa makundi hayo.

### NCHINI AFRIKA KUSINI

Afrika Kusini ni miongoni mwa nchi zilizokumbwa na kadhia ya kutomkamata Al Bashir hadi pale Mahakama ya Pretoria, ilipoamuru asitoke nchini humo mwaka 2015 kusubiri uamuzi kuhusu kukamatwa kwake.

Al Bashiri alikuwa nchini humo kushiriki mkutano wa viongozi wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) na aliripotiwa kuondoka Afrika Kusini usiku ili kukwepa asikamatwe.

### JORDAN NAYO 'IKAMKINGIA KIFUA'

Sakata la mzozo kati ya ICC na Al Bashir likaikabili pia Jordan ambayo Mei 6 mwaka huu, ICC ilijulishwa na ofisi ya mwendesha mashtaka wake kuwa utawala wa kifalme wa nchi hiyo ulishindwa kumkamata kwa kipindi chote alichokuwa Rais na kufanya ziara nchini humo.

Jordan ilisaini na kuwa mwanachama wa Mkataba wa Rome tangu mwaka 2002.

Miongoni mwa ziara zinazotajwa kufanywa na Al-Bashiri huko Jordan pasipo 'kutiwa nguvuni' ni ile ya Machi 29, mwaka juzi, alipohudhuria mkutano wa mataifa ya Kiarabu nchini humo.

Majaji walio na mtazamo tofauti na uamuzi uliochukuliwa walieleza kutoridhwa na uamuzi uliofikiwa dhidi ya Jordan kwa kigezo kwamba haukuwa wenye taswira ya adhabu ama vikwazo dhidi ya taifa hilo.

Hivyo hatua ya majaji hao ikatafsiriwa kuwa rai ya kuchukuliwa hatua zaidi zinazolenga kuchagiza ushirikiano kwa ICC na kutambua kiwango kikubwa cha misingi na malengo yanayoainishwa kwenye Mkataba wa Rome.

### BURUNDI MIKONONI MWA ICC

Novemba 9, mwaka juzi, chemba iliyoundwa na majaji Chang-ho Chung (Jaji Kiongozi), Antoine Kesia-Mbe Mindua na Raul Pangalangan, ilitoa agizo la kisheria kwa mwendesha mashtaka wa ICC kuanza uchunguzi kuhusu makosa ya jinai yanayodaiwa kufanywa nchini Burundi wama na raia wake waliopo nje ya nchi hiyo kwa kipindi cha kati ya Aprili 26, 2015 hadi Oktoba 26, mwaka juzi.

Hata hivyo, mwendesha mashtaka alikuwa na mamlaka ya kuongeza muda wa upelelezi wake kwa makosa yaliyofanywa kwa kipindi hicho ikiwa mahitaji kadhaa ya kisheria yangefikiwa.

### KUJITOA ICC

Oktoba 28, mwaka juzi, Burundi ilijitoa rasmi ICC ikiwa ni mwaka mzima baada ya nchi hiyo kuwasilisha kusudio lake hilo kwenye mahakama hiyo.

Waziri wa Sheria wa Burundi, Aimé Laurentine Kanyana, akazungumzia hatua hiyo na kusema si ajabu kufanya hivyo na haijamanisha kwamba makosa ya jinai ambayo yangeshughulikiwa na ICC ama makosa mengine hayatoadhibiwa na taasisi za sheria nchini humo.

Burundi ilieleza kuwa hatua hiyo ilifikiwa kwa vile ICC imekuwa ikishughulikia kesi za viongozi wa Afrika pekee na kwamba imekuwa kama chombo cha nchi za magharibi cha kuzikandamiza nchi za Afrika.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Mkataba wa Rome, nchi mwanachama inapojiondoa kutoka ICC haiwezi kunusurika dhidi ya mashtaka yaliyoanza kuchunguzwa kabla ya hatua hiyo, na hivyo hatua ya Burundi isingeweza kuifanya mahakama hiyo isitishe mchakato wake dhidi ya makosa yanayodaiwa kufanyika nchini humo.

Ni kwa hali hiyo, ICC ikawa na mamlaka ya kuendelea na uchunguzi ama mashtaka kwa makosa yanayodaiwa kutokea Burundi wakati Taifa hilo lililopo ukanda wa Afrika Mashariki, likiwa mwanachama wa Mkataba wa Rome.

Pia Burundi ikatakiwa, kwa mujibu wa mkataba huo, kushirikiana na ICC kwa masuala yanayohusu uchunguzi wa matukio ulioanza Oktoba 25, mwaka juzi, kabla ya kujiondoa kwake rasmi.

Burundi ilikubaliana na masharti hayo wakati ilipo saini na kuuridhia Mkataba wa Rome.

Katika uchunguzi uliofanyika nchini humo, ICC ikaridhika kwamba vithibitisho vya mwendesha mashtaka vilionyesha kuwapo umuhimu wa kuendelea kwa mashtaka ya watuhumiwa wa makosa dhidi ya ubinadamu yanayodaiwa kufanyika nchini humo.

Miongoni mwa makosa hayo ni mauaji, utesaji, ubakaji, watu 'kupotezwa' na unyanyasaji vilivyofanyika katika kipindi cha kuanzia angalau Aprili 26, 2015.

Mahakama hiyo ikajiridhisha kwamba kiasi cha takribani watu 1,200 waliuawa, maelfu wakafungwa magerezani na maelfu wengine kuteswa huku mamia ya raia wa nchi hiyo 'wakipotezwa'.

Idadi ya watu waliokimbia makazi yao katika kipindi cha Aprili 2015 na Mei mwaka juzi (kwa mujibu wa ICC) walibainika kuwa 413,490.

Makosa hayo yakadaiwa kufanywa na taasisi za serikali ya nchi hiyo ndogo katika ukanda wa Afrika Mashariki na vikundi vingine vinavyounga mkono sera za watawala likiwamo Jeshi la Polisi, Idara ya Intelijensia na vitengo vya jeshi la nchi hiyo.



HABARI MBEYA

# Wazazi CCM yaonya utafunaji fedha

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, Dk. Edmond Mndolwa, amewataka viongozi na watendaji wa Chama Cha Mapinduzi kuacha tabia ya kutafuna fedha za miradi ya chama hicho badala yake zitumike kunufaisha jumuiya na wanachama wake.

Mndolwa aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake mkoani Mbeya ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM pamoja na kukagua miradi ya Jumuiya ya Wazazi zikiwamo shule za sekondari na kuzungumza na Baraza la Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Mbeya.

Alisema chama kinatoa fedha za miradi kwa lengo la kuwanufaisha wanachama wake na kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo, lakini sio kuwanufaisha wachache.

"Chama hakitamvumilia kiongozi au mwanachama yeyote ambaye atabainika kutafuna fedha za miradi, lazima ashughulikiwe, tunahitaji kuijenga CCM sisi wenyewe alisema," Dk. Mndolwa.

Aidha, Dk. Mndolwa aliishauri Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Mbeya, kuachana na makundi ambayo yanaendelea kuwagawa badala yake washikamane kukijenga chama.

Aliwataka wanachama kujitathmini na kuiga mfano wa mikoa mingine kwa kuwa na mshikamano na upendo ili uchaguzi ujao ishinde mitaa yote.

"Tunaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa hatutaki kupoteza hata mtaa mmoja tunataka CCM ishinde kwa kishindo ," alisema Dk. Mndolwa.

**"Chama hakitamvumilia kiongozi au mwanachama yeyote ambaye atabainika kutafuna fedha za miradi, lazima ashughulikiwe, tunahitaji kuijenga CCM sisi wenyewe alisema," Dk. Mndolwa.**

# Dk. Mwakyembe atoa msaada tani sita za chakula

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, ametoa msaada wa tani sita za chakula kwa wananchi wa maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, walioathiriwa na mafuriko yaliyoua watu watano na kuwaacha wengine zaidi ya 2000 bila makazi.

Mbali na chakula hicho pia alitoa msaada wa magodoro, mablanketi na mashuka kwa familia zilizopoteza makazi kutokana na mafuriko hayo hasa familia za watu wasiojiweza wakiwamo wazee na watu wenye ulemavu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika uwanja wa Shule ya Sekondari Mwaya, baada ya kukabidhi misaada hiyo kwa wananchi wa vijiji vitatu vya Kata ya Mwaya, Mwakyembe alisema amepata misaada hiyo kwa kuchangiwa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya.

Mwakyembe ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kyela, alisema misaada hiyo ya chakula pamoja na vitu vingine ililenga kuwanufaisha zaidi wazee, wenye ulemavu na watu wengine ambao hawajiwezi ili kupunguza ukali wa maisha baada ya mafuriko kusomba chakula na mali zao zingine ikiwamo mifugo.

"Wadau mbalimbali wameniunga mkono akiwamo Naibu Spika Dk. Tulia Akson, kupitia taasisi yake ya Tulia Trust, vyakula ambavyo tumeleta ni mchele, unga, maharage na sukari na kila mlengwa anachagua chakula anachotaka apewe," alisema Dk. Mwakyembe.

Pia aliwaomba wadau mbalimbali kuendelea kujitolea misaada ya hali na mali kwa ajili ya wananchi hao kwa madai bado kuna mahitaji mengi yanahitajika ikiwamo vifaa kwenye shule za msingi na sekondari.

Baadhi ya wananchi waliopata misaada hiyo walimshukuru Mwakyembe kwa kuwakumbuka, huku wakimuomba aendelee kuwashawishi wadau wengine kuwasaidia ili waondokane na adha wanazopata.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Masebe, Saimon Mwakibuje, alisema katika kijiji chake wananchi wanaohitaji msaada wa haraka walikuwa 108 na wote walinufaika na msaada uliopelekwa na Mwakyembe.

Alimshukuru mbunge huyo kwa kuacha shughuli zingine za kitaifa na kuamua kwenda kuwasaidia wananchi wake ambao waliathirika na mafuriko kwa kuwapatia chakula na vitu mbalimbali ikiwamo vifaa vya kulalia.

"Tunajua kuwa kwa sasa vikao vya Bunge vinaendelea Dodoma, lakini Mheshimiwa Mwakyembe ameamua kuviacha na kuja kutoa misaada kwa wananchi walioathirika na mafuriko, tunamshukuru na tunaomba aendelee na moyo huo," alisema Mwakibuje.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Ngusa, alisema chanzo cha mafuriko hayo ni mabwawa yaliyopo katika eneo la Tenende ambayo hayana mifereji ya kupeleka maji katika Ziwa Nyasa.

Alisema kutokana na kutokuwapo kwa mifereji hiyo, maji yakijaa yanaanza kurudi kwenye makazi ya wananchi na hivyo kuleta maafa kama ilivyotokea hivi karibuni.

Aliiomba serikali kuwasaidia kutengeneza mifereji hiyo ili kuepuka madhara hayo kuwa endelevu kwa wilaya hiyo na kusema idadi kubwa ya mashamba yameharibika kutokana na mafuriko hayo.

Kuanzia Aprili 29, mwaka huu mpaka katikati ya mwezi Mei, wananchi wa kata nane za Wilaya ya Kyela walikumbwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zilizokuwa zinanyesha katika Wilaya ya Rungwe hali iliyosababisha watu watano kupoteza maisha na wengine 2,570 kukosa makazi.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (kulia), akimkabidhi msaada wa chakula mmoja wa wazee wa Kijiji cha Malungo, wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya walioathiriwa na mafuriko ya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TGNP yaadhimisha Siku ya Hedhi kwa mdahalo

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP-Mtandao) kwa kushirikiana na mashirika ya Plan International, Femina Hip na wadau wengine, wamefanya maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani kwa kuandaa mdahalo wenye lengo la kuongeza uelewa wa mabinti kuhusu hedhi salama na kuwapa mtazamo chanya kuhusu hedhi na hali ya binti.

Akizungumza kwenye mdahalo huo uliowahusisha wanafunzi wa vyuo vikuu, shule za msingi na sekondari kutoka jijini Dodoma, Ofisa Programu wa TGNP-Mtandao, Deogratius Temba, alisema mdahalo huo umetoa nafasi kwa wanafunzi kuibua changamoto mbalimbali zinazowakabili wanapokuwa hedhi.

Alisema miongoni mwa changamoto zilizoibuliwa na wanafunzi hao ni pamoja na mazingira ya kujifunzia kutokuwa rafiki kwao hasa wanapokuwa kwenye hedhi hali inayosababisha washindwe kuhudhuria baadhi ya vipindi vya masomo darasani. Ikiwa ni Siku ya Maadhimisho ya Hedhi Salama Duniani yenye kaulimbinu isemayo, "Wakati wa kuchukua hatua, tenga rasilimali kuwezesha upatikanaji wa mahitaji ya hedhi salama shuleni," TGNP-Mtandao, Plan International na Femina hip pamoja na wadau wengine wa hedhi nchini wameandaa 'Kilinge Salama' kama jukwaa linalolenga kuwapa nafasi wanawake na mabinti kuzungumza kuhusu masuala ya hedhi," alisema Temba.

Aliongeza kuwa ili kuendana na kaulimbiu ya mwaka huu inayohimiza hedhi salama shuleni, wameishauri serikali kutenga bajeti ya ununuzi wa pedi hasa kwa wanafunzi wa sekondari za umma ambako kumeripotiwa changamoto nyingi. Pia walihamasisha wanawake na mabinti kuvunja ukimya wanapokuwa kwenye hedhi, kupata sauti za mabinti ili wazitumie kushawishi watunga sera na watekeleza sera umuhimu wa hedhi salama.

Alisema watahakikisha wanaunda kikosi kazi cha wadau wa hedhi kutoka wizara mbalimbali zinazohusika na masuala ya hedhi, wabunge, wawakilishi wa vyuo vikuu na wawakilishi wa shule za msingi na sekondari.

Akizungumzia maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alisema kwa kutambua umuhimu wa hedhi salama kwa mtoto halmashauri yake imeongezeka bajeti ya ununuzi wa pedi kutoka Sh. milioni moja hadi Sh. milioni 7.5.

Alisema lengo la kuongeza bajeti ya ununuzi wa pedi ni kuwafikia wanafunzi wote wa shule za sekondari za serikali ili isiwe kikwazo cha kushindwa kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu nao walipongeza hatua mbalimbali zinazofanywa na wadau kuhusu masuala ya hedhi salama, walisema imeleta chachu na kuwakumbusha wazazi wajibu wao.





# Nacte yafungua udahili wa wanafunzi kada huduma afya

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BARAZA la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), limefungua udahili wa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na shahada, huku likisitisha udahili wa wanafunzi wa kada ya huduma ya afya ngazi ya jamii kwa mwaka wa masomo 2019/20.

Hatua hiyo, imetokana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kulielekeza baraza hilo kuwa kwa mwaka huu hakutakuwa na udahili wa wanafunzi wapya wa kada hiyo hadi hapo itakapotangazwa tena.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mkuu wa Kitengo cha Udahili Nacte, Twaha Twaha, alisema utaratibu uliopo mafunzo yote ya kada ya afya yanasimamiwa na wizara hiyo, hivyo wamepokea maelekezo hayo ya kusitisha udahili.

Awali, Mkurugenzi wa Uzingativu, Ufuatiliaji na Tathmini wa baraza hilo, Dk. Jofrey Oleke, alisema baraza hilo limefungua rasmi udahili wa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na stashahada kwa kozi zote isipokuwa ualimu.

"Udahili umefunguliwa rasmi leo (jana) na utaendelea hadi Septemba 2, mwaka huu, kwa vyuo vyote vinavyotoa mafunzo katika ngazi hizo," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa waombaji wa kozi za afya katika vyuo vya serikali watatakiwa ama kuomba moja kwa moja kupitia vyuo ambavyo vitawasajili kupitia 'Institutional panel' (jopo) la chuo husika.

"Pia wanaweza kuomba kupitia tovuti ya Nacte, na kwa waombaji wa programu za afya kwenye vyuo visivyo vya serikali na waombaji wa programu nyingine zote watatakiwa kuomba moja kwa moja kwenye vyuo husika," alisema.

Alisema vyuo hivyo vitapokea maombi na kufanya uchaguzi wa wanafunzi wenye sifa kisha kuwasilisha Nacte majina ya waliochaguliwa kwa ajili ya uhakiki kabla ya kuyatangaza.

Alitoa wito kwa wahitimu wa elimu wenye sifa ya kuomba kozi hizo kufanya maombi kwa makini ili kupata nafasi ya kujiunga kozi wanazozipenda.

# Chuo Bandari kupitia mitaala

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

CHUO cha Bandari kimeanza kupitia upya mitaala ya kozi mbalimbali zinazotolewa na chuo hicho ili kuendana na mahitaji ya sasa.

Mapitio hayo yanatarajiwa kukamilika mwezi ujao.

Hayo yalielezwa jana na Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Joseph Kakeneno, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya vyuo vya ufundi yanayoendelea jijini hapa.

Alisema chuo kimeamua kufanya mapitio upya ya mitaala baada ya kufanya utafiti wa kina kuangalia kama mitaala ya sasa inakidhi mahitaji.

"Hasa sasa baada ya kuwapo kwa ongezeko la teknolojia na mahitaji ya soko ya sasa na matokeo ya utafiti tulioufanya umetufanya kufanya mapitio upya ya mitaala yetu kwa kozi tunazotoa ili kuwa na mtaala ambayo itaendana na hali ya sasa na mahitaji ya soko na mabadiliko ya teknolojia," alisema.

| 800 | 458 | T | 3,237,500 |
| 801 | 459 | T | 1,991,500 |
| 802 | 460 | T | 2,852,500 |
| 803 | 461 | T | 2,047,500 |
| 804 | 462 | T | 2,074,000 |
| 805 | 463 | T | 2,072,000 |
| 806 | 464 | T | 1,809,500 |
| 807 | 465 | T | 22,925,000 |
| 808 | 466 | T | 1,564,500 |
| 809 | 467 | T | 1,453,500 |
| 810 | 468 | T | 1,954,500 |
| 811 | 469 | T | 1,806,000 |
| 812 | 470 | T | 1,515,500 |
| 813 | 471 | T | 1,536,500 |
| 814 | 472 | T | 138,000 |
| 815 | 473 | T | 2,054,500 |
| 816 | 474 | T | 934,500 |
| 817 | 475 | T | 2,142,000 |
| 818 | 476 | T | 2,229,500 |
| 819 | 477 | T | 2,604,000 |
| 820 | 478 | T | 2,044,000 |
| 821 | 479 | T | 2,103,500 |
| 822 | 480 | T | 2,096,500 |
| 823 | 481 | T | 231,500 |
| 824 | 482 | T | 2,121,000 |
| 825 | 483 | T | 2,068,500 |
| 826 | 484 | T | 2,419,400 |
| 827 | 485 | T | 2,443,000 |
| 828 | 486 | T | 2,688,000 |
| 829 | 487 | T | 2,079,000 |
| 830 | 488 | T | 2,142,000 |
| 831 | 489 | T | 2,124,500 |
| 832 | 490 | T | 2,047,500 |
| 833 | 491 | T | 2,012,500 |
| 834 | 492 | T | 2,191,000 |
| 835 | 493 | T | 2,187,500 |
| 836 | 494 | T | 2,019,500 |
| 837 | 495 | T | 1,753,500 |
| 838 | 496 | T | 2,073,000 |
| 839 | 497 | T | 2,149,000 |
| 840 | 498 | T | 2,076,400 |
| 841 | 499 | T | 2,068,500 |
| 842 | 500 | T | 6,000,000 |
| 843 | 501 | T | 1,859,500 |
| 844 | 502 | T | 2,135,000 |
| 845 | 503 | T | 2,065,000 |
| 846 | 504 | T | 2,096,500 |
| 847 | 505 | T | 2,481,500 |
| 848 | 506 | T | 1,935,500 |
| 849 | 507 | T | 491,000 |
| 850 | 508 | T | 3,185,000 |
| 851 | 509 | T | 1,869,000 |
| 852 | 510 | T | 16,355,000 |
| 853 | 511 | T | 1,165,500 |
| 854 | 512 | U | 6,000,000 |
| 855 | 513 | U | 2,575,000 |
| 856 | 514 | U | 3,504,400 |
| 857 | 515 | U | 3,739,500 |
| 858 | 516 | U | 2,076,400 |
| 859 | 517 | U | 3,913,000 |
| 860 | 518 | U | 4,781,000 |
| 861 | 519 | U | 5,418,000 |
| 862 | 520 | U | 5,085,500 |
| 863 | 521 | U | 2,500,000 |
| 864 | 522 | U | 3,160,500 |
| 865 | 523 | U | 6,000,000 |
| 866 | 524 | U | 415,000 |
| 867 | 525 | U | 200,000 |
| 868 | 526 | U | 5,890,000 |
| 869 | 527 | U | 5,000,000 |
| 870 | 528 | U | 2,761,500 |
| 871 | 529 | U | 7,000,000 |
| 872 | 530 | U | 10,007,000 |
| 873 | 531 | U | 8,570,000 |
| 874 | 532 | U | 6,990,000 |
| 875 | 533 | U | 7,080,000 |
| 876 | 534 | U | 3,080,000 |
| 877 | 535 | U | 7,600,000 |
| 878 | 536 | U | 5,950,000 |
| 879 | 537 | U | 9,490,000 |
| 880 | 538 | U | 6,920,000 |
| 881 | 539 | U | 6,210,000 |
| 882 | 540 | U | 4,377,000 |
| 883 | 541 | U | 5,130,000 |
| 884 | 542 | U | 5,340,200 |
| 885 | 543 | U | 5,230,000 |
| 886 | 544 | U | 5,780,000 |
| 887 | 545 | U | 4,000,000 |
| 888 | 546 | U | 7,120,000 |
| 889 | 547 | U | 8,890,000 |
| 890 | 548 | U | 8,600,000 |
| 891 | 549 | U | 9,750,000 |
| 892 | 550 | U | 12,840,000 |
| 893 | 551 | U | 3,494,000 |
| 894 | 552 | U | 2,653,000 |
| 895 | 553 | U | 2,513,000 |
| 896 | 554 | U | 2,625,000 |
| 897 | 555 | U | 5,390,000 |
| 898 | 556 | U | 1,841,000 |
| 899 | 557 | U | 1,946,000 |
| 900 | 558 | U | 2,016,000 |
| 901 | 559 | U | 1,795,500 |
| 902 | 560 | U | 1,848,000 |
| 903 | 561 | U | 2,537,500 |
| 904 | 562 | U | 2,068,500 |
| 905 | 563 | U | 2,128,000 |
| 906 | 564 | U | 2,173,500 |
| 907 | 565 | U | 2,128,000 |
| 908 | 566 | U | 2,079,000 |
| 909 | 567 | U | 2,093,000 |
| 910 | 568 | U | 1,935,500 |
| 911 | 569 | U | 1,946,000 |
| 912 | 570 | U | 1,963,500 |
| 913 | 571 | U | 1,753,000 |
| 914 | 572 | U | 30,695,000 |
| 915 | 573 | U | 2,296,000 |
| 916 | 574 | U | 265,000 |
| 917 | 575 | U | 2,100,000 |
| 918 | 576 | U | 2,100,000 |
| 919 | 577 | U | 6,000,000 |
| 920 | 578 | U | 5,000,000 |
| 921 | 579 | U | 6,000,000 |
| 922 | 580 | U | 3,000,000 |
| 923 | 581 | U | 6,000,000 |
| 924 | 582 | U | 2,100,000 |
| 925 | 583 | U | 7,990,000 |
| 926 | 584 | U | 2,590,000 |
| 927 | 585 | U | 2,709,000 |
| 928 | 586 | U | 2,835,000 |
| 929 | 587 | U | 2,229,500 |
| 930 | 588 | U | 2,229,500 |
| 931 | 589 | U | 2,138,500 |
| 932 | 590 | U | 1,750,000 |
| 933 | 591 | U | 1,935,000 |
| 934 | 592 | U | 7,280,000 |
| 935 | 593 | U | 5,970,000 |
| 936 | 594 | U | 5,200,000 |
| 937 | 595 | U | 1,879,500 |
| 938 | 596 | U | 7,720,000 |
| 939 | 597 | U | 5,690,000 |
| 940 | 598 | U | 7,140,000 |
| 941 | 599 | U | 3,139,500 |
| | | **JUMLA: 5,335,010,130** | |

**TAARIFA YA VIWANJA IYUMBU NEW TOWN CENTER**

| NA. | KIWANJA NA. | KITALU |
|---|---|---|
| 1 | 1 | L |
| 2 | 2 | L |
| 3 | 3 | L |
| 4 | 4 | L |
| 5 | 5 | L |
| 6 | 6 | L |
| 7 | 1 | M |
| 8 | 2 | M |
| 9 | 3 | M |
| 10 | 4 | M |
| 11 | 5 | M |
| 12 | 6 | M |
| 13 | 7 | M |
| 14 | 8 | M |
| 15 | 9 | M |
| 16 | 10 | M |
| 17 | 11 | M |
| 18 | 12 | M |
| 19 | 13 | M |
| 20 | 14 | M |
| 21 | 15 | M |
| 22 | 16 | M |
| 23 | 17 | M |
| 24 | 18 | M |
| 25 | 19 | M |
| 26 | 20 | M |
| 27 | 21 | M |
| 28 | 22 | M |
| 29 | 23 | M |
| 30 | 24 | M |
| 31 | 25 | M |
| 32 | 26 | M |
| 33 | 1 | N |
| 34 | 2 | N |
| 35 | 3 | N |
| 36 | 4 | N |
| 37 | 5 | N |
| 38 | 6 | N |
| 39 | 7 | N |
| 40 | 8 | N |
| 41 | 9 | N |
| 42 | 10 | N |
| 43 | 11 | N |
| 44 | 12 | N |
| 45 | 13 | N |
| 46 | 14 | N |
| 47 | 15 | N |
| 48 | 16 | N |
| 49 | 17 | N |
| 50 | 18 | N |
| 51 | 1 | P |
| 52 | 2 | P |
| 53 | 3 | P |
| 54 | 4 | P |
| 55 | 5 | P |
| 56 | 6 | P |
| 57 | 7 | P |
| 58 | 8 | P |
| 59 | 9 | P |
| 60 | 10 | P |
| 61 | 11 | P |
| 62 | 12 | P |
| 63 | 13 | P |
| 64 | 14 | P |
| 65 | 15 | P |
| 66 | 16 | P |
| 67 | 17 | P |
| 68 | 18 | P |
| 69 | 19 | P |
| 70 | 20 | P |
| 71 | 21 | P |
| 72 | 22 | P |
| 73 | 23 | P |
| 74 | 24 | P |
| 75 | 25 | P |
| 76 | 26 | P |
| 77 | 27 | P |
| 78 | 28 | P |
| 79 | 29 | P |
| 80 | 30 | P |
| 81 | 31 | P |
| 82 | 32 | P |
| 83 | 33 | P |
| 84 | 34 | P |
| 85 | 35 | P |
| 86 | 36 | P |
| 87 | 37 | P |
| 88 | 38 | P |
| 89 | 39 | P |
| 90 | 40 | P |
| 91 | 41 | P |
| 92 | 1 | Q |
| 93 | 2 | Q |
| 94 | 3 | Q |
| 95 | 4 | Q |
| 96 | 5 | Q |
| 97 | 6 | Q |
| 98 | 7 | Q |
| 99 | 8 | Q |
| 100 | 9 | Q |
| 101 | 10 | Q |
| 102 | 11 | Q |
| 103 | 12 | Q |
| 104 | 13 | Q |
| 105 | 14 | Q |
| 106 | 15 | Q |
| 107 | 16 | Q |
| 108 | 17 | Q |
| 109 | 18 | Q |
| 110 | 19 | Q |
| 111 | 20 | Q |
| 112 | 21 | Q |
| 113 | 22 | Q |
| 114 | 23 | Q |
| 115 | 24 | Q |
| 116 | 25 | Q |
| 117 | 26 | Q |
| 118 | 27 | Q |
| 119 | 28 | Q |
| 120 | 29 | Q |
| 121 | 2 | R |
| 122 | 3 | R |
| 123 | 4 | R |
| 124 | 5 | R |
| 125 | 6 | R |
| 126 | 7 | R |
| 127 | 8 | R |
| 128 | 9 | R |
| 129 | 10 | R |
| 130 | 11 | R |
| 131 | 12 | R |
| 132 | 13 | R |
| 133 | 14 | R |
| 134 | 15 | R |
| 135 | 16 | R |

# Ataka masharti yalegezwe kupata makamishna madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Utumishi na Utawala Bora imeombwa kulegeza vigezo vya kuwapata makamishna wa Tume ya Madini ili kuziba pengo la uhaba uliopo.

Vigezo vya sasa vinavyotakiwa ili kuajiriwa makamishna hao ni lazima wawe na shahada ya uzamili.

Ombi hilo lilitolewa jana na Waziri wa Madini, Doto Biteko, kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, George Mkuchika, katika mafunzo ya watendaji wa Wizara ya Madini na taasisi zake jijini hapa.

Biteko alimwomba Waziri Mkuchika kupunguza masharti na vigezo hivyo vya kuwa na shahada ya uzamili ili kuziba pengo la watumishi katika tume hiyo.

"Kada hii ni muhimu katika sekta ya madini katika kuhudumia masoko na kudhibiti utoroshaji wa madini kwani tayari wamefanyiwa 'vetting' wapo vizuri na hawana shida yeyote tatizo ni hilo la kigezo cha elimu," alisema.

Aidha, alibainisha kuwa tume inakabiliwa na uhaba wa watumishi 220 wakati mahitaji ni kuwa na watumishi 637, lakini waliopo ni watumishi 417.

"Hawa waliopo ni wale waliohamishwa kutoka taasisi zinazolandana, hivyo tume hii ina upungufu wa wafanyakazi 220," alisema.

Alisema pia wizara hiyo ina uhaba wa watumishi 61, wakiwamo watano wa kuteuliwa na 56 wa kuajiriwa.

"Tunaomba kibali cha kuajiri watumishi ili kufikia lengo wizara hiyo imepewa katika kukusanya mapato ya serikali," alisema.




Wateja wa benki ya DTB-Tanzania jijini Tanga, wakipata futari iliyoandaliwa na benki hiyo juzi. Zaidi ya wateja 300, wakiongozwa na Sheikh wa mkoa huo, Alhaji Juma Luwuchu, walihudhuria. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa ataka kasi ya majadiliano AKDN, NHIF

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameutaka uongozi wa Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN) ukamilishe majadiliano yao na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuhusu matumizi ya kadi za NHIF kwenye hospitali zao, ili Watanzania wengi zaidi waweze kunufaika.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokutana na viongozi kadhaa wa taasisi hiyo pamoja na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ofisini kwake bungeni jijini Dodoma.

Waziri Mkuu alisema serikali inatambua mchango unaotolewa na taasisi ya AKDN katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya.

"Nilijionea kazi kubwa inayofanyika pale Hospitali ya Aga Khan, Machi, mwaka huu, niliongea na wagonjwa na kupata maoni yao, lakini kikubwa tu mpunguze gharama na muimarishe huduma zenu," alisema.

Aliwapongeza viongozi hao kwa utoaji wao wa huduma kwenye sekta nyingine kama elimu, maji na kilimo. "Tunategemea mtaendelea kuimarisha huduma hizo ili ziwasaidie Watanzania wengi zaidi," alisisitiza.

Kwa upande wake, Waziri Ummy Mwalimu alimweleza Waziri Mkuu kwamba hospitali za Ocean Road na Bugando zinatoa huduma za radiotherapy na chemotherapy, wakati hospitali ya KCMC inatoa huduma ya chemotherapy tu.

"Hospitali ya Rufani ya Mbeya bado huduma hizo zinaandaliwa ili ziweze kutolewa," alisema.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI,** Tunahitaji Fundi wa COMPUTER na CCTV CAMERA Awe na Uzoefu wa mwaka mmoja Awe na Diploma. Mawasiliano: 0713 164462/ 2110836


***NIPASHE***
***NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



115250802

**Kagenzi Ngaro** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba P0942-0011** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2001 katika shule ya Sekondari Rumanyika. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa : **DAR/MBA/RB/30204/2019**

## KUPOTEA KWA CHETI



115250502

**Johari Francis Ruoma** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2762-0037 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika shule ya Sekondari Halisi. Cheti hicho kilipotelea Gongolamboto Majohe, Dar es Salaam

**yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**STK/RB/3840/2019**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HALIDI IDDI MADUKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya GUTA aina ya sky mark yenye RANGI ya blue namba za usajili **MC727 ALR.** Chassis namba **BZINEF11K14X00114** Engine na. **BZ1N163FMLE000114** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/26543/2019.**

115251302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo **DODOMA MJINI**
Usimamizi wa mirathi 35/2019

Ombi la **JOYCE PASCAL** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu **MWANAULU HASSAN**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 30/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

Tarehe 28/5/2019

115251402

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.29 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late FARAJA TAMSON SIMBOWE**
**of NDOGOYE area within Dodoma Region.**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by**
1. **Tamson Patison Simbowe............1st Applicant**
2. **Josephath Gasiba...................2nd Applicant**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before 29th /05/2019.

Dated at Dodoma this ....21 /03/2019

115251502

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HALIDI IDDI MADUKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SUNLG yenye namba za usajili **MC131 AVB.** Chassis namba **LFFWUOIC4AZL11969** Engine na. **156FMIAB2282065** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/26481/2019.**

115251302

## KUPOTEA KWA KADI

**PETRO SAMSON** MKAZI WA WILAYA YA ITILIMA MKOANI SIMIYU ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI AINA YA **SUNLG** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 436 BFQ,** AMBAPO KADI HIYO ILIPOTEA WILAYANI ITILIMA. NAOMBA KWA YOYOTE ATAKAEIOKOTA AIWASILISHE KATIKA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI MKOANI SIMIYU
Polisi Taarifa: **ITL/RB/65/2018**

115251002

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Joseph Gerema Mashebo** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SANLG yenye namba za usajili **T463 CRN.**

Yoyote atakayeiona atoe Taarifa kituo cha polisi

Taarifa ya polisi
**KHM/RB/2223/2018**

215250302

**IN THE REGIONAL COIRT FOR ZANZIBAR**
**HOLDED AT VUGA**
**CIVIL CASE NO. 07 YA 2016**
**KHALID MAMBO MUSSA**

**ABDILLAH MAISARA ABDALLAH..........PLAINTIFF**
**Versus**
**PILI LASSIM..........................................DEFENDANT**

**TANGAZO**

Mahkama ya Mkoa Vuga, Zanzibar inataka umtangazie Mdaiwa PILI KASSIM popote alipo ahudhurie mbele ya Mahkama siku ya Jumatano ya tarehe 29 ya mwezi wa Mei, 2019 kuja kusikiliza ombi lililofunguliwa dhidi yake na Mdai, asipofika Mahkamani, Mahkama itasikiliza kesi upande mmoja na kutoa maamuzi.

**Imetiwa sahihi na Mhuri wa Mahkama hii leo tarehe 16 Mei, 2019**

215250702


KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

***0767 223311***

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# KANE: NIPO TAYARI KUIVAA LIVERPOOL

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI na nahodha wa klabu ya Tottenham, Harry Kane, amesema yupo tayari kuivaa Liverpool kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumamosi.

Kane, 25, alipata majeraha makubwa ya kifundo cha mguu baada ya kuteleza na kuanguka kwenye mchezo wa robo fainali ya kombe hilo dhidi ya Manchester City Aprili 9, mwaka huu.

Kocha wa Spurs, Mauricio Pochettino awali alisema nahodha huyo wa England angelikuwa nje ya uwanja kwa mechi zote zilizosalia.

"Najisikia vema sana sasa. Sina shida tena," alisema Kane.

"Nilianza kurudi kwenye kikosi tangu mwishoni mwa wiki iliyopita. Wiki hii narejesha nguvu na ukakamavu wa mwili kwa kadri ya uwezo wangu," alisema.

"Baada ya hapo itakuwa juu ya kocha kuamua. Yeye ndiye atafanya tathmini yake na kufanya maamuzi ya kunijumuisha kikosini ama la. Lakini mpaka sasa mimi najisikia vizuri na nipo tayari kwa mchezo.

Kane ameifungia Tottenham mabao 24 msimu huu kwenye michuano yote licha ya kuwa nje ya uwanja kwa wiki sita kati ya Januari na Februari baada ya kuumia kifundo cha mguu huo huo alioumia mwezi uliopita.

Kuhusu uwezekano wa Kane kucheza, Pochettino amesema : "Siwezi sema kuwa yupo sawa kwa 100%, ama iwapo atakuwa kwenye orodha ya wachezaji wa akiba ama la. Lakini tuna furaha kuona anapona kwa kasi."

"Ni jambo la muhimu sana kwake kuona kama anajisikia nafuu. Mimi naombea heri zaidi. Tuna wiki moja zaidi ya kuendelea kufuatilia maendeleo yake.

Kocha huyo amesema japo Keane ni mtu muhimu, lakini wanaelekeza nguvu yote kwenye timu kwa ujumla.

"Mpira ni mchezo unaohusisha timu nzima, umoja na imani thabiti. Tazama namna ambavyo tumefika fainali. Pale Harry (Kane) alipoumia kwenye robo fainali, nini kilitokea," alisema Pochettino.

"Hilo halimaanishi kwamba yeye si moja ya wachezaji bora wa kikosi chetu. Kwangu yeye ni moja ya washambuliaji mahiri kabisa duniani - yupo kwenye tatu bora.

"Inatubidi tuwafunge Liverpool na kama atakuwapo, litakuwa jambo jema zaidi."

## Conte bora kuliko Mourinho - Pirlo

**MILAN,** Italia

ANDREA Pirlo anaamini Antonio Conte anaweza kuipa mengi zaidi Inter Milan kuliko Jose Mourinho, huku uvumi ukienea kwamba kocha huyo wa zamani wa Chelsea anapanga kumrithi Luciano Spalletti.

Conte ameripotiwa kwamba anatarajiwa kuichukua mikoba pale Inter, licha ya Spalletti kuiwezesha Inter kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kumaliza nafasi ya nne msimu huu kwenye msimamo wa ligi.

Kocha wa zamani wa Inter, Mourinho alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi katika klabu hiyo, hata hivyo, Pirlo - ambaye alicheza chini ya Conte pale Juventus anaamini bosi huyo wa zamani wa Italia ni bora zaidi kwa Nerazzurri.

"Kwa maoni yangu, Conte ni bora zaidi ya Mourinho, hasa ikizingatiwa kwamba analifahamu soka la Italia vizuri," alisema Pirlo akiiambia Sky Sport Italia.

"Kama akijiunga na Inter mashabiki wataipa sapoti timu, zaidi atakuwa karibu zaidi na wachezaji."

Mazungumzo kuhusu ujio wa Conte hapo Inter pia yamehusishwa na mpango wa kusajiliwa kwa Romelu Lukaku kutoka Manchester United, ambako Mourinho alifukuzwa Desemba mwaka jana.



## Alves kuvaa kitamba cha Neymar Copa America



**SAO PAULO**

NEYMAR hatakuwa nahodha wa Brazil kwenye michuano ya Copa America, huku Dani Alves akiwa amepewa kitambaa kwa ajili ya kuongoza michuano hiyo ya Mataifa ya Amerika Kusini.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain, Neymar alitajwa kuwa nahodha wa kudumu wa Brazil na kocha Tite Septemba mwaka 2018, hata hivyo nafasi yake sasa imechukuliwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36.

Katika taarifa iliyotolewa Jumatatu, Shirikisho la Soka la Brazil (CBF), lilisema: "Maamuzi yalifanywa baada ya Neymar kuwasiliana na Tite Jumamosi."

Tangazo hilo limekuwa siku chache baada ya kocha wa klabu yake ya PSG, Thomas Tuchel kuondoa uwezekano wa mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona kuwa nahodha. Neymar ambaye alifunga mabao 23 katika mashindano yote msimu huu baada ya kupona goti anatarajia kukosa mechi tatu baada ya fujo zake kwenye mchezo wa fainali ya Kombe la Ufaransa dhidi ya Rennes wiki iliyopita.

## HABARI MICHEZO

# Rais Madrid athibitisha Ramos kutaka kuondoka

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez amebainisha kwamba, Sergio Ramos ameomba kuruhusiwa kuondoka kipindi cha majira ya joto na kwenda kwenye klabu moja ya China.

Akizungumza na Gazeti la Marca, Perez amethibitisha uvumi kwamba nahodha huyo wa Real alikuwa na ofa mezani.

Alinukuliwa akisema: "Hakuna kilichotokea. Watu wake wameniambia kwamba amepata ofa nzuri zaidi kutoka nchini China, lakini hawawezi kutoa ada ya uhamisho kwa sababu kuna sheria zinawataka kulipa mara mbili.

"Yeye mwenyewe amesema kwamba anataka kuondoka baada ya kukaa na sisi kwa muda wa miaka 11, na mimi sikuwa na tatizo lolote juu ya hilo, ingawa uwezekano wa kwenda China ni mdogo zaidi kwake na pengine anaweza kwenda sehemu nyingine."

Ramos amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Klabu ya Manchester United ya England, huku pia miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, PSG ikiwa imetia mkono kutaka kuwania saini yake.

Nahodha huyo wa timu ya Taifa ya Hispania amekuwa na klabu hiyo kwa kipindi cha miaka 11 na sasa anataka kuondoka kwenye klabu hiyo kwa ajili ya kutafuta changamoto mpya.

Hata hivyo, kocha wa Klabu ya Real Madrid, Zinedine Zidane, amebainisha kwamba, Ramos bado yupo kwenye mipango yake na kwamba anataka kuendelea kuwapo katika kikosi hicho ambacho kwa sasa kinajengwa upya baada ya kushindwa kutwaa taji lolote msimu huu.






# BARCELONA KUMTEUA MARTINEZ KUWA MRITHI WA VALVERDE

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inaweza kumteua kocha wa zamani wa Wigan Athletic na Everton, Roberto Martinez kama kocha wao ajae, huku Ernesto Valverde akitarajiwa kujulishwa kwamba hataendelea kuwa kocha wao msimu ujao.

Valverde, ambaye Februari alisaini kuongeza mkataba wake hadi mwishoni mwa msimu ujao, hivi karibuni aliwapa ubingwa wa La Liga.

Hata hivyo, Barca ilipoteza kwenye fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] dhidi ya Valencia na ikatolewa kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya kuongoza kwa mabao 3-0 kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kikosi cha Valverde kilijikuta kikikubali kichapo cha mabao 4-0 kwenye mchezo wa pili pale Anfield na kutolewa mashindanoni.

Ilivumishwa kwamba kocha huyo mwenye umri wa miaka 55, angeweza kuendelea kuwa kocha wa kikosi hicho hapo Camp Nou.

Mwandishi, Jota Jordi, akizungumza na Gazeti la El Chiringuito akinukuliwa na Sky Sports, amedai kwamba bodi ya Barca imefanya uamuzi juu ya majaliwa ya Valverde baada ya kushindwa kwenye Kombe la Mfalme kutoka kwa Valencia, huku Martinez sasa akitarajiwa kupewa timu.

RACI, imebainisha kwamba, Martinez atateuliwa kuwa kocha mpya wa Barca wakati wowote kuanzia sasa.

# Gattuso ajiuzulu ukocha AC Milan

**MILAN,** Italia

GENNARO Gattuso amejiuzulu kama kocha wa AC Milan, baada ya kushindwa kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa pointi moja.

Mkurugenzi wa michezo wa Milan, Leonardo anayetarajiwa kufuata nyayo za Gattuso kujiuzulu, huku Ofisa Mtendaji, Ivan Gazidis akitaka kuimarisha timu hiyo.

Gattuso ameliambia Gazeti la La Repubblica kwamba ataondoka klabuni hapo baada ya kushindwa kutimiza kile alichokipanga.

"Maamuzi ya kuondoka benchi la Milan hayakuwa rahisi. Lakini ni maamuzi ambayo nimelazimika kuyachukua. "Haikuwa kitu rahisi, lakini nimelazimika kuondoka na nimekaa hapa kwa zaidi ya miezi 18 na sasa nakaa."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD KUAGA CHELSEA KWA UBINGWA EUROPA

**Ninataka kutwaa kombe tu, haijalishi endapo nitafunga ama la, kama ni mechi yangu ya mwisho...**

**BAKU,** Azerbaijan

EDEN Hazard amesema ushindi kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Europa League dhidi ya Arsenal leo utakuwa "kumtakia mema sahihi" kwa Chelsea kama ataondoka klabuni hapo majira haya ya joto.

**Hazard aliweka wazi kuwa mwishoni mwa msimu alifanya uamuzi kuhusu mustakabali wake wa baadaye na anatarajia utapatiwa ufumbuzi kufuatia fainali hiyo jijini Baku.**

Hata hivyo, Sky Sports inatambua kwamba Chelsea inataka pauni milioni 130 ili kumwachia Hazard, lakini Real Madrid ambayo inaamini itamsajili - inamthaminisha Mbelgiji huyo na euro milioni 100 sawa na pauni milioni 88 kutokana na ukweli kwamba anaingia mwaka wa mwisho katika mkataba wake hapo Stamford Bridge.

Hazard amesisitiza hakuna lolote ambalo limeshakamilika kuhusu mustakabli wake wa baadaye, lakini anapania kuinua kombe jijini Baku kutawezesha kuagwa.

"Ni mashindano ya Ulaya, hivyo kwangu mimi, kwa klabu, kwa kocha, kwa mashabiki, ni kitu fulani muhimu," alisema. "Wakati unapocheza fainali, haijalishi endapo ni Ligi ya Mabingwa, Europa League ama Kombe la Ligi, unataka tu kushinda, unataka tu kuleta kombe nyumbani na kushangilia hilo.

"Wakati unapoichezea Chelsea mwanzoni mwa msimu, watu wanafikiri ni kombe gani tunaweza kuwa nalo mwishoni mwa Mei, hivyo hili moja ni mojawapo muhimu.

"Tumepoteza mechi ya fainali ya Kombe la Ligi, hivyo mwishoni mwa msimu hili ni kombe tunaloweza kwenda nalo. "Ninataka kutwaa kombe tu, hivyo ndivyo ilivyo. Haijalishi endapo nitafunga ama la. Kama ni mechi yangu ya mwisho, ninatumai kuleta kombe.

Akisajiliwa kutokea Lille kwa pauni milioni 32 mwaka 2012, Hazard amefunga mabao 108 katika mechi 351 alizoichezea Chelsea, akitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mara mbili, Kombe la FA, Europa League na Kombe la Ligi.

Alitangazwa kuwa Mchezaji Bora wa Mwaka wa Kulipwa, kitu anachokiona kwamba ulikuwa ni msimu bora kwake, wakati wakitwaa ubingwa chini ya Jose Mourinho msimu wa 2014/15. Hata hivyo, Hazard amesema hataweza kuchezea klabu nyingine ya England endapo dili hilo litashindikana.

"Hakuna nafasi hiyo, hakuna nafasi. Mimi ni Bluu! Inamaana kubwa," alisema. "Siwezi kuichezea klabu nyingine katika nchini hii."Mshambuliaji wa Chelsea, Willian alisema itakuwa 'huzuni sana' kuona Eden Hazard akiondoka klabuni hapo majira haya ya joto.

"Itakuwa kumtakia mafanikio sahihi huko aendako, ndiyo."

Cesar Azpilicueta amesema Chelsea imeweka 'mtazamo' na 'kujituma sana' kuelekea mechi hiyo ya fainali ya Europa League jijini Baku leo.

## ZISIKUPITE

### RAMOS ALILIA KWENDA CHINA

BEKI Mhispania Sergio Ramos, 33, amemuomba Rais wa Real Madrid, Florentino Perez amruhusu aondoke kwenda kucheza soka China. ***(LaSexta - in Spanish)***

### DE LIGT AIKANA UNITED

BEKI wa Ajax, Mholanzi Matthijs de Ligt, 19, amesema taarifa zinazomhusisha na kujiunga na Manchester United majira haya ya joto "zinatiwa chumvi". ***(Fox Sports)***

### YAMTAKA DONNARUMMA

Arsenal imefanya mawasiliano na kipa wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma, 20. ***(Tutto Mercato Web via Star)***

### NEYMAR KUITOBOA MADRID

Real Madrid italazimika kumlipa mshambuliaji wa Paris St-Germain, Mbrazil Neymar, 27, pauni milioni 1.2 kwa wiki ili kuweza kumhamishia hapo Bernabeu. ***(AS via Mail)***

### SARRI, JUVE WAKUBALIANA

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri amekubaliana malipo binafsi na Juventus ambapo atakuwa akilipwa ongezeko la pauni milioni 1.2 kwa mwaka . ***(Mail)***

### MARTINEZ KUMRITHI VALVERDE

KOCHA wa Ubelgiji, Roberto Martinez ni chaguo la kwanza kwa Barcelona endapo Ernesto Valverde hataendelea na kazi hiyo. ***(RAC 1 - in Spanish)***

### EMERY, ALLEGRI WATAZAMWA

KOCHA wa Uholanzi, Ronald Koeman, kocha wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri na wa Arsenal, Unai Emery ni miongoni wa wanaopewa nafasi ya kurithi mikoba ya Ernesto Valverde hapo Barcelona. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### MALCOM ANUKIA KUSEPA

WINGA wa Barcelona, Malcom, 22, anaweza kuwa njiani kuondoka ikiwa ni miezi 12 tangu aliposaini mkataba na miamba hao wa Catalunya akitokea Bordeaux. Mbrazil huyo alikuwa akihusishwa na kujiunga na Tottenham pamoja na Everton katika dirisha la Januari, ***(Sport via Star)***

### DYBALA ANOGEWA JUVENTUS

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Muargentina Paulo Dybala, 25, amethibitisha kwamba anataka kubaki kuwatumikia mabingwa hao wa Serie A msimu ujao, licha ya kuhusishwa na kujiunga na Manchester United. ***(Independent)***

### PEREZ AJIAMINI KWA HAZARD

Rais wa Real Madrid, Florentino Perez ameiambia Redio ya Hispania "anatumai" kiungo wa Chelsea, Eden Hazard, 28, atasaini mkataba wa kuichezea klabu hiyo ya La Liga majira haya ya joto. ***(Mail)***

### JOVIC AITAMANI EPL, SERIE A

STRAIKA wa Eintracht Frankfurt, Mserbia Luka Jovic, 21, anaamini Ligi Kuu England ama Serie A kutakuwa sehemu sahihi kwake wakati huu akifikiria kuondoka. ***(Die Welt via Mirror)***

## Straika, mabeki kuipeleka Polisi Zanzibar sokoni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya Polisi ya Zanzibar, Nassor Salum, amesema kufanya vibaya kwa timu hiyo msimu uliopita kumetokana na kuwapo kwa mapungufu katika safu yake ya ushambuliaji ambayo sasa wataingia sokoni kuiimarisha kwa ajili ya msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili wiki hii, kocha huyo alisema kuna nafasi nyingi katika timu hiyo wachezaji wake walipwaya husus an washambuliaji pamoja na viungo wa kati, beki wa kulia pamoja na kushoto.

Alisema licha ya mapungufu hayo, lakini timu hiyo ilijitahidi kupambana na kuhakikisha haishuki daraja licha ya mara kwa mara kutopata matokeo mazuri hususan wanalishuka katika viwanja kisiwani Unguja.

"Tulianza vibaya, na mzunguko wa pili tulijitahidi kupambana hadi tukafanikiwa kuinusuru timu kutoshuka daraja, licha ya mapungufu ambayo yapo katika timu, lakini wachezaji waliweza kujituma kwa kiasi kikubwa," alisema.

Aidha, alisema timu hiyo inahitaji kufanya usajili mzuri utakaoiwezesha kufanya vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar ambayo klabu nyingi zinazoshiriki ligi hiyo zina wachezaji wazuri na wenye ushindani wa kweli.

Alisema kama mwalimu, yeye tayari ameshapeleka ombi juu ya idadi na nafasi anazotaka kuzisajili ikiwamo washambuliaji wawili, kiungo mmoja, beki wa kulia na wa kushoto pamoja na mlinzi mmoja.

## MRFA wafunguka uchaguzi wilayani

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

CHAMA cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), kimezitaka wilaya zake kuhakikisha zinafanya uchaguzi kabla ya Septemba mwaka huu, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa MRFA, Charles Mwakambaya, alisema tayari vyama vyote vya wilaya vimepewa barua za kuhakikisha wanakamilisha mchakato huo ili kuruhusu maandalizi ya uchaguzi ya mkoa yanaanza mapema.

Mwakambaya alisema wanahitaji kuona wilaya zote zinafanya uchaguzi kwa kufuata maelekezo ili waweze kupata viongozi watakaokuwa na nia ya kuendeleza soka mkoani hapa.

"Tumeshatuma taarifa rasmi katika wilaya zetu zote saba, na tayari wameanza mchakato kuhusu dokezo tulilowapatia, hatutakuwa kimya kwa wilaya ambayo itakwenda kinyume na maelekezo haya, wakimaliza wao na mkoa utaanza mara moja mchakato wake wa kupata viongozi wapya," alisema Mwakambaya.

Alizitaja wilaya za mkoa huo ambazo zinatoa wajumbe watakaoshiriki katika mkutano mkuu wa MRFA kuwa ni Morogoro Mjini, Kilosa, Mvomero, Gairo, Kilombero, Ulanga na Malinyi.

# NDEMLA AZISUBIRISHA KWANZA SIMBA, YANGA

**Na Somoe Ng'itu,** MOROGORO

KIUNGO wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Said Ndemla amesema hana haraka ya kusaini mkataba na klabu yoyote ya hapa nchini kwa sababu anaamini mazungumzo na timu mojawapo ya Ulaya yanaweza kukamilika na kwenda kuanza maisha mapya.

**Ndemla amemaliza mkataba wake na Simba na kwa muda mrefu amekuwa akiwindwa na watani zao, Yanga kwa sababu kiungo huyo amekosa namba katika kikosi cha kwanza cha mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Akizungumza na gazeti hili mjini hapa jana, Ndemla alisema kuwa mbali na kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara, pia anahitaji kupata timu itakayomlipa vizuri kulingana na thamani yake uwanjani.

Kiungo huyo aliyeanzia soka katika timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (Simba B), alisema anaamini ana kiwango kizuri na ana uwezo wa kupangwa katika kikosi cha kwanza jambo ambalo kwa sasa halipati.

"Bado sijasaini, sitaki kusaini Simba mapema hii, najipanga kwanza kuangalia kama mchakato wangu wa kupata dili la kucheza nje ya nchi utakamilika, kama nitakwama basi nitakuwa tayari kusaini hata Yanga au kuongeza mkataba Simba kama watakuwa bado wanahitaji huduma yangu," alisema Ndemla.

Aliongeza kuwa maneno ambayo yamekuwa yakizungumzwa juu yake si ya kweli na anasema utulivu alionao utamsaidia kufanya uamuzi sahihi wa wapi atakwenda.

Hata hivyo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alipoulizwa kuhusu mazungumzo ya kumpa mkataba kiungo huyo yamefikia wapi, alisema kuwa bado Ndemla ni mchezaji wa Simba na hawana wasiwasi juu ya kumkosa katika msimu ujao.

Manara alisema wachezaji wengi wa Tanzania kwa sasa wanahitaji kusajiliwa na Simba kutokana na mafanikio waliyopata na itashangaza kama Ndemla ataondoka klabu hiyo ambayo msimu huu ilifika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa vipindi viwili tofauti, uongozi wa Simba ulimruhusu Ndemla kwenda kufanya majaribio katika klabu moja ya Ligi Daraja la Kwanza nchini Sweden.



Balozi wa Castle Lager Africa 5s, Ivo Mapunda (mbele), akizungumza na wachezaji wa timu ya Four Ways FC ya Kinondoni na Girls Queens ya Msimbazi Kariakoo zinazowakilisha nchi kwenye fainali za mashindano ya Castle Africa 5s, wakati wa uzinduzi wa Kambi maalumu ya maandalizi ya mashindano hayo yanayotarajiwa kufanyika nchini Juni 7- 8, mwaka huu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Four Ways, Girls Queens kambini kujiandaa na Castle Africa 5s 2019*

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Four Ways Park FC yenye makazi yake Kinondoni na Girls Queens ya Msimbazi Kariakoo, zote za jijini Dar es Salaam zimeingia kambini rasmi jana kujiandaa na mashindano ya Castle Africa 5s (5 - aside) yanayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Juni 7-8, mwaka huu, katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Balozi wa Castle Lager Africa nchini Tanzania, Ivo Mapunda alisema timu zote ziko vizuri tayari kwa kuwakilisha Watanzania katika fainali za kimataifa na ushindi ni lazima kulingana na maandalizi waliyonayo na watakayoendelea nayo.

"Mwaka huu Tanzania itawakilishwa na timu ya wanaume ya Four Ways ya Kinondoni na ya wanawake ya Girls Queens ya Msimbazi Kariakoo kwa ujumla timu zote ziko sawa na zipo tayari kwa fainali hizo na leo (jana) rasmi sasa zimeingia kambini kujiandaa na fainali hizo," alisema Mapunda.

Naye Meneja wa Bia ya Castle Lager, Pamela Kikuli, alizitaji nchi zinazotarajiwa kushiriki mashindano hayo ya Africa 5s mbali na wenyeji Tanzania kuwa ni Africa Kusini, Zambia, Zimbabwe, Swaziland, Lethoto, Uganda na nchi alikwa ya Nigeria.

Kikuli alisema nchi hizo zikiwakilishwa na timu ya wanaume na wanawake zinatarajiwa kuwasili nchini Juni 5, mwaka huu tayari kwa fainali hizo za Castle Africa 5s.

"Juni 6, mwaka huu timu zitakabidhiwa vifaa vya michezo katika Hoteli ya Lamada jijini Dar es Saalaam tayari kwa kuanza mashindano rasmi Juni 7 hadi 8.

"Tunawaomba Watanzania wapenda michezo wajitokeze kuja kuzishangilia timu zao zinazowakilisha nchi katika fainali hizo za Castle Africa 5s," alisema Kikuli.

Mwisho Kikuli alisema fainali hizo zinatarajiwa kuhudhuriwa na Balozi wa Castle Africa 5s, Samwel Eto'o hivyo akawataka mashabiki wa soka kujitokeza kwa wingi kuja kumshuhudia mchezaji huyo mkongwe pamoja na kupiga naye picha.

Wawakilishi hao wa Tanzania kwa upande wa timu ya wanawake na wanaume, walipata nafasi hiyo kufuatia kuibuka washindi katika bonanza kubwa la soka lililofanyika hivi karibuni katika viwanja vya Posta Kijitonyama kwa udhamini wa Kampuni ya Bia nchini (TBL) kupitia bia yake ya Castle Lager na kuzawadiwa kikombe, medali za dhahabu, pesa taslimu Sh. 1,500,000, Caton ya bia ya Castle Lager.

# Michezo

Jumatano Mei 29, 2019

Nipashe




Hazard kuaga Chelsea kwa ubingwa Europa UKURASA 30



Wachezaji wa Simba wakisherehekea ubingwa wao baada ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, kumkabidhi kombe nahodha msaidizi wa klabu hiyo, Mohammed Hussein 'Tshabalala' katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro jana. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 38 | 29 | 6 | 3 | 77 | 15 | 93 |
| 2. Yanga | 38 | 27 | 5 | 6 | 56 | 27 | 86 |
| 3. Azam | 38 | 21 | 12 | 5 | 54 | 21 | 75 |
| 4. Kinondoni MC | 38 | 13 | 16 | 9 | 40 | 25 | 55 |
| 5. Mtibwa Sugar | 38 | 14 | 8 | 16 | 36 | 34 | 50 |
| 6. Lipuli | 38 | 12 | 13 | 13 | 32 | 40 | 49 |
| 7. Mbeya City | 38 | 13 | 9 | 16 | 38 | 39 | 48 |
| 8. Coastal Union | 38 | 11 | 15 | 12 | 32 | 42 | 48 |
| 9. Ndanda | 38 | 12 | 12 | 14 | 25 | 37 | 48 |
| 10. JKT Tanzania | 38 | 11 | 14 | 13 | 28 | 34 | 47 |
| 11. Alliance | 38 | 12 | 11 | 15 | 33 | 42 | 47 |
| 12. TZ Prisons | 38 | 11 | 13 | 14 | 30 | 31 | 46 |
| 13. Singida United | 38 | 11 | 13 | 14 | 30 | 39 | 46 |
| 14. Biashara United | 38 | 11 | 12 | 15 | 30 | 35 | 45 |
| 15. Ruvu Shooting | 38 | 11 | 12 | 15 | 35 | 43 | 45 |
| 16. Mbao | 38 | 11 | 12 | 15 | 27 | 41 | 45 |
| 17. Mwadui | 38 | 12 | 8 | 18 | 47 | 52 | 44 |
| 18. Kagera Sugar | 38 | 10 | 14 | 14 | 33 | 43 | 44 |
| 19. Stand United | 38 | 12 | 8 | 18 | 38 | 50 | 44 |
| 20. African Lyon | 38 | 4 | 11 | 23 | 23 | 54 | 23 |

# Simba wanacheeeka

## Kagera Sugar, African Lyon zashuka daraja, Stand United, Mwadui zasubiri mchujo kujua...

**Na Somoe Ng'itu**, MOROGORO

WAKATI mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wakifunga msimu wa 2018/19 kwa kicheko baada ya kuutwaa ubingwa, huku wakilazimishwa sare ya bila kufungana na Mtibwa Sugar katika mechi ya kufunga pazia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani hapa, kwingineko Stand United imeungana na African Lyon kushuka daraja rasmi, wakati Mwadui FC na Kagera Sugar zenyewe zikisubiri mechi ya mchujo dhidi ya timu za Ligi Daraja la kwanza kujua hatima yao Ligi Kuu msimu ujao.

**Kwa matokeo hayo, Simba imemaliza msimu ikiwa na pointi 93 wakati wenyeji Mtibwa Sugar ambao walipokea kichapo cha mabao 3-0 katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wamefikisha pointi 50.**

Baada ya mchezo huo uliochezeshwa na refa, Emmanuel Mwandembwa kutoka jijini Mbeya kumalizika, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola akiongozana na Rais wa Shirikisho la Soka Tanzani (TFF), Wallace Karia waliwakabidhi Simba kombe la ubingwa sambamba na medali.

Mabeki wa Mtibwa Sugar jana walionekana kuwa makini zaidi na kuokoa mashambulizi huku wakifanikiwa kumdhibiti kinara wa kupachika mabao straika Meddie Kagere, huku pia jana ikimchezesha kipa Benedict Tinoco badala ya Shabani Kado ambaye alidaka katika mechi iliyopita.

Simba ndio ilikuwa ya kwanza kufanya shambulizi, lakini kipa wa Mtibwa Sugar, Tinocco alifanikiwa kuwahi na kutoa nje mpira uliopigwa wa kushtukiza na Clatous Chama dakika ya kwanza.

Dakika ya 13 mabingwa hao watetezi waliendelea kulishambulia lango la Mtibwa Sugar, lakini krosi iliyopigwa na Zana Koulibaly aliyepewa mpira na Chama ilikosa mtu wa kuunganisha na kutoka nje huku wenyeji wakijibu shambulio hilo, lakini mshambuliaji wake Salum Kihimbwa akiwa katika nafasi nzuri alipaisha juu dakika ya 18.

Kiungo Mzambia Chama alipoteza nafasi nyingine ya kufunga baada ya kupiga juu mpira na kupoteza pasi nzuri aliyopenyezewa na Hassan Dilunga dakika ya 21, huku Jaffer Kibaya wa Mtibwa Sugar akipaisha juu dakika sita baadaye na kuinyima timu yake nafasi nyingine ya kufunga.

Simba ilianza kasi katika kipindi cha pili, lakini kipa Tinocco aliwahi kutoa nje mpira wa kichwa uliopigwa na Meddie Kagere na kuwanyima mabingwa hao nafasi ya kupata bao dakika ya 49.

Simba ilikaribia kupata bao baada ya piga nikupige iliyotokea katika lango la Mtibwa Sugar kupitia kwa wachezaji wake, Nicolas Gyan, Chama na Mohammed Ibrahim, lakini nafasi hiyo iliota mbawa kutokana na mabeki wa Mtibwa Sugar kujilinda vema dakika ya 87.

**KWINGINEKO**

Wenyeji Yanga wakiwa katika Uwanja wa Taifa walikubali kufunga msimu kwa kipigo cha mabao 2- 0 kutoka kwa Azam F C na kuhitimisha msimu vibaya.

Nao African Lyon ambao walikuwa wakikamilisha ratiba kufuatia kushuka daraja mapema, walikubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Kinondoni MC kwenye Uwanja wa Chamazi, wakati Coastal Union ikiwa katika dimba lao la Mkwakwani ililazimishwa sare tasa na Singida United.

Kwa upande wa JKT Tanzania ikiwa katika Uwanja wake wa Meja Jenerali Isamuhyo iliibuka na ushindi wa mabao 2 - 0 dhidi ya Stand United ya Shinyanga.

Katika Uwanja wa CCM Kirumba, Mbao FC ililazimishwa sare ya bao 1 - 1 dhidi ya Kagera Sugar, hivyo kuungana na African Lyon kushuka daraja kutokana lipokutana na Stand United ilifungwa (head to head).

Mbeya City ikiwa katika Uwanja wake wa Kumbukumbu ya Sokoine, ililazimishwa sare tasa dhidi ya Biashara Mara United, wakati ambapo Mwadui FC nayo ikisubiri mechi ya mchujo kujua hatima yake Ligi Kuu msimu ujao kufuatia kuibuka na ushindi wa mabao 3 - 1 dhidi ya Ndanda.

Ruvu Shooting ilijinusuru baada ya kushinda bao 1 - 0 dhidi ya Alliance wakati Tanzania Prisons nayo ikiwa nyumbani iliibuka na ushindi wa mabao 3 - 1 dhidi ya Lipuli FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002